Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 17 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika(Mhe. Pius Msekwa Alisoma Dua)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Juu ya Hesabu za Halmashauri za Miji na Wilaya kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2002. *(Report of the Controller and Auditor General on the Local Authorities Accounts for the year ended 31st December, 2002).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 130

**Matumizi ya Makambi ya Wakimbizi wa Ukombozi**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni kudumisha kumbukumbu ya historia na mchango wa Tanzania katika ukombozi wa Bara la Afrika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeamua kuweka alama za kudumu kwa kujenga kituo ambapo majina ya wapiganaji wote waliokufa wakati wa harakati hizo yataandikwa; na kwa kuwa ni dhahiri kuwa kituo hicho daima kitawakumbusha Watanzania na watoto wetu, majukumu yetu na vizazi vingine vijavyo mchango wetu katika ukombozi wa Bara la Afrika:-

(a) Je, Serikali kwa kupitia Wizara husika kwa nini isiamue kutunza na kutumia kwa shughuli za kielimu majengo au maeneo yote yaliyotumika kama makambi ya Wakimbizi wa mapambano ya ukombozi wa Afrika kama vile Kambi ya Mgagao (Kilolo-Iringa), Nachingwea, Tunduru, Kongwa na Morogoro Mjini;

(b) Je, maeneo hayo yanatumikaje hivi sasa;

(c) Kwa kuwa baadhi ya wapigania uhuru wanayaona makambi hayo kama mahali pa "Hija" na kila wakija Tanzania hupendelea kufika katika maeneo hayo ili kujikumbusha walikotoka; Je, isingelikuwa vizuri kuzishirikisha nchi hizo katika kufikiria matumizi ya makambi hayo baada ya nchi hizo kupata uhuru ili kutunza historia ya ukombozi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli vyama mbalimbali vya ukombozi wa Afrika, baada ya nchi zao kupata uhuru zilikabidhi Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania makambi yapatayo 12 waliyokuwa wakiyatumia katika mapambano ya ukombozi wa nchi zao. Makambi hayo yanahusisha Kaole Bagamoyo *(FRELIMO),* Itumbi Chunya *(PAC);* Dakawa *(ANC),* Kidogozero Handeni *(PAC); Kongwa (ANC/SWAPO); Mazimbu (ANC/PAC); Mbeya (Airport) (FRELIMO-MPLA); Mgagao (ANC), Pongwe (PAC); Nachingwea (FRELIMO); Tunduru (FRELIMO);* Kingolwira na Madizini (Vyama vyote vya Ukombozi).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuyapokea makambi niliyoyataja hapo juu iliamua kuyatunza na kuyatumia kwa shughuli mbalimbali za maendeleo ya kijamii kutokana na mahitaji halisi ya sehemu ilipo Kambi. Kwa msingi huu isingekuwa vyema kuyatumia makambi yote katika shughuli za sekta moja tu ya elimu kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo zaidi ya asilimia 50 ya makambi hayo yanatumika kwa shughuli za kielimu.

(b) Mheshimiwa Spika, matumizi ya maeneo ya makambi hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Shughuli za kielimu:

* Kaole Bagamoyo - Sekondari ya wazazi;
* Dakawa - Chuo cha Ufundi *VETA, Dakawa High School* na Shule ya Msingi;
* Kongwa - Sekondari ya Kongwa;
* Mazimbu - Kitengo cha Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA);*
* Tunduru - Sekondari ya Masonya na Waheshimiwa Madiwani wa Tunduru wako pale juu ni mashahidi;
* Nachingwea - Shule ya Sekondari Matekwe;
* Kingolwira - Shule ya Sekondari ya Nelson Mandela; na
* Mbeya *(Airport)* - Shule ya Sekondari Samora.

(ii) Shughuli za Kijeshi:

* Kidogozero Handeni - Kambi ya JKT;
* Pongwe (Msata) - Eneo la Mafunzo ya Kijeshi.

(iii) Shughuli nyingine:

* Mgagao (Kilolo - Iringa) - Magereza;
* Itumbi Chunya - Iko chini ya Serikali ya Mkoa wa Mbeya.

(c) Mheshimiwa Spika, wakati wa makabidhiano ya maeneo ya makambi yaliyokuwa yakitumiwa na wapigania uhuru wa ukombozi wa Afrika hakukuwepo na mkataba wa masharti wa namna ya kutumia maeneo hayo. Hata hivyo, Serikali iko tayari na imekuwa ikiwapokea wageni kutoka nchi hizo kwa lengo la kutembelea maeneo hayo.

Aidha, wageni kutoka Zimbabwe, Namibia, Msumbiji na Afrika ya Kusini wamekuwa wakifika katika Kambi za Kongwa na Dakawa na kupokelewa vizuri.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sikusema makambi hayo yatumike kwa elimu tu. Mwaka 1964 wakati harakati za ukombozi ziko juu katika Bara la Afrika Hayati Mwalimu Nyerere aliamua kwamba Kongwa iwe ndiyo eneo ambapo vyama vyote vya wapigania uhuru vitumie kama Kambi yao ya mapambano. Je, isingekuwa vizuri pamoja na matumizi hayo unayoyasema Waziri tukaweka Kongwa kuwa ni mahali pa kumbukumbu kwa Afrika nzima kwa shughuli hizi ili vizazi vyetu vya baadaye viweze kutambua mchango wetu katika ukombozi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli hata *delegation* zilivyokuja kutoka Zimbabwe na nchi nyingine tumekuwa na mazungumzo nao na wamependekeza nao vile vile tujenge mnara wa kumbukumbu kwa historia hiyo maalum ya Kongwa. Kwa hiyo, mazungumzo tunaendelea na pengine wakati muafaka tukikubaliana hayo anayoyapendekeza Mheshimiwa Makwetta yanaweza yakafikiwa.

Na. 131

**Barabara Kati ya Gua na Ngwara na Wilaya ya Mpanda**

**MHE PAUL E. NTWINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kata za Gua na Ngwara zinapakana sana na Wilaya ya Mpanda; na kwa kuwa hakuna barabara inayounganisha eneo hilo na ile barabara ya Mbalizi-Kanga-Kikwajuni-Saza-Kapalala hadi Kininga; na kwa kuwa barabara toka Mbalizi-Kininga haipitiki vizuri na ile ya Kininga/Kapalala-Gua nayo ni mbaya sana na haijafanyiwa matengenezo ili iweze kupitika kwa urahisi:-

(a) Je, ni lini Serikali itaunganisha sehemu hiyo ili kuunganisha Wilaya ya Chunya na Mpanda na Mikoa ya Mbeya na Sumbawanga;

(b) Je, ni lini Serikali italijali eneo hilo ambalo lina utajiri mkubwa na hifadhi za wanyama za *Lukwati Game Reserve* na *Katavi National Park* kwa kutengeneza barabara zake ili iweze kuwavutia wawekezaji kwenye sekta za Utalii na Madini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul E.Ntwina, Mbunge wa Songwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbalizi-Kanga-Mkwajuni-Makongolosi na Saza - Kanga - Kapalala ni barabara za Mkoa na zinahudumiwa na Meneja wa Wakala wa barabara *(TANRODS)* wa Mkoa wa Mbeya. Barabara hizi zimetengenezwa zikiwa na mchanganyiko wa changarawe na udongo na zina urefu wa km 117.8 na nyingine km 97.8. Barabara ya Saza - Kapalala huchepuka kutoka barabara itokayo Mbalizi - Mkwajuni hadi Makongolosi katika Kijiji cha Saza.

Kwa upande wa pili, barabara kati ya Kininga hadi Gua na Kininga hadi Ngwala hizi ni barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Chunya. Kwa sasa Mikoa ya Mbeya na Rukwa haijaweka mkakati wowote wa kuunganisha sehemu hiyo inayopita katika Hifadhi za Wanyama za *Lukwati Game Reserve* na *Katavi National Park.* Kutokana na barabara hizi kupita kwenye hifadhi, Mamlaka inayostahili kuhudumia eneo hili ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii tutakaa pamoja na kuangalia jinsi gani tunaweza kushughulikia tatizo hili analolisema Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inalijali eneo hilo na imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kwamba barabara hizo zinafanyiwa matengenezo ili ziweze kupitika. Barabara ya Mbalizi - Mkwajuni - Makongolosi inapitika bila matatizo baada ya kufanyiwa matengenezo katika sehemu korofi. Barabara ya Saza - Kapalala imo kwenye mpango wa matengenezo baada ya mashimo kujitokeza kutokana na mvua. Mwaka wa fedha wa 2002/2003 jumla ya Shs.

288,739,00/= zilitengwa na mwaka 2003/2004 Shs. 112,507,420/= zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizi. Mchanganuo wa fedha na kazi zilizopangwa kutekelezwa katika miaka hiyo ni kama ifuatavyo:-

| Na. | Barabara | Mwaka/Kiasi | Mwaka/Kiasi |
|---|---|---|---|
| | | 2002/2003 | 2003/2004 |
| 1. | Mbalizi-Mkwajuni Makongolosi | 247,339,000/= | 93,693,000/= |
| 2. | Saza-Kapalala | 41,400.000/= | 18,814,420/= |
| | **JUMLA** | 288,739,000/= | 102,497,4200/= |

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini nina maswali la nyongeza.

Je, kwa kuwa sasa hivi Wilaya hazina fedha tena za kuweza kujenga barabara baada ya mapato mengi kupunguzwa. Ile barabara ya Kininga - Kapalala ni tatizo kubwa la wananchi na hasa kwamba tumbaku inalimwa sana kule. Je, atakuwa tayari kuangalia hii barabara na kuweza kusaidia Wilaya. Swali la kwanza? *(Makofi)*

Swali la pili, pamoja na kwamba barabara ya Mbalizi-Mkwajuni imetengenezwa yapo maeneo ambayo hayapitiki. Lipo eneo ambalo limejengwa na lami kilomita moja hivi. Sasa bado kwa mbele kuna mawe mawe. Je, anaweza kukubaliana na mimi kuongeza lami au sementi kama wanavyofanya maeneo mengine korofi katika nchi hii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la kwanza labda niseme kwamba inaelekea jambo hili la Serikali kutoa ruzuku Halmashauri ni kama vile bado linatuchanganya kidogo. Ni kweli Serikali imeondoa baadhi ya kodi na ushuru. Lakini imetamka bayana kabisa kwamba hivyo vilivyoondolewa vitafidiwa na Serikali Kuu na ndio zoezi ambalo sasa linafanyika. Kwa hiyo, kama hilo litazingatiwa basi tatizo analolisema kuhusiana na suala la kwanza ni jambo linaweza kuwa *accommodated* ndani ya mfumo wa utaratibu wa fedha zilizopo hivi sasa. Kwa hiyo, nina hakika kabisa Halmashauri ikijipanga vizuri bado inaweza ikatumia fedha hizo kuweza kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni kweli lazima tukiri kwamba pamoja na juhudi za Serikali za kujaribu kutengeneza barabara hizi lakini tukumbuke ili mradi ni tope tunatengeneza kwa udongo wa kawaida ni dhahiri kabisa kila msimu wa mvua kwa kweli unapowadia tutegemee kwamba kutakuwa na matatizo ya msingi yatajitokeza. Hata hivyo naomba tu tushirikiane na Mheshimiwa tujaribu kuwasiliana Halmashauri na kupitia Ofisi yetu tuone kama kuna namna ya kuweza kusaidia katika hiyo sehemu ndogo anayoizungumzia.

Na. 132

**Barabara ya Sirori Simba Rung'abure na Natta Mugumu**

**MHE IBRAHIMU W. MARWA (K.n.y. MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara za Sirori Simba hadi Rung'abure na ile ya Natta hadi Mugumu na Mto Mara hadi Mugumu ni za udongo na huharibika sana nyakati za masika kiasi cha kutopitika na hivyo kuwa kero kubwa sana ya usafiri kwa wananchi wa Serengeti:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya kero hiyo?

(b) Je, ni lini barabara hizo zitatengenezwa kwa kiwango cha changarawe na hatimaye lami?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitumika katika utengenezaji wa barabara hizo tangu mwaka 1997 hadi 2002?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara za Sirori Simba-Rung'abure (km. 45), Natta-Mugumu (km. 37) na mto Mara -Mugumu (km. 31) zimetengenezwa katika kiwango cha udongo na changarawe hivyo wakati wa mvua sehemu ambazo hazina changarawe huharibika. Serikali kwa kutumia rasilimali zilizopo tayari ilikwishaanza kushughulikia tatizo la usafiri katika barabara za Sirori Simba-Rung'abure, Natta-Mugumu na ile ya Mto Mara -Mugumu kwa kutenga fedha katika Bajeti yake kwa lengo la kuzifanyia matengenezo ya dharura *(spot improvement and emergency repair)* katika sehemu korofi. Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 Serikali ilitenga jumla ya Shs. 244.7 milioni na kiasi cha Shs. 193.44 milioni zilitolewa na kutumika. Mwaka 2003/2004 jumla ya Shs. 115.5 milioni zimetengwa kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara hizi.

(b) Mheshimiwa Spika, gharama ya kujenga km. 1 ya barabara kwa kiwango cha changarawe inakisiwa kuwa ni Shs. 18 milioni na kwa upande wa kiwango cha lami nyembamba ni Shs. 200 milioni. Kutokana na makisio haya, ni dhahiri kuwa ili Serikali iweze kujenga jumla ya km. 113 ya barabara hizo kwa kiwango cha changarawe inatakiwa itenge kiasi cha Shs. 2,034 bilioni na Shs. 22.6 bilioni kama ni kwa kiwango cha lami nyembamba. Serikali kwa sasa haina uwezo wa kutenga kiasi hicho cha fedha katika mwaka mmoja wa fedha. Serikali kulingana na uwezo uliopo itaendelea kutenga fedha ili kuzifanyia barabara hizo matengenezo ya kawaida kila mwaka na hasa kuimarisha sehemu korofi.

(c) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichotumika katika utengenezaji wa barabara hizo tangu mwaka 1997 hadi 2002 ni Shs. 334.9 milioni ambazo zimegawanyika katika mgawanyiko mbalimbali kuanzia mwaka 1997 mpaka 2002.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa matengenezo ya barabara hizi ambazo zimetajwa kila mwaka na bado tatizo hili limeendelea kuwepo Serikali haioni kwamba utaratibu huo sasa haufai ili iweze kuandaa fedha za kutosha angalau barabara hizi zitengenezwe kwa kiwango cha changarawe?

La pili, kwa sababu barabara hii ya Sirari/Simba ni barabara ambayo inaelekea kwenye mbuga za wanyama za Serengeti. Na kwa kuwa Serikali sasa inakamilisha ujenzi wa barabara ya Makuyuni/Ngorongoro kwa upande wa Arusha. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuhakikisha kwamba barabara ya Makutano kwenda *Fort Ikoma* inatengenezwa kwa kiwango cha lami ili iweze kuvutia watalii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Ujenzi sasa hivi inakamilisha barabara ya Makuyuni-Ngorongoro na tungependa kujenga kwa lami kuingia kwenye upande wa mbuga za wanyama lakini tulikwishapata msaada huo tayari tukaambiwa na wataalamu wa Maliasili kwamba wasingependa lami ijengwe ndani ya mbuga za wanyama. Wana sababu za msingi kabisa kwamba kutokana na uzoefu wa *South Africa* wanyama wana-*develop* magonjwa ambayo hayajulikani.

Kwa hiyo, nao sasa hivi wangengoja waone matokeo ya kule *South Africa* ni magonjwa gani yanayosababishwa na wanyama kula lami. Kwa hatua hiyo hatutajenga lami ndani ya mbuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo linakwenda na swali la pili juu ya Fort Ikoma. Ni mbuga ya wanyama mpaka tupate matokeo. Lakini tumepata msaada na bure tu wa kujenga. Wajapan walikuwa tayari kujenga lakini kwa kweli kwa sababu hiyo ya kwamba wanyama wana-*develop* magonjwa tunangojea matokeo na tukapata positive tutajenga.

Na. 133

**Matoleo ya Awali ya Kompyuta**

**MHE. SALOME J. MBATIA** aliuliza:-

Katika ulimwengu huu wa utandawazi na ukuaji wa habari mawasiliano na teknolojia, "kila kukicha" matumizi ya kompyuta yanakua kwa haraka na kupelekea kifaa hiki muhimu kuboreshwa "kila kukicha" na hivyo kufanya matoleo ya nyuma kuwa *"obsolete"* vitakuwa vingi mno:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa namna ya kuviharibu vifaa hivi kwa usalama na bila ya kuathiri mazingira?

(b) Je, Serikali inatoa wito gani kwa watumiaji wake - Wizara, Idara na kadhalika, wa mahali pa kuhifadhi hasa ikizingatia kuwa, sasa utakuta vifaa hivi *"obsolete"* vimewekwa tu sehemu mbalimbali za Maofisi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (UMASKINI) (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Mbatia lenye sehemu ya (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza ningependa nitoe maelezo ya awali kwa kusema kwamba katika miaka ya mwaka 1990 kumekuwa na ongezeko kubwa sana la uzalishaji na matumizi ya vifaa vya elektroni kama vile kompyuta, televisheni, mashine za kutoa nakala na simu za mkononi. Teknolojia ya kutengeneza vifaa hivi nayo imekuwa ikibadilika kila mara na kusababisha matoleo ya awali kupitwa na wakati na hivyo kuwa taka.

Baadhi ya maunzi *(materials)* zinazotumika kutengenezea kompyuta ni kama vile metali za shaba, risasi, zebaki, *cadmium* na *zinc* ambazo zina madhara kwa mazingira na kwa afya ya binadamu. Kwa mujibu wa Mkataba wa *Basel* unaohusu kudhibiti usafirishaji wa taka sumu baina ya nchi na nchi na utupaji wake *take* zenye metali za aina hii zinatambulika kama taka sumu. Mkataba unahitaji taka za aina hii zitupwe kwa kufuata taratibu zisizo na madhara kwenye afya ya binadamu na mazingira. Tanzania ni mwanachama wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbatia lenye sehemu ya (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa wakati huu, Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingine zinazoendelea haina teknolojia inayokubalika ya kuangamiza vifaa hivyo. Katika baadhi ya nchi zilizoendelea teknolojia ya aina hiyo ipo. Mikakati iliyopo ni ya kuhifadhi vifaa chakavu katika hali ya usalama bila kuathiri mazingira na afya ya binadamu.

Aidha, utaratibu wa kurejeleza vifaa vya elektroni hapa nchini kwa sasa hivi haufanyiki kutokana na kutokuwa na Teknolojia inayofaa.

(b) Watumiaji wanatakiwa kununua vifaa vyenye ubora unaotakiwa na ambavyo vinaweza kufanyiwa matengenezo kirahisi *(upgradable equipment).* Kwa kufanya hivyo mtumiaji atabadilisha vitu vichache tu

ili kifaa cha zamani kiendelee kutumika badala ya kutupwa. Vifaa vichakavu vinatakiwa kuhifadhiwa vizuri sehemu ambapo havitaendelea kuharibika na hivyo kusababisha uchafuzi wa mazingira. Aidha, natoa wito kwa viwanda kuingia katika biashara ya kurejeleza vifaa vya elktroni ikiwa ni pamoja na matoleo ya awali ya kompyuta ambayo yamepitwa na wakati.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kuna utaratibu wa baadhi ya wafanyabiashara kuagiza kutoka nje vifaa vya electronik ambavyo vimekwishatumika ambavyo vinajulikana kama mitumba. Je, Serikali inachukua hatua gani kuzuia biashara kama hiyo kwa bidhaa hizi za eletroniki ili zisiingie nchini kwa kuzuia kama ilivyoelezwa katika swali la msingi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (UMASKINI):** Mheshimiwa Spika, Serikali inao utaratibu kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Fedha ya kuvikagua vifaa ambavyo vinaingizwa nchini na hata hivi karibuni baadhi ya Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba hata magari yanayoingizwa ya mitumba hayaingizwi kiholela au kwa kichwa kichwa tu hivi hivi. Utaratibu unafanywa na ushauri alioutoa utazingatiwa katika kuhakikisha kwamba utaratibu huo unafuatwa ili kuzuia uletwaji wa vifaa kama hivyo na hata sheria ile ya *Dumping* vitu kama hivi vinaweza vikasimamiwa ili nchi yetu ilindwe na vifaa chakafu ambavyo vinaweza kuharibu mazingira.

**MHE. DR. BATLDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa baadhi ya vifaa hivi kama vya kompyuta pia vinapatikana kwa njia ya zawadi. Mfano mzuri sisi Wabunge akinamama tulivyopata zawadi kutoka *British Council.* Kwa vile kompyuta hizo zilikuwa chakavu, Je, Serikali itasemaje kwa haya Mashirika na hizi nchi zinazotoa zawadi ambazo ni chakavu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (UMASKINI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa vyotevyote vile mnakubaliana Mheshimiwa Dr. Batilda ni msomi aliyobobea na kuomba vitu sio vibaya lakini ombaomba ikizidi unaweza kutupiwa tupiwa vitu ambavyo pengine kule vinakotoka sio vilikuwa vinatumika lakini vinaweza vikatoka kwenye hifadhi kama hizi za kwetu. Umeomba wanasema sasa tutawapa nini. Mwezi uliopita tuliwapa sasa katazame kwenye stoo ndio wanawazolea kuleta huku. *(Kicheko)*

Ushauri wangu ni kwamba wale wanaopata misaada wawe macho na kuhakikisha hawapokei vitu ambavyo ni vichakavu ambavyo vinaweza kuleta madhara kwa afya za binadamu na mazingira. Tuwe macho. *(Makofi)*

Na. 134

**Ukosefu wa Elimu ya Biashara Kwa Wanawake**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa wanawake wengi Tanzania sasa wanao mwamko mkubwa wa kuendesha biashara ndogo ndogo ili kujipatia kipato kwa njia ya kuwa na miradi ambayo ikianzishwa mara hufa kutokana na tatizo la kukosa elimu ya biashara:-

(a) Je, Serikali inajua tatizo hili na kama inalifahamu imechukua hatua gani kuwasaidia wanawake kuwapatia elimu ya biashara.

(b) Je, wanawake wangapi ambao hufanya biashara nchi za nje na wanatoka mikoa ipi na ni biashara za aina gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inalifahamu tatizo hilo na kwa kutambua hivyo imekuwa ikisisitiza utoaji wa mafunzo ya biashara kwa walengwa wa mikopo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF).* Vile vile imekuwa ikishirikiana na Shirika Lisilo la Kiserikali la Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF)* kutoa mafunzo ya elimu ya biashara kila mwaka kwa wanawake wafanya biashara ndogo ndogo kutoka Wilaya zote za Tanzania Bara na Zanzibar, wanaoshiriki katika maonyesho ya Biashara ya Kimataifa. Kwa mfano kati ya mwaka 1996 na 2002 wastani wa wanawake 200 kwa mwaka walipewa mafunzo. Aidha, mfuko wa mafunzo kwa wanawake Tanzania *(TFTW)* uliokuwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ulitoa mafunzo ya elimu ya biashara kwa wanawake wafanyabiashara wapatao 97 ambao wameweza kuwafundisha wengine. Wizara pia mwezi Oktoba, 2003 iliendesha mafunzo ya elimu ya biashara kwa wanawake 60 kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Dodoma, Morogoro, Iringa, Tanga, Arusha na Kilimanjaro walioshiriki katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. ingawaje hatuna takwimu kamilifu kwa sasa kuhusu idadi ya wanawake ambao hufanya biashara nchi za nje, napenda nielezee kwamba, wanawake wanaofanya biashara nchi za nje hupitia njia nyingi tofauti kama ifuatavyo:-

Wapo ambao hupitia katika vyama mbalimbali. Kundi kubwa la wanawake wanaofanya biashara nchi za nje ni lile linalopitia Chama cha *Federeation of Association of Women Entrepreneurs of Tanzania (FAWETA)* ambao huuza batiki, mikeka, vikapu na bidhaa za ususi, vinyago, ushanga, *Gemstone Jewellery*, vikoi, khanga na vitenge. Wengine ni *TAWOMA* na *TAWE* wanaouza bidhaa mbalimbali za madini na Samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi lingine ambalo linakadiriwa kuwa kubwa ni wafanyabiashara wa mipakani yaani *Border trade* kutoka Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Mtwara ambao huuza vyakula kama vile matunda, mchele, korosho na majongoo ya baharini. *(Makofi)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na najibu mazuri ya Naibu Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza je, taasisi za fedha ngapi zimekopesha wanawake wa Mkoa wa Mtwara mikopo ya thamani gani na wanawake wangapi wamefaidika biashara hiyo? Kwa kuwa wanawake wa Mkoa wa Mtwara wameitika wito wa kuanzisha biashara ndogo ndogo na kwamba Serikali haijawasimamia kupata soko hilo la uhakika, je, anajua hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, la kwanza linahusu takwimu kwa hiyo naomba alilete swali hilo aliloliuliza katika njia inayotakiwa ili tuweze kumjibu kikamilifu. Hilo la kwanza.

La pili, anataka kujua kuhusu soko kwa ajili ya akina mama wa Mtwara. Nimejibu katika swali langu la msingi kwamba, masoko yapo na ninafurahi kusema kwamba ninakumbuka Mtwara wana Shirika hili la *FAWETA,* Viongozi wa Mtwara wako mstari wa mbele katika kutafuta masoko kwa ajili ya Wanawake wa Mtwara. Kwa hiyo, ninaomba wawe nao ili waweze kupata masoko hayo, lakini tutakuwa tayari kusaidiana nao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tumesikia akina mama wa Mtwara. Akina mama wa Pemba je? Mheshimiwa Faida. Samahani, Mheshimiwa Waziri anataka kutoa majibu ya nyongeza.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuongezea majibu mazuri sana yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kumjibu Mheshimiwa Lydia Boma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka jana mwishoni nilipata fursa ya kutembelea Kituo chetu ya Biashara kilichopo Uingereza na nilileta taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge, hususan Waheshimiwa Wabunge Wanawake, kueleza fursa za masoko zilizopo kwa bidhaa mbalimbali hususan bidhaa za korosho na bidhaa zinazotengenezwa kwa mikono. Taarifa hizo nilizisambaza kwa Waheshimiwa Wabunge Wanawake ili waweze kusaidia vikundi hivyo. Lakini kama Mheshimiwa Lydia Boma hakupata, basi nitakuwa tayari kutoa tena taarifa hizo. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mbali na elimu inayotolewa madarasani, ya mambo ya biashara kwa wanawake, lakini njia nzuri zaidi pia ni ile ya study tour kwa wanawake kupelekwa nchi mbalimbali kama Bangladesh, Nairobi (Kenya) na nchi nyingine zozote ili kuona wenzao wanafanya nini. Je, hapa Tanzania ni wanawake wangapi ambao wamepelekwa *study tour* kwa mwaka wa 2003/2004? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Halitokani na swali la msingi, lakini Mheshimiwa Waziri naona anayo majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, tutaomba swali hilo lije kwa utaratibu wa kawaida ili tutoe takwimu. Lakini kwa hali ilivyo hivi sasa tunafahamu kwamba Serikali kwa kushirikiana na Serikali za nje imekuwa ikitoa fursa hiyo na katika kipindi kilichopita tunafahamu kwamba baadhi ya vikundi vya wanawake vilishiriki katika hiyo wanayoita *tour* huko Marekani kuangalia ni fursa gani zipo katika soko la *AGOA* na tunaamini kabisa kwamba hilo limekuwa likifanyika, siyo kupitia Serikali tu, hata kupitia Vyama vya Wafanyabiashara.

Lakini kadri fursa zitakapojitokeza, basi tutajielekeza kwa makundi mbalimbali ili nao wapate fursa ya kupata masoko zaidi ya bidhaa zao. *(Makofi)*

Na. 135

**Kuwatambua Watoto Yatima**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA** aliuliza: -

Kwa kuwa UKIMWI ni janga la Taifa ambao unaendelea kuua nguvu kazi muhimu ya Taifa na kuacha mamia kwa maelfu ya watoto yatima nchini na wengine kukosa wazazi wote wawili na kusababisha watoto hao kukosa matunzo mazuri, elimu na kukosa afya nzuri.

Je, Serikali inao mpango gani madhubuti na wa makusudi wa kuweza kuwatambua watoto yatima wa nchi nzima wenye matatizo kama niliyoyataja na kuwaandalia namna bora ya kuwahudumia kuliko utaratibu wa sasa wa makazi ya wachache yaliyopo ya kuwahudumia?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe, kama ifuatavyo: -

Nakubaliana na Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, kuwa ni kweli UKIMWI ni janga la Taifa na linasababisha kuua nguvu kazi muhimu ya kitaifa na kuacha maelfu ya watoto yatima ambao wengi wao wanakosa huduma ya matunzo, malezi, elimu, afya na ulinzi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya maisha magumu wanayoishi watoto hao, Wizara yangu kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii, ilifahamu hali za watoto hao na kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)* iliandaa mpango na mikakati ya kuwahudumia watoto yatima pale walipo *(Community Based Care).* Katika kutekeleza mpango wa mikakati hiyo, tayari Wizara yangu imeanza zoezi la kuwatambua watoto yatima na walio katika mazingira magumu zaidi kwa kushirikisha jamii husika.

Kwa kutumia mikakati hiyo, jamii zimeweza kuwatambua watoto yatima na walio katika mazingira magumu zaidi kwa kutumia vigezo ambavyo vimewekwa na jamii zenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)* imefanya zoezi la kuwatambua watoto yatima na walio katika mazingira magumu katika Wilaya 10 za Bagamoyo, Karagwe, Kisarawe, Makete, Musoma Vijijini, Magu, Jijini Mwanza, Bunda, Masasi na Singida. Aidha, kwa kushirikiana na Kampuni ya Madawa ijulikanayo kwa jina la *Abbott Laboratories and Pharmaceutical* chini ya Shirika la *Axios Foundation,* imefanya zoezi kama hilo katika Wilaya tatu za Rungwe, Manispaa ya Mbeya na Muheza. Jumla ya watoto 25,029 yatima na walio katika mazingira magumu wametambuliwa katika Wilaya 13 hapa nchini.

Katika kutekeleza zoezi la utambuzi huo mambo yafuatayo yamefanyika:-

* Kuhamasisha jamii na Viongozi wa Wilaya katika suala zima la malezi na matunzo kwa watoto yatima na walio katika mazingira magumu.

* Kuunda Kamati za kuwahudumia watoto hao katika ngazi mbalimbali.

* Kuunda mifuko ya kuwahudumia watoto yatima katika ngazi za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, jitihada zinaendelea kufanyika ili zoezi la kuwatambua watoto yatima na walio katika mazingira magumu liweze kufanyika katika Wilaya zilizobakia. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa, Serikali inachangia jitihada zinazofanywa na Wahisani kwa kushirikisha jamii, Halmashauri za Wilaya, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Dini na watu binafsi katika kuhudumia watoto yatima na walio katika mazingira magumu kwa kuwapatia huduma za msingi.

**MHE. KHALIFA MOHAMMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Ninamshukuru na ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pamoja na majibu hayo, nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni vigezo gani ambavyo vinatumika katika kuwatambua hao watoto yatima.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyowekwa na jamii katika zoezi la kuwatambua watoto yatima na walio katika mazingira magumu zaidi hutofautiana kati ya jamii na jamii nyingine. Hata hivyo, baadhi ya vigezo hivyo ni viwili kama ifuatavyo: -

* Wale ambao wazazi wao wote wamefariki na hawana ndugu au jamaa wa kuendelea kuwalea; na

* Wale ambao wazazi wao wote wamefariki na hawakuacha raslimali yoyote kama vile labda nyumba, mashamba na kadhalika.

Hata hivyo, Kamati zinazosimamiwa na jamii, za kuwahudumia watoto yatima zimekwishaundwa katika Wilaya hizo 13 nilizozitaja awali na zipo katika maeneo yote ambayo watoto hao wametambuliwa.

Na. 136

**Elimu kwa Wakulima wa Tumbaku**

**MHE. SAID J. NKUMBA (k. n. y. MHE. DR. JAMES A. MSEKELA** aliuliza: -

Kwa kuwa kilimo cha tumbaku kinahitaji elimu na taaluma ya uhakika zaidi na kwa kuwa wakulima wengi wa zao hilo huko Tabora Kaskazini wamelidhihirisha hilo na kufikiri juu ya umuhimu wa kupatiwa elimu mbali na ile ya mapokeo waliyonayo na kwa kuwa pamoja na kusaidia kuinua ubora wa zao lenyewe elimu itawawezesha kuzalisha tumbaku kulingana na mahitaji ya soko na hivyo kuwaongezea wakulima tija zaidi na kupunguza umaskini: -

(a) Je, katika siku zilizopita kumewahi kuwepo kwa juhudi rasmi za makusudi za kutoa elimu kwa wakulima wa zao hilo?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya kuanzishwa kwa program ya uhakika ya elimu kwa wakulima hao na itakuwa tayari kuwashirikisha wadau wengine wote katika suala hilo?

(c) Kwa kuwa kuna habari za kuwepo kwa juhudi binafsi za baadhi ya wanunuzi wa zao hilo kutoa elimu kwa wakulima. Je, Serikali inasema nini juu ya udhibiti wa zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Serikali inalipa umuhimu wa pekee suala la kutoa elimu kwa wakulima juu ya kilimo bora cha tumbaku. Katika ya mwaka wa 1950 na 1962, Serikali iliweka utaratibu uliowataka wakulima wa tumbaku kuhudhuria na kufaulu mafunzo ya kilimo bora cha tumbaku katika Shule iliyoitwa: *"Green Leaf School."*

Aidha, Wataalam wa Makampuni ya Tumbaku walitoa elimu ya kusimamia uzalishaji wa tumbaku kwa wakulima kuanzia kwenye kitalu hadi sokoni. Wizara imekiteua Chuo cha Kilimo cha Tumbi kilichopo Mkoani Tabora, kutoa mafunzo ya astashahada ya kilimo cha tumbaku. Chuo hicho pia kimeanza kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu uzalishaji bora na tumbaku kulingana na mahitaji ya soko. Tangu mwa 1977 hadi mwaka wa 2002 jumla ya wakulima 1,304 walipatiwa mafunzo katika chuo hicho.

Aidha, mwaka wa 2000/2001, Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku *"Tobacco Research Institute of Tanzania (TORITA)* ilitoa mafunzo ya muda mfupi ya kilimo bora cha tumbaku kwa wakulima 120 kutoka Vijiji vya Uyogo, Wilayani Urambo, Ugowola, Uyui na Mitowo Wilayani Sikonge. Taasisi hiyo itaendelea kuandaa na kutoa mafunzo hayo kwa wakulima wengi zaidi. Bodi ya Tumbaku vile vile hutoa mafunzo ya kilimo bora cha tumbaku kwa wakulima kwa njia ya Redio Tanzania, kupitia kipindi cha 'Tumbaku ni Utajiri' ambacho hurushwa kila siku ya Jumanne ya pili na ya nne ya mwezi kati ya saa 11.45 na saa 12.00 jioni.

(b) Bodi ya tumbaku imeandaa program ya miaka 10 ya kuendeleza Sekta Ndogo ya Tumbaku. *Program* hiyo inalenga kutoa elimu kwa wakulima kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni pamoja na Halmashauri za Wilaya, Makampuni ya Ununuzi, Chama Kikuu Kilele cha Tumbaku na Vyama Vikuu vya Ushirika. Serikali itaendelea kuboresha huduma za elimu ya ugani na kutoa mafunzo kwa wataalam na wakulima kwa kushirikiana na wadau wote.

(c) Makampuni ya Tumbaku yameajiri jumla ya wataalam 80 kwa lengo la kutoa elimu kwa wakulima katika maeneo ya Tabora, Sikonge, Urambo, Chunya, Mpanda, Kahama na Bukombe. Elimu hiyo huratibiwa na Bodi ya Tumbaku ili kuhakikisha kuwa inakuwa na manufaa yaliyokusudiwa. Aidha, ili kuondoa tofauti ya elimu iliyotolewa baina ya Wataalam wa Serikali na wale wa Makampuni binafsi,

Wizara ya Kilimo na Chakula imeandaa mtaala wa mafunzo rejea utakaotumika kufundishia Wataalam wa Tumbaku wa Serikali na wa Sekta binafsi.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kumekuwa na maelezo yanayopingana (maelezo haya yanawapotosha sana wakulima) juu ya matumizi ya pembejeo na nafasi za upandaji wa zao la tumbaku kati ya Wataalam wa Makampuni na Wataalam wa Serikali na kwa kuwa Serikali inalitambua hili; je, mmeishafanya utafiti na kujua ni wataalam gani wanaowapotosha wakulima? Ni Wataalam wa Makampuni ya Tumbaku au ni Wataalam wa Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Kwa kawaida Serikali hufundisha watu wake kwa makini na haitakiwi ipotoshe, hasa wale wa ugani na ndiyo maana tuna Chuo. Lakini vile vile, katika jibu langu la msingi nimeeleza wazi kuwa, sasa tutakuwa na mtaala mmoja wa mafunzo ambao utatumika kote kote. Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba uwe na subira mtaala utakapoanza matatizo haya yatatafutiwa ufumbuzi.

Na. 137

**Uchimbaji wa Bwawa la Maji Ulyanyama**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza: -

Kwa kuwa eneo la Ulyanyama lililopo kwenye Kata ya Sikonge limeshafanyiwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya uchimbaji wa bwawa litakalotumika kutoa maji kwa ajili ya shughuli za kilimo cha umwagiliaji kwenye bonde lililopo kwenye eneo hilo: -

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi huo?

(b) Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufika Sikonge kuona eneo hilo na kutilia mkazo ukamilishaji wa mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba; Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Eneo la Ulyanyama, lililoko kwenye Kata ya Sikonge lilifanyiwa tathmini ya awali na wataalam kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula tarehe 10 Novemba 2003, ili kubaini kuwepo kwa eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Tathmini hiyo ilibaini kuwa iwapo bwawa na miundombinu yake vitajengwa, eneo la hekta 250 litafaa kwa kilimo cha umwagiliaji mashambani.

Kutokana na tathmini hiyo, zinahitajika Shilingi milioni 40 kwa ajili ya maandalizi ya mradi, Shilingi milioni 245 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na Shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa mifereji, banio na vigawa maji.

Wizara inatafuta fedha za kuandaa na kutekeleza mradi huo. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge inashauriwa kuomba fedha za kutekeleza mradi huo katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2004/2005, kupitia Mpango wa Wilaya wa Kuendeleza Kilimo yaani *District Agricultural Development Plan (DADP).*

(b) Nitakapotembelea Mkoa wa Tabora, nitakuwa tayari kutembelea maeneo na miradi yote nitakayopangiwa kutembelea, ikiwa ni pamoja na Mradi wa Umwagiliaji Maji Mashambani wa Ulyanyama.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kuuliza kwamba, kuna baadhi ya miradi ya umwagiliaji baada ya kuanzishwa inaonekana ina maji ya chumvi na kisha miradi hiyo huachwa. Iliwahi kutokea Ruvu Mferejini kule Same na sasa naambiwa hapa Hombolo Dodoma na kuna baadhi ya maeneo mengine. Je, miradi hii huwa inaanzishwa bila utafiti wa kutosha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kawaida miradi hii inapoanzishwa utafiti unafanyika, lakini kama unavyojua, hali ya hewa hubadilika. Kwa mfano, mwaka huu ukame uliotokea haufanani na wakati mradi huu ulipoanzishwa. Kwa hiyo, tatizo la Hombolo mwaka huu limeonyesha kwa hali ya juu zaidi kuliko ilivyokuwa wakati wa nyuma. Mara nyingi ikinyesha mvua nyingi huzamisha zile hali za chumvi na hali huwa ya kawaida. Lakini utafiti hufanyika kwa makini zaidi. Sasa, ikitokea chumvi imezidi mno ukitumia maji hayo kwa umwagiliaji unaua ardhi kwa sababu *salinity* ni adui wa ardhi.

Na. 138

**Baraza la Ushauri wa Madini**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali ya Tanzania inaunga mkono kuendelezwa kwa majadiliano baina ya Viongozi wa Sekta ya Madini na kwa kuwa Uongozi wa *Tanzania Chamber of Mines* unasubiri kuundwa kwa Baraza la Ushauri wa Madini *(Mining Advisory Council)* ambalo litakuwa chombo cha kuangalia masuala kadhaa yanayojitokeza mara kwa mara: -

(a) Je, Baraza hilo litaundwa lini ili kukabili mapungufu yanayojitokeza katika shughuli za uchimbaji madini nchini katika kutatua migogoro?

(b) Je, kama Baraza hili halitaundwa ni kitu gani kinachokwamisha makubaliano ya kuundwa Baraza hilo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard N. Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chombo ambacho tayari kimeundwa hapa nchini ni Kamati ya Ushauri wa Madini kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 1998, chini ya kifungu Na. 20 ambacho kinataka iundwe Kamati ya Ushauri wa Madini *(Mining Advisory Committee).*

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge hili Tukufu kwamba, tangu mwezi Machi 2001, Kamati hii tayari ilikwishaundwa na Mheshimiwa Rais alimteua Meja Jenerali (Mstaafu) Godfrey Mang'enya, kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilianza kazi mara moja ambapo imekuwa ikishauri pamoja na mambo mengine ufumbuzi wa migogoro mbalimbali.

Licha ya kuchunguza na kushauri ufumbuzi wa migogoro ya madini, Sheria ya Madini imeainisha majukumu mengine ya Kamati kama ifuatavyo: -

* Kumshauri Waziri maeneo yanayofaa kutengwa kwa ajili ya uchimbaji mdogo mdogo ambao ni kwa Watanzania tu. Kamati imekuwa ikilitekeleza jukumu hili na imefanya hivyo kwa eneo la Nyamtukuza Wilayani Kibondo na Muheza;

* Kumshauri Waziri katika utoaji wa leseni maalum *(Special Mining Licences);*

* Kumshauri Waziri leseni za madini za kusitisha kwake ama kuzifuta baada ya kupitia maelezo ya utetezi ya mwenye leseni; na

* Kupendekeza viwango vya mauzo nje ya nchi ambavyo wafanyabiashara wa madini wanapaswa kufikia kwa mwaka ili waweze kuhuishiwa leseni kwa kipindi kipya.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini pia suala la msingi ni kwamba, nilikuwa najaribu kutafuta suluhu na namna gani tuweze kusikilizana kwenye mizozo hii ya uchimbaji madini. Sasa, ningependa tu kufahamu kwamba, Wizara inachukua hatua zipi kurekebisha Sheria ya Madini ili iweze kupunguza mizozo hii kwa sababu sasa hivi taratibu ni kwamba Kamishna wa Madini anaingia kwenye eneo la madini na kuanza kufanya kazi pale bila hata kuwasiliana na wenyeji au Wilaya hiyo ambako anakwenda kufanya kazi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niliarifu Bunge kwamba, Kamati hii ya Ushauri wa Madini imekuwa ikijihusisha na ufumbuzi wa migogoro ikiwa ni pamoja na migogoro ya fidia ya Nyamongo, mgogoro wa Geita, mgogoro wa uchimbaji wa madini Wilayani Mpanda na sehemu nyinginezo ikiwemo Mererani Arusha na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la kupitia upya sheria na kutazama upya namna ya utekelezaji wa Sheria ya Madini ya Mwaka 1998, napenda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua Kamati maalum aliyoiteua kufuatia ahadi aliyoitoa hapa Bungeni wakati wa Bajeti ya 2003/2004, ambayo kazi yake ni kutazama upya masuala mbalimbali ya utekelezaji wa Sheria ya Madini na suala zima la madini na ningewaomba Waheshimiwa Wabunge tusubiri matokeo ya kazi ya Kamati hii ambayo itasaidia katika kutazama masuala mbalimbali yanayohusu mambo ya madini.

Na. 139

**Umeme kwenye Jimbo la Nanyumbu**

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza: -

Kwa kuwa umeme wa Masasi unahudumia Wilaya ya Nachingwea hadi Ruangwa Mkoani Lindi, Newala hadi Tandahimba na Masasi hadi Ndanda Mkoani Mtwara na kwa kuwa umeme huo bado unaonekana kuwa wa kutosha na uhakika: -

(a) Je, ni lini umeme huo utapelekwa kwenye Jimbo la Nanyumbu na baadaye kwenda hadi Tunduru?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kupatikana kwa umeme kwenye Jimbo la Nanyumbu kutafungua milango kwa wawekezaji wa viwanda kama vya mbao na vya kusindika mazao hivyo kuleta ajira zaidi kwa Wananchi wa Jimbo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Mwananche Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Wilayani Tunduru kuna mitambo ya kuzalisha umeme kama ile ya Masasi. Hata hivyo, katika mpango wa kufikisha umeme wa uhakika katika Mikoa ya Kusini ni matarajio yetu kwamba Tunduru watatarajiwa kufaidika pia na umeme wa aina hiyo, jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru amekuwa akilifuatilia kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kupeleka umeme Nanyumbu inabidi kujenga njia ya umeme ya msongo 33 kutoka Masasi mpaka Nanyumbu umbali wa kilomita 108, kufunga *transformer* na kujenga njia ndogo za

umeme na jumla ya Shilingi bilioni 2.9 zitahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kama ambavyo tumekuwa tukisema, miradi hii yote Serikali inaitilia maanani na endapo fedha zitapatikana basi miradi kama hii ukiwemo huu wa Nanyumbu utatekelezwa.

(b) Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kupatikana kwa umeme kwenye Jimbo la Nanyumbu ni muhimu sana na kutafungua milango kwa wawekezaji wa viwanda kama vile vya mbao na vya kusindika mazao na hivyo kuleta ajira zaidi kwa Wananchi wa Jimbo hilo.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mji mdogo wa Mangaka uko kilomita kama 50 hivi kutoka Masasi, kwa nini basi umeme huu usianzie angalau kwenye Mji mdogo wa Mangaka ili Taasisi na Wananchi ambao wako pale nao waweze kufaidika?

(b) Kwa kuwa kuna kigugumizi juu ya umeme gani upelekwe kwenye Mikoa ya Kusini hasa ya Lindi na Mtwara na kwa kuwa nchi jirani ya Msumbiji ina umeme wa ziada. Je, Serikali sasa itafikiria kuvuta umeme kutoka Msumbiji na kupeleka kwenye Mikoa hii ya Kusini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusu Mangaka, napenda nirejee jibu langu la msingi tu kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kufikisha umeme kwenye maeneo muhimu kama hayo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Ukweli ni kwamba, utekelezaji wa azma hii unategemea upatikanaji wa fedha na katika kipindi kigumu hiki ambacho tunacho kwenye suala zima la uzalishaji umeme nisingependa kutoa ahadi ambayo haitekelezeki. Isipokuwa, napenda nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, pale ambapo patatokea uwezekano wa kupata fedha, maeneo kama haya ya Mangaka yanafahamika Wizarani na katika Shirika la Umeme *TANESCO* kwamba ni maeneo muhimu ya kufikishiwa umeme.

(b) Kuhusu kigugumizi, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kweli Serikali haina kigugumizi juu ya umeme gani ufike Mikoa ya Kusini. Kinachoangaliwa ni unafuu wa aina ya umeme utakaofika kwa sababu hatimaye mtumiaji wa umeme ndiyo ambaye anaweza akabeba mzigo mkubwa kutokana na utekelezaji wa mradi ambao hauzingatii unafuu wa upelekaji umeme kwenye maeneo husika na hili ni suala la kitaalam na ndiyo maana huwa kunakuwa na kazi kubwa inayofanywa, ya upembuzi yakinifu na mengineyo ili kuhakikisha kwamba watumiaji wa umeme wanapata umeme kwa gharama ambazo zinakubalika.

(c) Juu ya kupata umeme kutoka Msumbiji, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imefanya uchunguzi na mazungumzo na wenzetu wa Msumbiji, hakuna uwezo huo wa umeme kutoka Msumbiji kwa ajili ya Mikoa ile ya Kusini kwa maana ya Mtwara na Lindi.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri, napenda kumuuliza swali moja la nyongeza.

Ndiyo, ni kweli kigugumizi hicho cha Serikali kinazidi kupungua, lakini katika Bunge hili hili wakati wa Bajeti, Serikali iliahidi katika eneo hilo hilo kuhakikisha kwamba inanunua majenereta kwa ajili ya Mwena, Chikundi, Chigugu, Namakongwa na kadhalika. Utekelezaji wa ahadi hii ya Serikali unakwenda taratibu mno.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuliahidi Bunge hili kwamba, mradi huu utakuwa umekamilika ifikapo mwezi Juni tarehe 30 kama alivyokuwa ameahidi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ilitolewa ahadi ya kupeleka umeme, ya kushughulikia maeneo mahsusi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, siyo haya ambayo amezungumza ya kuweka majenereta katika kila kituo. Kuhusu utekelezaji wa ahadi hiyo, mwaka wa fedha bado haujaisha na ningemuomba Mheshimiwa Mbunge kwa yale maeneo yake yeye ambayo aliyataja yaliyokuwa yakimsibu afanye subira.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa ni Kikao cha Bajeti ndogo muda wa maswali umekwisha. Sasa tunaendelea na shughuli nyingine kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni tangazo la vikao vya Kamati. Kamati tatu zimepangiwa kukutana leo kama ifuatavyo:-

Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Simba, anaomba kikao kifanyike leo tarehe 17 saa saba mchana, ukumbi wa 428 ghorofa ya nne.

Kamati ya pili ni ya Miundombinu, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Mgombelo, anaomba Wajumbe wakutane ukumbi Namba 231 *Wing C* ghorofa ya pili mara baada ya kumaliza shughuli za Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza. Lengo ni kukutana na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Uongozi wa Shirika la Reli Tanzania. *(Makofi)*

Kamati ya mwisho iliyopangiwa kukutana leo ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba wajumbe wa kamati hiyo, wakutane leo tarehe 17 Februari, 2004 saa saba mchana katika ukumbi 219 ghorofa ya pili. Mwisho wa matangazo ya vikao vya kamati.

Sasa maelezo kuhusu ratiba ya shughuli za leo. Ofisi yangu ilighafilika kuweka katika *Order Paper* shughuli ambayo inakamilisha kufikiria makadirio ya nyongeza nayo ni ule Muswada unaohalalisha makadirio hayo kisheria, inaitwa *Supplementary Appropriation Act.* Kwa hiyo, tumetengeneza *Order Paper* ya nyongeza inayoweka *item* hiyo. Ili kazi ya Bunge iweze kukamilisha ya kufikiria makadirio lazima Muswada huo vile vile ufikishwe.

Kwa hiyo, tutakapomaliza mjadala Waziri atawasilisha Muswada wake huo na kwa mujibu wa kanuni, ule hauendi kwenye kamati inapita katika hatua zake zote mfululizo tu kwa sababu ni kuidhinisha yale yaliyobadilika na Bunge tayari. Kwa hiyo, tafadhali mpokee *Supplementary Order Paper* ambayo itafuata. Mjadala bado unaendelea, lakini utakamilika tutaingia kwenye hatua hiyo ya pili. Halafu ningependa kueleza vile vile kwamba kuna Wabunge wengi, wanasubiri kujadili hotuba ya Rais, kwa hiyo, tumepanga kwamba haya tunayofanya sasa yatakamilika mnamo saa sita na robo ili Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuwasilisha hoja ya kujadili hotuba ya Rais ndiyo ratiba ya leo. Tunaendelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza kwa Mwaka 2003/2004

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza nianze tu kwa kusema *Supplementary Budget* ni kitu ambacho kilikuwa kinategemewa. Lakini niseme tu labda kuomba *Supplementary Budget* siyo hoja, lakini ni matumizi ya hiyo pesa ambayo itatolewa na pia ni kuangalia *priorities* ambazo zipo.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo kama Msemaji wa Upinzani alivyosema, nakubaliana nayo na kuna mengine ambayo bado tutayatilia mashaka na tutaendelea kuyapinga mpaka dakika ya mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la *TANESCO* kuombewa *Supplementary Budget* na huku tukijua kabisa kwamba *TANESCO* ni shirika la biashara sioni popote pale umuhimu wa kupewa fedha ya Serikali, ili iweze kujiendesha. Kwa sababu nakumbuka pale mwanzo tuliposema tunakabidhi uongozi wageni ndiyo waliendeshe hilo shirika maana ilikuwa ni kwamba kuniwapunguzia mzigo Watanzania wa kuliendesha shirika hilo ili liweze kuendeshwa kwa faida. Sasa hatuoni sababu gani tena watu ambao tulitegemea wao waliendeshe kwa faida tuwaongezee fedha ya kuweza kuliendesha, tena badala ya kuonyesha kwamba baadaye tutarudisha Serikalini kwa riba tunawapa tu ili waweze kujiendesha na kukaa pale. Kama ingekuwa ni hivyo wale waliokuwepo kwanza na wenyewe tungewaongezea bilioni hizo 37 wangeweza kuliendesha bila hata kuagiza watu wengine kutoka nje kuliendesha hili shirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili tungeangalia basi ni ipi ambayo ni *priority* kwa wakati huu, *priority* ya nchi kwa wakati huu sidhani kama ni shirika la umeme kuliendesha, sidhani kama *priority* nchini kuwa na Ndege ya Rais ya kununua 40 billion. Mimi nilikuwa nafikiri *priority* ya nchi hii kwa leo hii ningeulizwa mimi ningesema ni njaa. Watu nchi nzima kila kukicha tunasikia wanakula mizizi, kila kukicha tunaambiwa tunasikia njaa, Mheshimiwa Mbunge, jana alilalamika jana wamekunywa uji, hajui leo watakula nini hiyo ndiyo ingekuwa *priority.* 40 billion ningekuwa mimi na kwa sababu wanafikiri kwamba zinalipwa kwa *installment* ningesema hiyo 40 billion inunue chakula cha kuwatosha Watanzania wote kwa vipindi vya miaka miwili, mitatu kwa sababu hatuna uhakika hata mwakani kama tunaweza kuwa na chakula. Kwa hiyo, 40 billion hii ingetumika kununua chakula cha Watanzania cha kuwatosha hata kama miaka miwili, miaka mitatu. *(Makofi)*

Lakini hiyo priority ambayo imewakwa hapa mimi inanishangaza kwa sababu nikiangalia hata Wilaya ya kwangu tu ya Bariadi pamoja na kwamba imetajwa kwamba ni Wilaya ambayo ina upungufu tu wa chakula na kwamba chakula kilichopelekwa Baridi kilikuwa kinatosha tu kwa watu 1,000 kama Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anatoa *briefing one time* anasema aliambiwa na *DC* wa Bariadi kuna familia 1,000 tu ambazo zimeathirika na zinahitaji chakula, ukweli ni kwamba Wilaya ya Bariadi ina njaa. Familia 1,000 zilizotajwa ni za uongo kata karibu tatu, nne, tano hazina chakula na kwa sababu mwaka jana kipindi kama hiki ambacho watu wa Bariadi walikuwa wanategemea wapate mvua ya kutosha na wapate chakula watu wale hawakupata mvua kabisa, hawakupata hata kilo moja ya mahindi, hawakupata hata kilo moja ya mchele na pamba ambayo labda ingeweza kuwasaidia kununua chakula na yenyewe ilikauka kabisa. Kata za Nkoma, Kata za Ng'waubingi, Kata za Somanda, karibu kata 8 za Wilaya ya Bariadi zilikuwa ni kavu kabisa hazikuweza kupata chakula. Sasa nashangaa hiyo ripoti ambayo ilipelekwa Serikali ikisema kwamba kuna *only 1000 vulnerable families* ni *families* gani hizo zilipata. Hizi ni takwimu ambazo ni takwimu za kufikirika. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba *priority* ya kwanza kwa hii *Supplementary Budget* ambayo tumeambiwa hapa ingekuwa inanunua chakula na hizi ten billion wangeifuta, hii 40 billion ambayo wameiomba kununua ndege ya Rais ambayo sioni *urgency* yoyote ile wangeipeleka kwenye chakula. Suala la njaa siyo suala ambalo tunaweza kulifikiria tu kwamba tunaweza tu kwamba tunaweza tukapeleka chakula kidogo kidogo. *(Makofi)*

Suala la reli kuongezewa fedha mimi nakubaliana nalo. Lakini hiyo reli ya kuongeza tu shilingi 2.4 billion mimi naona ni kidogo sana kwa sababu reli yenyewe ni mwaka 1896, mwaka 1914 ndiyo itapita natumaini Kigoma. Ni reli ambayo imezeeka natumaini hata yenyewe kama suala la kwamba tunataka tuwasaidie Watanzania ambao wanaishi kanda ya Kaskazini ambao sasa wanaathirika na njaa na matatizo kibao, mimi nilikuwa nafikiri hiyo, shilingi milioni 37 ambayo inapelekwa kwenye umeme pamoja na *part of the ten billion* ambayo tumesema milioni 40 tukanunue chakula *ten billion* ile ingekwenda pia kuimarisha reli ili watu wangu wasombewe chakula leo hii, imesemekana kimekwama sijui Dar es Salaam, sijui kimekwama Dodoma kiweze kusafirishwa kwa watu wa Mwanza, Bariadi, Mara chakula kwa uharaka zaidi kwa kutumia reli ya Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi leo nilikuwa nataka niwaambie kwamba *priorities* za nchi hii siyo kununua ndege, *priority* ya nchi ya leo hii ni watu wana njaa *they need food.* Kama kuna mtu unategemea kwamba atakuwa mstaarabu hutapata ustaratibu wowote ule hata kama ungekuwa ni nani ukaenda na ndege ukashuka pale ukawakuta watu wana njaa hata kukupokea hawataweza kukupokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasoma kwenye gazeti wanasema Mheshimiwa Rais alisema yeye hahitaji hii ndege labda mpaka baadaye, wakashawishi kwa Rais anayekuja. Lakini hata huyu Rais

anayekuja, unapewa ndege mpya ya 40 billion uende wapi wakati watu wa masasi hawana umeme wa uhakika, wakati watu wa Newala hawana umeme wa uhakika, watu wa Kigoma hawana umeme wa uhakika, watu wa Kibondo na Kasulu kila siku wanalia umeme hakuna, wewe unataka ndege ya fahari ya nini? Peleka umeme kwa watu wa Kibondo, peleka umeme wa uhakika kwa watu wa Kusini, peleka umeme wa uhakika kwa watu wengine, 40 billion mwaka jana nilisema Shirika la Umeme Zanzibar ilipe fedha ya *TANESCO* ili waendeleze umeme kusini, Serikali ika- *deal* sijui walifikia wapi na leo tena narudia hii fedha yote ingetumika kujenga umeme wa uhakika kwa watu wa Kusini. Hata yule Rais angekwenda kwa *Land Rover* angekwenda na gari yoyote watu wangempokea kwa fahari zaidi kwa sababu wana uhakika wa mambo mengine chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda kwa leo niishie hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nikumbushe tu kwamba Kanuni za majadiliano zinakataza kurudia rudia yaliyokwisha kusema sasa hayo ya ndege yameshasemwa.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza mchango wangu nitumie nafasi hii kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake mahiri ambayo aliitoa katika Bunge hili siku ya tarehe 12 mwezi huu, hotuba ambayo ilikuwa nzito na ilikuwa ndefu au ya marathon kitu ambacho mimi nimefarijika kuelewa kuwa kweli Rais wetu bado ana nguvu imara. Kwa vile sitapata nafasi ya kuchangia hoja ya kujadili hotuba ya Rais, basi naomba nitamke kuwa ninaiunga mkono hotuba hiyo kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu moja kwa moja kwa suala la njaa. Janga la njaa limekuwa kubwa sana kwani sehemu kubwa ya nchi yetu imekumbwa na njaa. Sisi ambao tunasafiri mara kwa mara katika maeneo kadhaa tumejionea jinsi mazao yalivyokuwa yamekauka, kwa kweli hali inatisha. Licha ya hali hiyo Serikali imekuwa inasisitiza kuwa hali siyo mbaya sana kwa sababu zifuatazo; sababu ya kwanza ni kuwepo kwa chakula cha kutosha nchini na sababu ya pili, ni kuwepo pengo dogo ambalo Serikali iliamini kuwa wafadhili wangeweza kusaidia. Sababu ya tatu ni kuwepo mipango mizuri ya kufikisha chakula kwa wanaokihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamini kuwa kwa maandalizi yaliyokwishafanywa hakuna mwananchi ambaye angekufa kwa njaa. Serikali ilipanga kugawa chakula kulenga makundi matatu ya watu. Kundi la kwanza ni chakula cha msaada na hiki kingetolewa kwa wazee, wasiojiweza, watoto na walemavu. Kundi la pili, chakula cha nguvu kazi nacho kingetolewa kwa watu wenye uwezo wa kufanya kazi, lakini hawana uwezo wa kununua. Kundi la tatu, tuliambiwa kuwa chakula kingetolewa kwa ajili ya biashara. Kwa hiyo, watu wenye pesa wajinunulie.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kuwa katika jimbo langu la Nanyumbu au Wilaya ya Masasi, tulibahatika kupata chakula cha aina moja tu, nacho ni cha biashara. Chakula cha msaada hakikupatikana, hali kadhalika chakula cha nguvu kazi. Chakula cha biashara kilikuwa nacho cha aina mbili kwanza ni kile cha bei nafuu ambacho kiliuzwa shilingi hamsini kwa kilo moja ya mahindi na chakula kingine ni cha wafanyabiashara ambao waliuza kwa bei holela hakukuwa na control yoyote ya bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chakula cha bei nafuu kililetwa kidogo mno katika Jimbo langu ni asilimia tatu tu ya walengwa ambao walipata chakula hicho. Lakini walio wengi hawakupata. Chakula cha biashara kiliuzwa kwa bei ya juu sana licha ya kusema chakula hiki kingine kilitoka kwenye Hifadhi ya Chakula ya Taifa na kingine kiliagizwa na wafanyabiashara baada ya kusamehewa kodi mbalimbali, lakini bado kiliuzwa kwa bei ya juu na sehemu nyingine hadi kufikia shilingi mia nne kwa kilo moja ya mahindi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya yote hayo ni makali ya njaa kuwa makubwa zaidi hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi. Wapo wananchi waliopoteza maisha yao kwa njaa na wapo wengine ambao kwa kweli wameathirika kiafya kutokana na kula majani, mizizi kwa muda mrefu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwanza ifute kauli yake ya hakuna atakayekufa kwa njaa kwani tayari vifo vimetokea. Mimi binafsi silaumu Serikali kutokana na hilo na hasa nikijua kuwa tatizo la njaa lilikuwa kubwa kiasi ambacho kwa Watanzania peke yake tusingeweza kulidhibiti.

Kwa hiyo, kwa Serikali kushindwa kuwasaidia wananchi wake walioathirika ni kitu ambacho hakiepukiki na hasa pale *response* ya wafadhili ilikuwa si nzuri na ilikuwa imechelewa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nieleze tu kuwa tatizo la njaa ndani ya nchi yetu linaeleweka sana. Wabunge tumekuwa tunatoa tahadhari ya njaa humu Bungeni, lakini bila ya kupewa uzito unastahili na Serikali kwa visingizio kuwa watalaam mbalimbali wanapita vijijini kufanya tathmini ya hali ya chakula.

Sasa je, ni tathmini gani hiyo inayosababisha wananchi wetu wafe kwa njaa? Naomba Serikali iache kupuuza tahadhari za njaa zinazotolewa na Wabunge kwa sababu Wabunge ndiyo walioko karibu sana na wananchi na wanapita kila kijiji na wanajionea hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo mdogo, mimi sina matatizo na takwimu ambazo zimetolewa kwa hiyo, ninaunga mkono hoja hii moja kwa moja. Lakini mwisho nikishukuru tena kwa kunipa nafasi hii na naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa suala la njaa ni kurudia tu yamesemwa vya kutosha.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kukushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hoja hii ya Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza bila kuchelewa nataka niseme wazi kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia sina matatizo. Sina tatizo la Serikali kununua ndege, sina tatizo la Serikali kupata fedha kwa ajili ya chakula kwa sababu kuna maeneo mengi katika jimbo langu vile vile kuna tatizo la chakula kwa hiyo, sina tatizo na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nijielekeze katika eneo moja tu ambalo linahusu pesa ambazo zinaombwa kwa ajili ya umeme. Kwanza nawahurumia sana wenzetu wa *TANESCO* kuingia katika kulipia gharama kubwa ya umeme na ndiyo sababu umeme katika nchi yetu ni wa bei kubwa na usio na uhakika. Sasa unaweza kujiuliza tatizo ni nini? Katika kipindi kirefu kumekuwa na ukosefu wa mwelekeo na mtazamo wa Wizara hii ya Nishati na Madini, ambao ungeielekeza nchi hii katika kutumia nishati rahisi na ya uhakika kwa kutumia rasilimali tulizonazo sisi wenyewe. Nasema kumekuwa na kipindi kirefu cha kutokuwa na mtazamo huo kwa sababu sasa hivi timu iliyoko pale Wizara Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mtazamo wao sasa unatia matumaini makubwa kwamba wanaelekeza juhudi zao kutumia raslimali tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia 68 ya umeme wetu unatokana na maji. Uzoefu umetuonyesha kwamba chanzo hiki sasa siyo cha uhakika kwa sababu kuu tatu.

Moja mvua hazina uhakika kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili vyanzo vya maji vinavyotumika kwa ajili ya kuzalisha umeme vinatumika na wakulima katika kilimo cha umwagiliaji maji. Mkulima wa kawaida ukimwelezea juu ya kuacha kulima ili maji yaende kuzalisha umeme hawezi kukuelewa kwa sababu yeye anahitaji chakula na katika hali ambayo kuna ukosefu wa chakula vyanzo hivi vya maji sasa vitatumiwa zaidi katika kilimo cha umwagiliaji maji.

Lakini la tatu huwezi ukapima na ukaweka makadirio ya uhakika ya kiasi cha maji kitakachokuwepo kwa ajili ya kuzalisha umeme. Mchango wa umeme duniani kwa chanzo hiki cha maji ni asilimia 6 tu. Asilimia 6 ya umeme duniani kwa wastani unatokana na chanzo cha maji. Kwa hiyo, utakuta kwa kweli sisi kutumia asilimia 68 kama chanzo cha umeme wetu katika maji ni kukosa kabisa dira ambayo inaweza kuwa ya uhakika zaidi.

Kama nilivyosema na Mheshimiwa Waziri ameliona hili kuna haja ya kubadilika katika mtizamo ambao utatusaidia sisi kama taifa. Asilimia 32 ya umeme wetu unatokana na mafuta, *diesel* na mafuta ya ndege. Uzoefu umeonyesha vile vile kwamba hakuna nchi yoyote duniani ambayo inazalisha umeme kwa kutumia mafuta ya ndege. Kwanza kuendesha ndege kumetushinda itakuwaje tuweze kusukuma mashine zile kwa kutumia mafuta ya ndege?

Lakini uzoefu vile vile umeonyesha kwamba bado kama taifa hatuna uwezo wa kukabiliana na majanga kama yale yaliyotokea Ubungo kwa sababu pale ni dhahiri kama iliyoonyesha kwamba ilikuwa na tatizo kabisa la namna ya kujikinga na ajali kama zile za moto. Jawabu la uhakika la umeme wetu ni ule unaotokana na makaa ya mawe.

Sasa mimi nilikuwa nataka nitoe takwimu kidogo hapa. Marekani inatumia asilimia 55 za umeme wake kutoka makaa ya mawe, Afrika Kusini inatumia asilimia 95 kutokana na makaa ya mawe, India inatumia asilimia 70 kutokana na makaa ya mawe, Urusi asilimia 75 kutokana na makaa ya mawe, China asilimia 80 kutokana na makaa ya mawe, Australia 70 kutokana na makaa ya mawe, Uingereza 60 kutokana na makaa ya mawe, Denmark asilimia 90 ya umeme wake unatokana na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, kule wanakwenda km ishirini, km kumi na tano chini kutafuta makaa ya mawe. Kwa hiyo, utakuta umeme unaotokana na makaa ya mawe duniani kote umeonyesha kwamba ni umeme wa bei poa, bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe takwimu tena hapa. *Capacity* charge kwa mwezi kwa umeme wa makaa ya mawe ya mchuchuma haitazidi dola za kimarekani milioni 4.4 kwa MW 400. Lakini Songosongo ambayo tunatarajia kuanza, itatoa *MW 150 capacity charge* yake ni dola milioni 6 za Kimarekani na umeme wa *IPTL* ambao ni MW 100 tu *Capacity Charge* yake ni milioni 2.8 dola za Kimarekani.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kwamba umeme wa makaa ya mawe hautazidi senti za Kimarekani 15 kwa *KW* moja kwa saa. Ukilinganisha na kiwango cha sasa cha umeme cha senti 15 za Kimarekani kwa hiyo utakuta umeme unaotokana na makaa ya mawe, hii ndiyo sababu ya msingi kwa nini duniani kote watu wanatumia mkaa wa mawe kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, mchuchuma peke yake ina hazina ya makaa ya mawe zaidi ya tani milini 527.8 *(potential).* Kama tukianza mradi wa mchuchuma utakuwa unatumia tani milioni 1.2 kwa mwaka kuzalisha *MW 400.* Sasa hesabu zinaonyesha kwamba kwa mwaka tutatumia tani milioni 1.2 kuzalisha *MW 400* je, tani 527 milioni ni miaka mingapi? Ni miaka mingi sana. Mimi hesabu zangu zinaonyesha kama ni karibu miaka mia tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utafiti wa mkaa wa mawe wa Mchuchuma sasa una miaka 40. Wajerumani wamefanya utafiti na wakamkubali, Waingereza wamefanya utafiti nao wakamkubali na sisi Makampuni fulani fulani yamefanya utafiti wakasema sawasawa. Lakini kama wenzangu walivyosema, mpaka sasa kazi hii haijaanza na makaa ya mawe haya yako juu juu hatujaanza kwenda chini kama walivyokwenda Urusi. Urusi wamekwenda chini kilometa 20 wanatafuta mkaa wa mawe. Mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba soko la umeme lipo, asiwe na wasiwasi. Soko la umeme lipo hapa ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba Bunge likubali kutoa hizi fedha za dharura ili *TANESCO* iendelee kutoa umeme lakini jawabu la kudumu kabisa ambalo halitaturudisha tena katika kuomba fedha za dharura kwa ajili ya umeme ni hili la kutumia umeme wa mkaa wa mawe na tunao.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, la kwangu lilikuwa ni hilo moja kukazia kwamba tusiwe na wasiwasi juu ya matumizi ya mkaa wa mawe na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri analiona hili na ametuhakikishia kwamba atalifanyia kazi na mimi namtakia kila la kheri ili asirudi tena siku nyingine kuomba pesa nyingine za dharura kwa ajili ya umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana..

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Christopher Wegga, usirudie rudie ya wenzako. *(Kicheko)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie kidogo na ni kweli sitarudia ya wenzangu, lakini kama pale panapohitaji kuboreshwa nitaomba unisamehe niboreshe kidogo maeneo hayo ya kurudiarudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze sana *TRA* kwa makusanyo mazuri pamoja na Wizara nzima ya Fedha na timu yake ya wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema kwamba wanaomba waongezewe fedha kutokana na janga lililotukuta; tunalo tatizo la ukame, kwa hiyo mambo mengi yameathirika na ukame. Kwa hiyo, tunaomba wenzetu waelewe ni kitu gani kinaombwa fedha, kwa nini zinaongezwa. Kwanza njaa tunapata kwa sababu ya ukame, umeme pia ni kwa sababu ya ukame, mabwawa yote yamekauka, fedha ya ndege ni kawaida. Sasa nashindwa kuelewa kwa nini watu wanapata shida kufahamu hili jambo hata fedha ya ndege tulishapitisha katika Bajeti iliyopita. *(Makofi)*

Hotuba ya juzi ya Mheshimiwa Rais ilizungumza suala la walevi wawili. Haya mambo yanaweza yakajirudia hata kwenye Bunge humu! Inakuwa kama walevi wawili wanauliza ule ni mwezi? Wanasema ule hapana, mtu mwingine anakuja anasema na wewe je, unauonaje ule ni mwezi? Anasema hapana mimi ni mgeni. Sasa humu Bungeni kunaweza kuwa na wageni wa Bajeti tuliyopitisha. *(Kicheko/Makofi)*

Naomba sana mkubali, halina tatizo ni suala kama anavyosema Mheshimiwa Spika, usirudie rudie, ila unasimama unapitisha. Mimi naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

Suala la ndege tumeshalizungumza na Mheshimiwa Profesa Mwandosya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi alifafanua. Kwa hiyo, hatuna haja ya kurudia. Wale ambao hawakuelewa jana nashangaa leo wanalizungumza. Bahati mbaya ndio mambo ya mwezi na jua na mlevi hayo na kukaa nyuma ya gari. Lakini kwa kweli fedha hii iongezwe na iende haraka sana kwa sababu yeye mwenyewe ameshasema ataacha mazingira ya kuruka, sasa ataruka na ndege ya zamani?! Ataacha mazingira ya kuruka, hata huyo Rais atakayekwenda kutumbukia baharini huko shauri yake. Yeye anaacha mazingira mazuri ya uchumi safi, siasa bora na ndio maana amesema kuna eneo hili la Vyama vya Siasa, tunavihitaji lakini visiwe na uongo, uongo utachelewesha mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la chakula, nimeshasema sana humu ndani, leo sisemi. Nimeshasema wezesheni Mkoa wa Morogoro. Simamieni pale Morogoro, limeni chakula kingi Mkoa wa Morogoro, chagueni Mikoa mitatu. Morogoro ile unaweza kulima mara mbili kwa umwagiliaji kidogo tu. Sasa leo tunazungumza kila mwaka njaa, wewe chakula unaweza ukakilima mahali pakavu? Kama watu wanafuga ng'ombe waacheni wafuge ng'ombe. Morogoro tunalima, tuacheni tulime. Sasa nyie mnachanganya wanaofuga na kulima. Sasa mtaweza kila mtu alime, kufuga, hii kazi ni ngumu sana!

Mheshimiwa Waziri tunaomba ukitoka katika Kikao hiki tukutane na Wabunge wa Morogoro, pale Morogoro na Mkuu wetu wa Mkoa Mheshimiwa Stephen Mwashishanga ameanzisha mambo mazuri sana kuhusu kilimo. Tunakuomba ufike pale. Mvua toka mwezi wa 11 zinanyesha nzuri tu. Ipo njaa maeneo madogo madogo lakini si kuzungumzia njaa humu watu wanakufa, watu wafanya nini, simamieni kilimo cha kisasa. Mheshimiwa Keenja, tulishasema mpeni hela, sasa mnamlaumu yeye, afanye nini? Ni suala la Wabunge kumpa Waziri hela! Sasa mnamlilia Waziri tupe chakula, atakitoa wapi? Hizi hela ndogo hamkuziona? Huu mwanzo mpeni hizo hizo kumi aangalie namna ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Wengine wanazungumzia fedha ya *STABEC*, sasa wewe unalima kahawa?! Fedha ya *STABEC* ni hela ya kahawa. Unajua kuna matatizo, ile fedha ilikuwa ni barabara ya sehemu zinazolima kahawa, kama Profesa Maghembe kule sawa akizungumza fedha hizo, Mheshimiwa Angwanile sawasawa, kule Moshi, Mbozi kule kwa Halinga hizo mngezungumzia sasa. Tunazungumza bajeti, wewe unazungumza hela ya barabara, imo humu? Matatizo kweli kweli! Waheshimiwa kwa suala la chakula, kiongezwe na tujihami kwa kulima wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la umeme nalo linahitaji mjadala. Umeme mwingi uko Morogoro, chunguzeni yale mabwawa mnayafanyaje? Mazingira, mmekata miti yote mkatengeneza mkaa mkapikia wenyewe, sasa mnalalamika. Pandeni misitu yote ya Morogoro. Kihansi tupande miti kwa wingi, Mtera kule kwa Mheshimiwa Dr. Samwel John Malecela, panda miti mingi sana, panda na kidatu vile vile tupate mvua. Mazingira, mnakata miti wenyewe sasa mnasema ooh, mabwawa hayajai, tukimbie mazingira haya ya kutumia umeme na maji. Mtaupata wapi umeme? Umeme ni Morogoro kwa kupitia maji mpaka tutakapoanza utaratibu, taratibu. Huwezi kuacha suala zima la umeme wa maji ghafla tu hivi hivi mnavyozungumzia nyie. Huo Mchuchuma mna miaka mingapi ninyi? Mnapohamia kwenye Mchuchuma mazingira mazuri ya kuweka maji katika mandhari nzuri, pandeni miti. Nimeshasema Mto wetu wa Ruaha upandeni miti kutoka Iringa unakoanzia na ondoeni watu wanaolima kwenye vyanzo vya maji, mmefanya hilo? Tunaiomba Serikali iwezeshe hata kupanda miti kwenye milima ile ya Vidunda, Kihansi na Uluguru. Kwa nini mnashindwa kuweka Bajeti hata ndogo tu kupanda miti katika milima ya Uluguru? Mvua nyingi iko pale. *(Makofi)*

Sasa mnahangaika sijui bwana maji haya yanatutoroka, hamna mawazo nayo kuyazuia? Kuzuia ni kupanda miti. Hawa wanaochoma mkaa hapo wapeni kazi nyingine. Wapeni utaratibu, kata mti panda mti. Hili linazungumzwa kila siku kata mti panda mti, lakini mnapanda? Mnayo mafungu?

Kwa hiyo, suala la umeme, mimi niko kwenye Kamati hii ya Umeme labda niseme kidogo kwenye umeme hapa. Umeme anaosema Mheshimiwa Waziri aongezewe fedha ni kwa sababu baada ya kwisha maji Mtera, Kidatu na Kihansi kwa kweli umeme unazalishwa kidogo sana. Mheshimiwa Rais juzi alizungumza hapa suala la kupungua maji. Sasa hata tukikataa si ndio tutakuwa giza zaidi? Mpeni fedha halafu mzungumze, hata huo wa Songo Songo mnaozungumza ndio fedha hiyo tunayoomba sisi kwamba tunaomba fedha hiyo itolewe ili Songo Songo mwezi Mei ianze kazi kuendesha mashine zilizoko Ubungo, kuongeza mafuta *IPTL.* Mafuta mengi yanatumika kwa sababu maji hayapo Kihansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi naunga mkono Wizara ya Nishati na Madini wapewe fedha ili tuweze kukabiliana na janga hili. Lakini pia tunaomba mtakapopewa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ajaribu kuendeleza lile suala la umeme Vijijini. Hawa Wabunge wanapiga kelele ni suala la kusema wakipata umeme Vijijini wote wanarudi Bungeni, sasa wanashindwa kulieleza vizuri. Ule umeme mliopeleka nguzo kila Kijiji mwaka 2000 haujatengenezeka. Hata mimi kwangu pale Kitete nimeshapitishiwa hela milioni 11 tu, sasa nategemea katika hizi milioni 40 nitamega pale Kitete umeme uende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ntwina kule kwake nguzo zipo barabarani tu kila mahali, sasa hili ndilo wanalolalamika, sasa wanashindwa kulichanganua vizuri kwamba unaposema umeme Vijijini. Je, umeme utakwenda kiasi gani kwenye Vijiji? Utekelezaji utakuwepo mwingi? Tutakapokwenda kuomba kura umeme utakuwa umeshafikia Vijiji vingapi? Nguzo zile zilizotupwatupwa kwenye Miji na Vijiji vidogo vidogo tumeshakubaliana kwenye Kamati kwamba kama ni aibu itatupata wakati wa uchaguzi mwaka 2003 ni zile nguzo zilizopelekwa Vijijini. Tunaomba waanze ili tunyamazishe hizi kelele. Lakini watu wa umeme wamefanya vizuri, wamekuta mtandano wa suala zima la Kampuni ya umeme ilikuwa ni pana sana, ilishindwa hata kuendesheka. Ndio wakaamua kwanza kuanza na zoezi la kupunguza watu. Wamepunguza na kulipa. Wamekuta utaratibu mzima unakoanza na unakomalizia haieleweki ndio maana wanasema sisi tuacheni tupunguze na kwa sababu hili janga limetukuta, Serikali tuongezeeni pesa kidogo. Sasa mnasema hapana, inakuwaje hii?

Mheshimiwa Spika, ingawa umesema tusirudierudie lakini sasa kama umeme lazima urudierudie. Naomba tuwe tunarudia maana yake wengine hawauelewi. Nashukuru sana. *(Kicheko)*

Suala la elimu, ni vizuri kwa kweli wanasema usipougharamia ujinga, gharama yake ni kubwa, maana yake utakufa na ujinga wako. Kwa hiyo elimu ipewe fedha ili tuendeleze kwenye shule zetu za Kata kupata mabati. Kwa mfano niombe tu kuainisha Sekondari zangu zinazojengwa za Kata. Tunajenga Sekondari pale Masanze, Zombo, Kata ya Ulaya na Kata ya Kidoli. Mheshimiwa Waziri wa Elimu anafahamu vizuri kwenye Jimbo langu Kata hizo hazijawahi kupata msaada mzuri wa mabati. Naomba hayo mabati kila shule hizo, mabati 200 ni mabati kidogo, jumla yake itakuwa mabati 600. Yeye ni Mtani

wangu ukifika pale Mikumi, Mheshimiwa Waziri wa Elimu basi na mimi nitakuwa nimeacha kumbukumbu kwamba nilisaidiwa na mtani wangu Mheshimiwa Joseph Mungai. Naomba hayo mabati, sisi tumeshajenga tayari bado kuezeka. Ni Mwana-CCM mwenzangu. *(Makofi)*

Nashukuru sana, makofi haya yanaashiria kwamba umekubali. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nisiseme mengi, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunisikiliza.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nawaita Mawaziri wasaidie kujibu hoja kabla ya kumwita Mtoa hoja mwenyewe. Namwita Mheshimiwa Waziri Yona, Waziri wa Nishati na Madini, atafuatia Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia mawili matatu kwenye hoja hii ambayo naiunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze kwa kuelezea hali ya umeme hivi leo. Taarifa tulizonazo ni kwamba maji kule Mtera leo yako Sentimeta 50 yaani nusu mita juu ya kile kiwango cha chini kabisa cha mita 690. Hali hiyo ni hali ya hatari sana kwa sababu yakishuka tu yakifika mita 690 basi itabidi tuanze kuchukua hatua nyingine ambayo ni kufungulia yale maji tunayoita *dead volume* ili tuweze kuzalisha umeme zaidi. Inavyoelekea ni kwamba mvua zinazonyesha kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, maji mengi yanaishia ardhini kwa sababu ya ukame na mengine yanatumiwa na wakulima ambao wako kandokando ya sehemu zile. Kwa hiyo, hali bado ni mbaya na kwa sababu hiyo, basi naomba Waheshimiwa Wabunge watupatie hizo fedha ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameziomba zisaidie *TANESCO* kuendesha na kuzalisha umeme katika miezi hii michache ijayo.

Mheshimiwa Spika, ukisikiliza Waheshimiwa Wabunge wanavyozungumza hapa ndani kuhusu umeme utakubaliana na mimi kwamba hili linatokana na ukweli kwamba ni asilimia 15 tu ya Watanzania wanafikiwa na umeme hivi sasa. Ndio kusema asilimia 85 wana kiu au hamu ya umeme na hao wanaowakilishwa na hawa Wabunge walioko hapa, kwa hiyo kero hizo ni kero ambazo ni za kweli na ni tatizo ambalo ni la kweli. Sasa kwa sababu gani tumefika hapa? Nitajaribu kuelezea kwa kifupi, lakini nitoe *facts* ambazo zitawasaidia Waheshimiwa Wabunge waelewe tuko wapi na tumefikaje hapa.

Ukweli ni kwamba umeme ni ghali sana kuupeleka mahali popote pale na hasa katika nchi kubwa kama hii. Lakini kama tungekuwa na uwezo wa kifedha katika Bajeti yetu, basi labda tungeweza kuufikisha umeme kwa haraka sehemu nyingi nchini humu. Hatuna uwezo huo, Bajeti yetu ni ndogo kama mlivyoona. *Development* Bajeti yetu, Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba ni tegemezi kwa kiasi kikubwa sana labda asilimia 80. Sasa kutokana na fedha zetu wenyewe, hatuna fedha za kutosha kusambaza umeme kila mahali kwa kasi ambayo tungependa. Kwa hiyo, imetubidi tutegemee misaada *(grants)*. *Grants* zinatokana na wafadhili wachache ambao wanataka kusaidia kwenye Sekta hiyo ya Umeme. Wafadhili wengi ndugu zangu wanataka kusaidia kwenye *social sectors* ambazo zinagusa *poverty eradication directly* na zipo kwenye *PRSP* yetu. Umeme wanasema ni sekta ambayo inaweza kuhudumiwa na *private sector*. Kwa hiyo, wanaotoa *grants* kwenye umeme ni wachache sana. *Spain* kwenda Ukerewe, bilioni nane naona Mheshimiwa Spika anatingisha kichwa, Sweden kupeleka Urambo na Serengeti na miradi hii ni umbali mfupi lakini utaona ni pesa nyingi sana.

Kwa mfano umeme uliokwenda Urambo na Serengeti ni bilioni tano kila sehemu. Kwa hiyo hata wafadhili nao ni wachache na fedha ni chache na wana masharti makubwa hutaweza kuamini. Pamoja na kwamba ni misaada utaambiwa ufanye hivi, usifanye hivi, *contract* usitoe kwa huyu, mikataba isainiwe na huyu, sheria gani itatumika wakati mkiwa na mgogoro, makandarasi wachaguliwe vipi, haya mambo yote yanachukua muda ndugu zangu. Hiyo ni *source* ya pili ya fedha tunazopeleka kwenye umeme, kwamba ni kutoka kwa wafadhili na ni chache.

*Source* ya tatu ni mkopo. Mikopo tunachukua toka *World Bank*, *African Development Bank,* nayo hii ni mikopo ambayo lazima tuiangalie. Tumepunguziwa madeni juzi juzi hapa. Kwa hiyo, tukikopa ni lazima tupate mikopo ambayo ni nafuu ili umeme uje uwe wa nafuu kwa watumiaji, lakini vile vile tuweze kulipa mikopo hiyo. Tusije tukalimbikiza madeni tena tukarudi kuwa nchi yenye madeni makubwa sana. Kwa hiyo, mikopo nayo sio mingi sana na ina masharti makubwa na makali kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine ni kitu tunaita *IPP (Independent Power Producers* au *Projects).* Hizi ni kama akina *IPTL,* akina Songosongo na akina Mchuchuma ambayo inazungumzwa hapa. *IPPs* ndugu zangu popote duniani ni miradi ambayo inakuwa financed na private sectors. Ni mtu ambaye ana fedha zake kutoka kwa *shareholders* wake anakuja kuwekeza ili apate faida. Sio msaada kama wa *SIDA,* sio mtu anayetuhurumia. *He is here to make money.* Kwa hiyo, mtu wa namna hiyo kama *IPTL, Songo Songo* ni lazima sisi Serikalini tukae tuzungumze naye kwa makini kabisa. Tusipofanya hivyo, tutatumbukia kwenye matatizo ya kuja kujitumbukiza kwenye deni kubwa ambalo kesho mtakuja kusema mlisainije hapa kwa haraka haraka hivyo? Ndio maana inachukua muda mrefu sana. Kutathmini miradi ya *IPP*

Lakini jambo lingine Waheshimiwa Wabunge, *IPP* wenyewe hizo fedha wanafanya kwenda kukopa huko nje, kwa hiyo hata mkielewana bado ni lazima waende wakazitafute huko nje, watafute na *terms* gani wanataka zile fedha na hizo hizo ndio wanazipitisha kwetu ili tuweze kuzalisha umeme au mradi uanzishwe utakaozalisha umeme na tuweze kuwalipa. Tunashindana kwenye hizo *terms* za *investment* wanazotupa. Mtu anakuambia anataka *rate of interest* ya 24 *percent,* huo umeme wewe utauuzaje kwa mlaji wa kule Same au kule Nanyamba au kule Mchambawima au kule Vijijini kwetu? Lazima tuwe waangalifu na ndio maana inatuchukua muda mrefu sana kuzungumza na hawa *IPP.*

Mheshimiwa Spika, lakini nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge na tumesikia hoja zao kwamba kwa kweli sasa tumefikia mahali ambapo ni lazima tuondokane na kutegemea nishati ambayo inatokana na maji. Hilo tunakubali kabisa na Wabunge wamesema, Mheshimiwa Profesa Mwaga pale amelizungumza sana, tunatoka huko, tunaelekea wapi. Kama tulivyosema kwenye Bajeti yetu iliyopita, tunaelekea kwenye *solar,* yaani jua, upepo, *gas* na makaa ya mawe. Hata *geothermal*, mvuke ambao unatoka ardhini tunautazama vile vile. Kwa hiyo, hayo mengine ya *solar, wind, gas* nitayazungumzia siku nyingine, sasa hivi ngoja nielezee Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mchuchuma ni muhimu sana sio Wizarani kwangu tu au *TANESCO* lakini hata kwenye *Mtwara Corridor. Mtwara Corridor* ambayo inatazama maendeleo ya Mikoa ya Kusini, kutoka Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mbeya mpaka Rukwa na Iringa, yote hiyo iko kwenye *Mtwara Corridor.*

Kwa hiyo, mradi huu ni muhimu sana na hilo linajibu lile swali la kusema kule Kusini labda tumekusahau, umeme wao utatoka wapi? Hii ni *source* mojawapo ya umeme ambao utapatikana kwa Mikoa ile ya Kusini. Hakuna ubaguzi katika kuendeleza miradi ya umeme. Wote hapa tuna *shortage* na niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba mimi Waziri wa Nishati Tanzania kwa miaka miwili iliyopita, Kijiji nilichozaliwa hakina umeme bado, Kata niliyozaliwa haijakuwa na umeme bado, Tarafa niliyozaliwa haijapata umeme bado. Sasa ningekuwa na uwezo wa kunyofoa kidogo, bila shaka ningepeleka kule kama kungekuwa na upendeleo. Lakini hakuna upendeleo, miradi hii inafuata taratibu. *(Makofi)*

Sasa kuhusu Mchuchuma tumefika wapi, naona dakika zangu zinakwenda. Imechukua muda lakini tulitaka tuwe makini ili tupate umeme wenye bei nafuu, bei nafuu kwa watumiaji. Hakuna hujuma yoyote, hakuna mfanyakazi wangu ambaye kwa kweli amekalia kwa makusudi pale Wizarani. Ni kwamba maswali ni magumu sana. Tunafanya kazi kitaalam kwa bidii kabisa, tunashirikisha wadau mbalimbali wa nje na ndani, Wizara nyingi, Wabunge ili tuwe na uhakika tunapata mradi ambao ni *affordable, energy* ambayo ni *affordable to the majority of our people* hapa nchini. Hatutaki matatizo ambayo tuliyapata *IPTL.* Naomba nieleweke hapo. Sisemi *IPTL* ni mradi mbaya, nasema *IPTL* ni *deal* mbaya. *IPTL* sio mradi mbaya, *it is a good project,* inayotuokoa sasa hivi na ndio *source* yetu ya *energy* na ni *standby* nzuri na imetufikisha mahali pazuri, tungekuwa katika hali mbaya sana. *But the deal,* wenzetu walikuwa sasa sijui nitasemaje, mimi nasema walikuwa wajanja wale *partners* walioleta ule mradi. Waliweka *terms*

ambazo ilibidi turudi Mahakamani kwenda kubishana ili tuweze kupata unafuu na kwa kweli tuliweza. Tumepunguza gharama ya mradi wa *IPTL* na sasa hivi *capacity charge* tunayoilipa, tunailipia kwenye *cost figure* ambayo ni ya chini kuliko ambayo walituambia hapo mwanzoni. Hii nawasifu wenzetu ambao walitutangulia wakaweka mikataba ambayo inaruhusu kuridhia mambo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Budget Paper* imepelekwa *Cabinet* kueleza Serikali kwamba mradi wa Mchuchuma tuuendeleze na tunasema tuuendeleze kwa hatua ambazo tuna-*afford.*

Leo nimepata barua hapa kutoka kwa wawekezaji wanaitwa Siemen, mkubwa wao anaitwa Smit. Nilimtafuta Mheshimiwa Simbakalia sikumpata lakini Smit ameniambia wawekezaji wa Mchuchuma wameshafika, wamezungumza na *TANESCO Board,* wamezungumza na *Tanzania CTI,* wamezungumza na Wadau mbalimbali kutengeneza kitu kinaitwa *Project Verification Document.* Hii ndio document ambayo itaonesha faida ya ule mradi.

Kwa hiyo, Profesa Mwaga nakushukuru kwa mawazo yako mazuri lakini hawajafikia bado *capacity charge* itakuwa kiasi gani. Itatokana na hiyo *Project Verification Document* ambayo inafanywa na wanakuja wiki ijayo ili izungumzwe na Wizara yangu, *TANESCO* na wadau wengine ambao wanahusika hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, niongezee tu kwamba watu wanasema kwa nini tunafanya hii *interconnection* kati ya Zambia, Tanzania na Kenya? Sababu ni kwamba dunia ya leo imefunguka. *Electricity is a commodity you have to buy. We are buying electricity right now* kutoka Kenya na Zambia kidogo kidogo sana. *But one day* tutakuwa na umeme wa kutosha ambao tunaweza kuuza.

Kwa mfano sasa hivi tunataka kuwauzia Kenya umeme kupitia Lungalunga, *Megawatt* chache tu. Lakini tukiwa na hiyo *interconnection* ambayo itaboresha *system* yetu hapa Tanzania, basi siku moja hata huu umeme wa Mchuchuma tukiuzalisha tutaweza kuwauzia Kenya. Kenya sasa hivi wanataka umeme *Megawatt 50. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa Mchuchuma nasema uko katika hali nzuri na tunazungumza na wawekezaji watakuja wiki ijayo tuone ni namna gani tuta-*implement* mradi huu kwa awamu. *Mnazi Bay* nayo tumeshasaini *Memorandum of Understanding* na wawekezaji gesi itoke pale ikatoe umeme Mikoa ya Kusini.

Lakini gesi ya Songo Songo itakuja Dar es Salaam mwezi wa Tano au wa Sita ambapo tutaubadilisha uwe umeme na ile mitambo pale ina uwezo wa kuzalisha *Megawatt 75* na tunaweza kuongeza. Ukiongeza chombo tu ile jenereta ipo, gesi ya kutosha kuzalisha hata *Megawatt 100* au *200.* Kwa hiyo, tunatokana na kutegemea maji, tunaingia kwenye kutegemea raslimali zetu ambazo ni za kujadidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nikimbilie ufafanuzi mwingine, hilo la Mchuchuma nadhani tumeelewana ndugu zangu, Bajeti yangu ikija Juni, niachieni ipite kwa sababu tunazungumza na wawekezaji vizuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie *Gold Audit.* Sheria yetu ya *Gold Assaying Ordinance* na *Mining Act* ya mwaka 1998 zote yanasema Serikali inaweza na inatakiwa ku-*appoint auditor* kuangalia jinsi madini yanavyochimbuliwa. Itaangalia *production,* itaangalia *quality* ya dhahabu au madini yanayotoka ardhini, (kwa sasa hivi ni dhahabu) na itaangalia gharama za uendeshaji wa hii migodi.

Mheshimiwa Spika, kule ndiko mambo yanakoweza kufanyika ya ajabu kabisa. Na huyu *Gold Assayes* ambaye ameshachaguliwa na alichaguliwa in *Open Tender* kufuatana na taratibu za tender za Benki Kuu, ameanza kazi na sasa ameingia kwenye ku-*audit operation costs* za hii migodi. Kule ndiko ambako tunaamini tutagundua kama tulikuwa tunadanganywa au vipi.

Mheshimiwa Spika, niliulizwa: Je, faida gani tutapata? Ukiwa na gari lako ukili-*insure* Shangingi lako ukalipa *One million Shillings a year insurance,* mwaka ukiisha unasema sikupata ajali*, there goes my one million shillings?*

Lakini unasema afadhali, maana ingetokea ajali ungeweza kwenda ukalipwa. Sasa sisi kweli kama tutazuia wasituibie, maana ni pesa nyingi, *the gold we produce every year is worth lot of money.* Hatutaki itokee udokozi au udanganyifu katika shughuli za kuendesha migodi yetu, ndio maana tumemweka huyu na tuta-*review* kila miezi sita, kila mwaka. Huu mkataba ni wa miaka miwili, tunau-*review all the time.* Baadaye tutauongeza labda utazame madini mengine pamoja na madini ya vito.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO (Net group); Net group* walikuja hapa kutusaidia ku- *bring in an up to date management into our parastatal,* tukubaliane hilo. Mashirika yetu yote yalikuwa yanaendeshwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Ohoo!

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, malizia maelezo yako.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Mashirika yetu mengi yalikuwa tunayaendesha sio kwa jinsi inavyotakiwa. Sasa *Net Group* walikuja wametusaidia kuongeza mapato, wametusaidia kupunguza gharama, wametusaidia kufundisha watu wetu. Mkataba wao wa ya miaka miwili unalipiwa na Sweden na tunau-*review* kila miaka miwili. Utafika wakati tutasema basi ahsanteni, ondokeni lakini kazi wanayoifanya ni nzuri, isipokuwa hali ya hewa ndio imetibua mambo mengi sana, sasa inabidi tuje hapa tuombe pesa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba *TANESCO* wapatiwe hizo fedha na kazi ya *Gold Assaying* nayo ipatiwe hizo fedha ili wananchi waridhike kwamba kweli Serikali inaangalia mapato tunayopata kutokana na madini. Hii ni pamoja na Kamati ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameianzisha jana ya kuweza kuangalia Sekta hii ya Madini.

Kero zote mlizozitaja Waheshimiwa Wabunge pamoja na kwamba sehemu gani ya mapato iende kwa wananchi kule iliko migodi, yote hayo yataangaliwa na hii Kamati ambayo itaongozwa na Dr. Kipokola aliyoizindua Mheshimiwa Waziri Mkuu jana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuendelea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi. Nimesimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, na napenda katika kuunga mkono nimpongeze sana kwa uhodari wake mkubwa ambao umewezesha maombi haya ya Bajeti ya nyongeza ayawasilishe Bungeni bila ongezeko lolote la kodi. Nampa hongera sana. *(Makofi)*

Pia napenda nimshukuru sana kwa maelezo mazuri aliyoyatoa kuhusu zile shilingi bilioni 2.424 zinazoombwa katika Bajeti hii au katika marekebisho ya mafungu aliyowasilisha Bungeni kwa ajili ya elimu. Napenda nichukue nafasi hii niwashukuru Wabunge wote waliochangia katika hoja hii kwa sababu hakuna hata mmoja aliyepinga zile bilioni 2.424 zinazohitajika kwa ajili ya elimu. *(Makofi)*

Lakini ningependa kuchukua nafasi hii kufafanua mambo mawili au matatu yaliyojitokeza katika mjadala ambayo naona yanahitaji ufafanuzi ili yaeleweke vizuri zaidi na sehemu kubwa yametoka kwa wenzetu wa Kambi ya Upinzani. Napenda niwashukuru Kambi ya Upinzani kwamba nao hawakupinga zile bilioni 2.424. Wameunga mkono vizuri. Lakini baadhi yao wamekosoa, wamekosoa visivyo, ambavyo ningependa kwa kweli kuweka rekodi ya Bunge hili sawasawa ningependa kutoa maelezo.

La kwanza ambalo wamekosoa wanasema imekuwaje Serikali hatukujua pale mwanzo tulipopanga Bajeti hata tufikie leo kuja kuomba nyongeza kwa ajili ya jambo ambalo tungestahili kulijua. Lakini ningependa wenzetu wa Kambi ya Upinzani waelewe kwamba katika mipango ya kisasa iliyo mizuri huwa inakuwemo dhana ya *monitoring and evaluation* kufanya tathmini kila wakati unapotekeleza mpango na mipango ya kisasa inahitaji iwe inaweza kubadilishwa kwa upesi kwa lugha ya Kiingereza wanasema mpango unatakiwa uwe *flexible. (Makofi)*

Ndiyo maana tuna mkakati huu katika Kanuni na taratibu zetu za kuendesha mambo kwamba inawezekana kuleta Bajeti ya nyongeza yaani *Supplementary Estimate* ni katika kutambua kwamba hata jambo ukilipamga vizuri namna gani unaweza ukahitaji kufanya mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, inafaa sisi wote tujue kwa vizuri zaidi nini kimetokea hata zikahitajika hizo fedha za nyongeza kwa ajili ya elimu. Mwaka wa kwanza wa MMEM ulikuwa ni 2002. Tunasema mpango wa MMEM ni 2002 mpaka 2006. Mwaka wa kwanza wa MMEM 2002 watoto waliofaulu mtihani wa darasa la saba waliongezeka kutoka asilimia 22 mwaka uliopita yaani 2001 mpaka asilimia 27 mwaka 2002, yaani baada ya hatua tulizochukua katika mwaka wa kwanza wa MMEM *pass rate* ilipanda kwa *point 5* asilimia, kutoka 22 mpaka asilimia 27.

Mwaka wa pili wa MMEM kufaulu kuliongezeka kutoka asilimia 27 ya mwaka wa kwanza wa MMEM mpaka asilimia 40.1 ukitoa ongezeko hilo ni asilimia 13.1. Ni kubwa zaidi, ongezeko limekuwa kubwa zaidi kuliko lile la mwaka wa kwanza kwa zaidi ya mara mbili na ni kubwa zaidi kuliko tulivyokuwa tume-*project* na ukichukua katika namba ya wanafunzi waliofaulu waliongezeka kutoka 133,000 mwaka 2002 mpaka 196,000 mwaka 2003. Wameongezeka 63,000.

Kwa hiyo, ongezeko hili kubwa tumelazimika kuongeza *in take* yetu, kuongeza wale wanafunzi wa kwenda katika Kidato cha Kwanza. Vinginevyo wangebaki wanafunzi wengi mno. Na inafaa pia tufahamu kwamba wanafunzi huandikishwa katika Sekondari zetu mwanzoni mwa mwaka. Bajeti mpya huwa inakuja mwezi wa saba, lakini *enrolment* ya wanafunzi katika shule zetu tunafanya Januari. Kwa hiyo, ndiyo maana imelazimika maombi haya ya nyongeza yasisubiri mpaka Bajeti ijayo. Yaje hapa kwa njia ya *Supplementary Estimate. (Makofi)*

Na hata sasa bado kutokana na kwamba sasa fedha zimepatikana Waheshimiwa Wabunge naona kuna kila dalili kwamba mnatupatia hizi fedha basi tutaweza kuongeza watoto wengi zaidi. Tunatarajia kuongeza watoto 18,000 katika *second selection* inayofanyika mwezi *March. (Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ningeshauri kuliko kulaumu, kuleta *supplementary* na kukosoa mimi ningeshauri kwamba sisi Wabunge wote wa Kambi zote mbili upande wa Serikali na upande wa Upinzani kwa kweli tuwapongeze sana Walimu wetu na Walimu Wakuu na Maafisa Elimu kwa kazi nzuri walioifanya hata tukaweza kupata matokeo haya mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nisahihishe dai lililotolewa hapa Bungeni na Kambi ya Upinzani kuwa Sera inayounganisha Elimu ya Msingi na ya Sekondari ni yao Kambi ya Upinzani. Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani alipokuwa anazungumza hapa Bungeni alitumia maneno yafuatayo na napenda ninukuu. Alisema: “Mheshimiwa Spika, kama sera ya elimu ya msingi ingeliunganishwa na sera ya elimu ya sekondari, kama ilivyo kwenye sera ya upinzani tungeweza kupanga vizuri zaidi na kuepukana na mtindo wa zimamoto”. Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Sasa dai hili ni la kusema sera inayounganisha ni sera ya upinzani. Napenda niwafahamishe wenzetu wa Kambi ya Upinzani kwamba sera ya Serikali ya CCM ni kupanga maendeleo ya elimu kwa mwelekeo wa kisekta yaani kwa lugha ya wenzetu lugha ya Kiingereza inaitwa *Sector Wide Approach.* Na hivi ndivyo tunavyopanga mipango yetu ya elimu. *(Makofi)*

Napenda nikumbushe kwamba katika hatua ya mwanzo tulianza *Education Sector Development Programme (ESDP).* Hii ilitazama ngazi zote za elimu kutoka elimu ya msingi, elimu ya sekondari, mafunzo ya ualimu, mpaka elimu ya juu. Sasa hii mipango inayokuja wa kwanza ukiwa ni mpango wa elimu ya msingi, ni utekelezaji wa ile *ESDP* ambayo *approach* ni *sector wide approach* na nimekwisha

sema kwamba Serikali imekamilisha sasa uaandaaji wa mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari ambao mambo yake kwa sehemu kubwa yatajitokeza katika Bajeti ya mwaka 2004/2005. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sahihi kwamba sera inayounganisha ni ya upinzani. Hiyo ni sera ya Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Ningependa pia nitoe ufafanuzi kuhusu MMEM. Mheshimiwa Spika, ningependa kutumia nafasi hii nifafanue kuwa mpango wa MMEM hautokani na msukumo wa Kambi ya Upinzani. Nimekwenda hivi karibuni, nimetembelea majimbo ya baadhi ya kambi ya Upinzani na nimekuta kule wametangaza kwamba ujenzi wa madarasa na ujenzi wa nyumba za walimu unaoendelea katika Wilaya zao ni kutokana na msukumo wa kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Napenda nifafanue kwamba hii siyo kweli hata kidogo. Mpango wa MMEM ni utekelezaji wa kifungu 54 cha Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu. Kwa hiyo, ningependa ninukuu, kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

"Katika kipindi cha uongozi wa CCM cha miaka mitano ijayo, Serikali kuzingatia haya yafuatayo:-

Moja, kukamilisha miradi yote ya ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, madawati, vyoo vya wanafunzi na kuendelea kuwahamasisha wananchi waendelee kujenga shule mpya za kutwa za sekondari kwa kila Tarafa au Kata". Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maneno hayo yanatoka kwenye Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Cha Mapinduzi na katika kuandaa Ilani hiyo hatukushirikiana na Vyama vya Upinzani hata kidogo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawashauri waache kudai kwamba MMEM inatokana na msukumo wa Kambi ya Upinzani. Katika jamii zetu udokozi ni tabia isiyopendeza katika jamii zetu. Sisi wote, kwa hiyo, napenda udokozi huu unaweza ukawa pia hata katika sera za vyama vya siasa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningewashauri wenzetu waache kudokoa dokoa sera za CCM na kusema ni za kwao kwa sababu tabia hiyo ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa nimalizie kwa kusema kwamba katika kipindi cha mpito tunachokiita sisi katika Wizara ya Elimu na Utamaduni kipindi cha mpito kutoka hapa tulipo mpaka tutakapoanza mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari. Tumejitahidi kupanua *intake* kupanua uandikishaji wa kidato cha kwanza kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

Kwanza kuongeza mikondo katika shule zilizopo kama shule pana mikondo miwili, tunashauri iongezwe mpaka minne ili mradi wananchi wako tayari wana matofali, wako tayari wanaweza kujenga ili mpango ule wa MMES utakapoanza tutawapa ruzuku ya maendeleo ya milioni saba kwa darasa waweze kujenga madarasa.

Mkakati wa pili Wizara imeidhinisha *double shift* ili wanafunzi waweze kusoma wengine asubuhi na wengine mchana katika kipindi hicho cha mpito ili mradi wako tayari kujenga madarasa mara mpango wa maendeleo ya elimu ya Sekondari utakapoanza.

Tatu: Tumeidhinisha pia katika baadhi ya shule kuzidisha wanafunzi darasani, badala ya wale 40 wanaoruhusiwa, nimeidhinisha waweze kuchukua mpaka wanafunzi 60 kwa muda wa miezi mitatu, minne kwa sababu mpango wa *Secondary Education Development Plan (SEDEP)* itakapoanza tutaweza kuwapa ruzuku waweze kujenga madarasa.

Nne: Tumeidhinisha pia katika kipindi cha mpito kufungua shule mpya kwa masharti ambayo tumeyalegeza badala ya kusema kila kitu kiwe tayari, tukikuta shule sasa wamekwishamaliza kujenga madarasa, wana ubao wa kufundishia wanafunzi, viti vya kukalia wanafunzi, vyoo vya kutumia wanafunzi,

hata kama maabara hazijajengwa, tunaidhinisha shule iweze kufunguliwa ili waweze kuchukua wanafunzi. *(Makofi)*

Sasa kinachofanywa katika bajeti hii ya nyongeza, Mheshimiwa Spika, ni kutupatia shilingi hizi bilioni 2.424 ili tuweze kuwaajiri Walimu kutokana na wanafunzi 41,000 wanaochukuliwa kwa mikakati hii. *(Makofi)*

Fedha hizi zitatuwezesha kuwaajiri walimu wenye vyeti, lakini pia tutawachukua vijana waliomaliza kidato cha sita na wamefaulu mitihani yao tutawapa mafunzo ya pedagoji yaani ile *method* ya mafunzo ya muda mfupi waweze kufundisha vizuri. Tutatangaza pia kuwaajiri baadhi ya vijana wetu ambao wana digrii zisizo za elimu, lakini wako mitaani humu, tutawachukua nao kuwapa mafunzo ya pedagoji ili wasaidie kufundisha. Kwa hiyo, fedha hizi zitatusaidia kuendesha mafunzo hayo kwa kuwaajiri walimu wapya na hao walimu ambao wao hawajapata mafunzo ya ualimu baada ya mafunzo ya muda tutawapa *teaching license* yaani leseni ya kufundisha ili tufute kabisa mapengo ya walimu katika shule zetu za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kumpongeza sana Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha vizuri sana haya marekebisho ya makisio na hasa hili la kutokuongeza kodi maana tungeongeza kodi sijui kama huku ndani kungekalika. Na haijapata kutokea marekebisho kama haya yasiendane na kuongeza kodi.

Naomba pia nichukue nafasi hii baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri, niipongeze pia *TRA* kwa kazi nzuri sana ya kukusanya mapato ya Serikali. Maana bila kuongezeka kwa mapato haya hata haya tunayozungumzia hapa Bungeni hayangekuwepo. *(Makofi)*

Lakini yote yanatokana na mwelekeo mzuri wa Serikali ya Awamu ya Tatu ya Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wetu wa Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingi zilizotolewa na kwa kuwa muda ni mfupi nitaomba nizungumzie kama hoja badala ya kwenda kwa moja moja ili niweze ku-*cover ground* kubwa zaidi kidogo.

La kwanza kabisa, ni lile alilolizungumzia Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, juu ya fedha za *STABEX.* Alitaka kujua hizi fedha ziko wapi, alikuwa anavihitaji akapangue mawe kule kwao ili waweze kupata barabara. Ningewashauri watafute maeneo ambayo hayana matatizo makubwa kama yale.

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Februari, 2004, juzi kilikaa kikao cha *Central Tender Board* kuupitisha utaratibu wa kumteua *Consultant* ambaye atasimamia matumizi ya hizi fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi kuteua barabara zitakazofaidika na fedha hizi. Wizara ya Ujenzi imepewa siku 30 kumaliza kazi za kumteua mtaalam huyo na baada ya mtaalam huyo kuteuliwa, kazi atakayofanya ni kupitia yale maombi yaliyotoka sehemu mbalimbali na kuangalia ni barabara zipi zitakazofaidika na fedha hizo. Hadidu za rejea kwa ajili ya mtaalam huyo zimeshaandaliwa zimeandikwa katika Kiingereza, Kiingereza kimeleta matatizo hapa Bungeni wakati huu. Lakini anayetaka kuziona anaweza kuja akazitazama. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, labda nilijulishe Bunge lako kwamba mpango huu ni mkubwa zaidi kuliko ule wa *STABEX,* wanachozungumzia *EU* ni makubaliano yao na Serikali ya Tanzania katika *paper* inayojulikana kama *Country Strategy Paper* ambayo inatoa *Euro 105* milioni kwa ajili ya kuendeleza sekta ya usafirishaji na katika hizi kuna *Euro 10* milioni ambazo zinatokana na *STABEX.* Kwa hiyo, kwa kweli fedha zinazozungumziwa ni nyingi zaidi na inawezekana ni kutokana na fungu hili kuwa kubwa zaidi na kuwa chini ya huu utaratibu wa *Country Strategy Paper* ndiyo maana halikuonekana na baadhi ya watu hawakuweza kulizungumzia.

Sasa katika hizi fedha za *STABEX* katika huu mwaka wa 2004 tutatumia bilioni 2 ama *Euro* milioni mbili, 2005 milioni nne na 2006 milioni nyingine nne jumla ndiyo hizo zinafika milioni 10. Na kwa hiyo tutakuwa tumemalizana na hizi, naomba Waheshimiwa Wabunge wasubiri baada ya muda si mrefu fedha hizi zitaanza kutumika.

Lingine lilikuwa ni tatizo la kule Singida linalohusiana na wale ndege wanaoitwa kasuku. Lilizungumzwa hapa na ikasemekana kwamba hawa kasuku walitusababishia hasara kubwa sana na ndiyo ilisababisha sehemu hizo zikawa na njaa kubwa sana. Ni kweli kwamba kulikuwa na tatizo la hawa ndege kuongezeka sana. Kabla ya kipindi hiki kulikuweko na utaratibu ambao wananchi walikuwa wanawakamata hawa ndege wanawaweka kwenye *konteina* wanawauza nje. Lakini ikafika mahali wakapungua sana kiasi kwamba Maafisa wa Maliasili walisimamisha ukamataji wa ndege hawa kwa sababu walifika mahali wakawa hatarini kutoweka moja kwa moja na kutokana na kusimamisha huko wakaongezeka kwa bidii sana. Sasa kwa kuwa walikuwa ni ndege waliokatazwa wasiharibiwe wakiwa wengi ni lazima tuwasiliane na watu wa Maliasili tuweze kukubaliana na hivyo ndivyo tulivyofanya. Lakini kwa kuwa ndege hao walikuwa hawajahi kuwa tatizo, maandalizi yetu ya kupambana nayo vile vile yalikuwa hayakuwa mazuri sana kwa sababu hatukuwa na dawa maalum za kuwashughulikia tulitumia dawa inaitwa Grand Atox tunayotumia kwa ajili kuulia kwelea kwelea pamoja na mitego, hizi njia mbili ndiyo zinazotusaidia tukapunguza sana hawa ndege. Sasa hivi tunazungumza na watu wa Maliasili ili tukubaliane kurudisha tena utaratibu wa kuwa-*harvest* ndege hawa ili waweze kuuzwa na kutupatia fedha na wakati huo huo kupungua.

Mheshimiwa Spika, sasa niende katika lile kubwa linalohusu chakula. Kwanza niseme kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi itafanya kila linalowezekana kuhakikisha chakula kinapatikana, kwamba ni fedha kiasi gani zitakazotengwa, nitamwachia Mheshimiwa Waziri wa Fedha atuambie ni kiasi gani ambacho Serikali imetenga kwa ajili ya kuhakikisha kwamba chakula kitapatikana. Lakini niwashukuru wachangiaji wote wa Chama Tawala hata wa upinzani maana wote kwa kweli walipiga debe kwamba fedha ziongezwe ili chakula kipatikane. Kwa hiyo, *concern* yetu wote hapa ni moja kuhakikisha usalama wa wananchi wetu kwamba wanapata chakula cha kutosha ili wasiathirike kutokana na hii hali ya njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii hali ya njaa tuliyoanza kuitabiri mapema, na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 31 March, 2002 alilihutubia Taifa akilitahadharisha juu ya uwezekano wa kuwepo kwa njaa. Kwa hiyo, halikuwa jambo lililokuja likatukuta hatulijui au hatukujiandaa na Mkuu wetu wa nchi alilizungumzia mapema kabisa kabla hata halijatokea. Na lilitokana na tathmini tulizokuwa tunafanya ambazo zilionyesha kwamba kungekuwepo njaa. Mwezi *June* Ofisi ya Waziri Mkuu, iliunda Tume iliyounganisha Wataalam wa Serikali pamoja na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na Wahisani tunashirikiana nao wakatembelea maeneo yote tuliyokuwa tunahisi kwamba yangekuwa na njaa, wakafanya tathmini nyingine iliyoonyesha hali ambayo ingekuwa kama mvua za vuli vingenyesha na kama mvua za vuli hazinyanyesha. Kwa hiyo, tulikuwa na taarifa za kutosha kabisa za kutuonyesha hali ambavyo ingekuwa. Lakini tulitegemea kwamba mvua za vuli zingenyesha. Kwa bahati mbaya hazikunyesha katika Mikoa karibu yote inayopata mvua za vuli na hiyo inatupunguzia chakula kwa asilimia 33 kwa theluthi moja.

Mheshimiwa Dr. Slaa amesema hatuzalishi kwa mvua za vuli, lakini sisi takwimu zinatuonyesha kwamba theluthi moja ya chakula kinachozalishwa humu nchini kinatokana na mvua za vuli. Kwa hiyo, kuzikosa mvua za vuli kulifanya hali yetu ikawa mbaya zaidi. Sasa tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba hali yetu ya uchumi ni nzuri, mapato yetu ni mazuri na kwa hiyo tunaweza tukatenga fedha za kutuwezesha kununua chakula ili kujazia pengo litakalojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nieleze kidogo juu ya hali ya chakula ilivyo sasa nchini nikianza na *SGR* ile hifadhi yetu ya Taifa. Hadi tarehe 13 mwezi wa pili, *SGR* ilikuwa na tani 28,969 katika maghala yake. Pale Dar es Salaam, Kipawa zilikuwepo tani 3,916, Arusha tani 3,181. Dodoma hapa ndiyo tuna stock za chini kabisa 1,046. Shinyanga tani 4,127, Makambako tani 3,714. Songea tani 8,158 na Sumbawanga tani 4,798.

Chakula hiki ambacho kiko katika maeneo ambayo hayana matatizo makubwa ya chakula kinahamishwa. Tunafanya operesheni maalum tukishirikiana na Shirika la Reli, namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Mwandosya kwa ushirikiano mkubwa sana. Tumeweka Afisa ambaye anasimamia uhamishaji wa chakula kutoka Sumbawanga kufikia Mpanda kwenda Shinyanga na tumeamua kwamba chakula kitakachopelekwa Tabora kitaachwa Tabora maana mwanzoni mpango ulikuwa chakula chote kiende Shinyanga na kingerudi kingetuletea matatizo.

Wakati huo huo chakula kilichopo Makambako na Songea kitahamishwa kwa magari kuletwa Dodoma ili kuhudumia wananchi wa Dodoma, Manyara, Singida na kadhalika na kidogo kitakwenda Tabora. Kwa hiyo, mipango imeandaliwa ambayo inahakikisha kwamba chakula hiki kitapatikana na kitahamishwa hivyo. Tumeamua pia kwa sababu matatizo mengi yako katikati ya nchi Makao Makuu ya *SGR* yatahamishiwa hapa na tumeamua mwaka huu tutaanza kununua mahindi katika Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Kagera.

Pamoja na chakula hiki tunachozungumzia cha *SGR/WFP* nao wamegawa tani 9,595 za chakula ambacho kimegawiwa Singida, mmesikia taarifa zikitolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa Dodoma na Shinyanga. *WFP* vile vile wana chakula tani 520 Tabora na tani 400 ambazo ziko Iringa nazo zitagawiwa na tunategemea chakula kingine kitaingizwa nchini ili kutimiza tani 27,000 kutokana na fedha tulizopewa.

Naomba Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wahisani waliotusaidia ambao Sweden waliotusaidia dola za Kimarekani milioni 1.5, *PFID* dola milioni 2.5. Ireland dola 654,000. Japan dola laki tatu, Belgium dola laki saba na moja elfu na Canada dola mia mbili na ishirini na tano elfu ambazo zinatumika kununua chakula ili kutimiza kiasi hicho ninachozungumzia.

Wakati huo huo tumeagiza mahindi kwa fedha zetu kutoka Kenya tani 10,000. Mheshimwia Makamu wa Rais alipotembelea Kenya wakati wa Sherehe za Uhuru aliomba Kenya watuuzie mahindi na wakakubali. Tumeshakamilisha mazungumzo nao kilichobakia ni chakula kuanza kuletwa na tunatarajia katika muda usiozidi wiki moja sasa chakula hicho kitaanza kuja tani 10,000.

Tani 6,000 kitatumika Mara na Mwanza tani 4,000 kitakwenda Shinyanga kuimarisha hali ya chakula katika eneo lile. Juzi nimezungumza na Makamu wa Rais wa Malawi, amekubali kutuuzia tani 10,000 wana *balance* kule kwao ya tani 73,000 na Katibu Mkuu wangu ameondoka jana usiku kuongea nao kumalizia bili hiyo kwa hiyo tutapata tani 10,000 kutoka kule.

Tunatarajia katika siku 10 zijazo kupata tani nyingine 10,000, 5,000 kupitia Dar es Salaam na 5,000 kutoka Uganda kupitia Mwanza ambazo zitakuja kuimarisha hali ya chakula katika maeneo haya.

Sasa ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge ni kwamba ili tuweze kununua chakula hiki tunachozungumzia na kuagiza chakula zaidi kutoka maeneo mbalimbali basi muiruhusu Serikali, muipitishe hii *Supplementary Budget* ambayo Waziri wa Fedha anawasilisha mbele yetu ili ituwezeshe kugharamia chakula hiki. Tutajihidi kuhakikisha kwamba chakula hiki kinagawiwa kwa utaratibu mzuri unavyowezekana. Lakini naomba basi na mimi mtusaidie kule kwenye majimbo kuhakikisha kwamba chakula hiki kinaelekezwa kwenye maeneo yenye matatizo.

Tutaandika kwamba Wabunge washirikishwe katika Kamati za Njaa ili kuhakikisha kwamba mnatusaidia kukielekeza. Lakini kama alivyozungumza Mheshimiwa Christopher Wegga, rafiki yangu kutoka Morogoro, Serikali kwa makusudi kabisa itaweka mkazo katika maeneo yanayozalishwa chakula kwa wingi ikiwa ni pamoja na Mikoa ya Kagera, Kigoma, Sumbawanga, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Mheshimiwa Wegga ametupa na Morogoro. Lakini Morogoro itabidi tuji-*organize* vizuri kabla hatujaweza kutumia hizi *process* zilizopo.

Tutaendelea kujitahidi kuongeza maeneo yanayomwagiliwa maji lakini naomba mtambue kwamba umwagiliaji maji unakwenda pole pole sana kwa sababu ya gharama kubwa sana zinazohusika na vile vile muda wa *construction* unaohusika.

Lakini mnaosikiliza Redio mnasikia kila siku miradi ikiwekewa mawe, miradi ikifunguliwa ya umwagiliaji maji na Mheshimiwa Rais alipozungumza hapa Bungeni alitueleza juu ya ongezeko kubwa sana la eneo la umwagiliaji maji lililotokea katika siku hizi chache zilizopita kutufikisha katika hekta 230,000.

Mheshimiwa Spika, kuna uwezekano wa kufikia hekta milioni 2.3 kama tukijipanga vizuri na tukapata *resources* ambazo ndiyo zitakazotusaidia. Katika miaka ijayo tutapendekeza Serikalini, kwamba tuwe na soko la uhakika la chakula.

Kwa hiyo, tutawahimiza wananchi wazalishe, wauze kwa watakaotaka kununua ziada ya mahindi yatakayobaki Serikali itanunua na kuhifadhi katika hifadhi ya chakula cha Taifa lakini vile vile kuuza ziada mahali patakapohitajika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naomba tena niunge mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la njaa. Kwa kuwa Mikoa mingi sasa hivi ina njaa Serikali ilione hili kuwa ni janga la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa kilimo cha mabondeni kihamasishwe. Badala ya kupitisha fedha benki ambapo wananchi walio wengi hawawezi kwenda kuomba mikopo, Serikali sasa isambaze mbolea Vijijini sambamba na kutoa chakula cha msaada. Wananchi wakopeshwe pembejeo zenyewe siyo fedha. Wakivuna mazao yao yanunuliwe na Serikali na ndiyo yasaidie kulipa gharama.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza naunga mkono bajeti hii ya nyongeza kwanza kugharamia mambo ambayo ni muhimu kwa maisha ya binadamu mia kwa mia ikiwa ni pamoja na chakula, umeme na ununuzi wa ndege ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali chakula kilichopo kisambazwe haraka ili kunusuru maisha ya wananchi ambao sasa hivi hawana chakula ukizingatia akina baba wengi wametoroka nyumba zao wakiwaacha wanawake wengi wakihangaika na watoto. Serikali iongeze fedha za kununulia chakula kwani chakula hakuna hasa Vijijini na ukizingatia bei sasa hivi imepanda, ndoo moja ya kilo ishirini ni shilingi 5,000/= mpaka 6,000/= kwa hiyo wananchi hawana uwezo.

Mheshimiwa Spika, mipango ya kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji ni muhimu kwa hiyo Serikali iwe na mipango ya kudumu ya kuchimba mabwawa. Mpango huu uwe wa kudumu na mabwawa yanayochimbwa yakamilike kwa wakati badala ya kuchimba bwawa moja kwa miaka miwili na kuendelea. Suala la umeme wa uhakika na wa kudumu na unaotokana na makaa ya mawe ni vizuri Serikali izingatie ushuri wa Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuwa na mpango ili kuondokana na tatizo la umeme wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe na uangalifu wa kutosha kuhusu matatizo ya matumizi ya Serikali hasa kutoa fedha ili kumpa mwekezaji kama zawadi sio sawa ingefaa wakopeshwe au wakakope benki. Fedha wanazopewa *TANESCO* zingesaidia chakula ili wananchi wapewe na hata kutengeneza mabwawa.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutumia fedha kwa ajili ya kugharamia watoto wa sekondari. Haya ndiyo mambo muhimu ambayo Serikali inapaswa kutumia fedha zake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono ununuzi wa ndege lakini inunuliwe ndege yenye hadhi na ya kubeba watu angalau Mheshimiwa Rais na ujumbe wake. Vile vile Serikali iwe na ungalifu kwani habari

ziko wazi katika mitambo na kwamba bei zichunguzwe upya na zielezwe zinapatikana wapi ili Mbunge anayeweza kutafuta akatafute.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya maombi ya matumizi ya nyongeza kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja hasa kutokana na ukweli kwamba hali ya ukame kwenye baadhi ya Mikoa inayotegemewa kulisha nchi yetu Kitaifa imeathiri sana chakula nchini, pamoja na athari zilizojitokeza za upungufu wa uzalishaji nishati kutokana na vianzio vya mito, mvua na maji kupungua sana. Hivyo kulazimika kununua nishati mbadala yaani kununua nishati mbadala yaani kununua mafuta kwa ajili ya kusukuma mitambo hiyo ili kuzalisha nishati kwa ajili ya kuendeleza kukuza uchumi wetu kwenye viwanda bali pia kutoa huduma muhimu na za lazima mahospitalini, shuleni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika utangulizi wako kuhusu hoja hii ulisema Serikali haitaongeza kodi yoyote ili kufidia pengo hilo, lakini cha ajabu Serikali inasema kwenye kifungu cha *5(1): "The Minister may........ borrow within or outside the United Republic or partly within and partly outside the United Republic.……"* Kwa nini Serikali ikope kutoa nje? Hii inamaanisha kwamba Serikali huenda kwa kitendo hicho ikalazimika kuongeza kodi ili kufidia hilo deni.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi kwa kipengele hicho. Pili, kwenye kifungu cha 5(3) Serikali inasema hizo fedha za kukopwa zitarudishwa kabla ya tarehe 31/10/2004. Ninavyoelewa ni kwamba matumizi yote haya ya fedha za nyongeza kama ilivyo kwenye original budget ziwe zimetumika mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2003/04 (30 Juni, 2004) na sio kuingiliana na mwaka wa fedha 2004/05. Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha hoja hii kwa mjadala Bungeni ili tupitishe kwa maslahi ya wananchi. Kwa hiyo naomba bajeti hii tukiipitisha ianze kutekelezwa mara moja. Kwa hayo machache naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa juhudi alizoonyesha tangu awe Waziri. Pia pongezi kwa *TRA* kwa kuinua uchumi wa nchi yetu. Pamoja na mazuri yanayofanywa na Serikali nachangia vipengele vifuatavyo kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, moja, fedha zilizopitishwa zikitumika kwa uzembe bila kuelekeza kwenye bajeti hii maafisa/wataalam wawajibishwe.

Mheshimiwa Spika, pili, suala la umeme Waziri wa Madini na Nishati waangalie matumizi ya mkaa wa mawe kama unatosheleza matumizi kwa wananchi basi waharakishe mradi wa Mchuchuma uanze kazi.

Mheshimiwa Spika, tatu, suala la njaa mkoani Shinyanga ni kweli wanawake wajawazito, watoto, wagonjwa na waathirika wa Ukimwi wanakosa chakula. Naomba Serikali isikilize kilio chetu Wanashinyanga kupitia viongozi tuliopo Bungeni tuongezwe chakula cha aina zote:-

(a) Cha nguvu kazi.
(b) Cha bure kwa wananchi wasiojiza na wagonjwa, wajawazito na watoto.
(c) Cha kuuziwa wananchi wenye uwezo.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo machache, narudia kuunga mkono hoja hii mia kwa mia na watekelezaji Mungu awape nguvu, afya ya kutekeleza wajibu wao.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningependa kuipongeza Serikali kwa kuleta makadirio ya matumizi ya nyongeza kwa utaratibu wa kuhamisha vifungu vya matumizi kutoka kasma moja hadi nyingine bila kuwapa wananchi mzigo zaidi wa kodi ya nyongeza. Aidha, matumizi ya nyongeza yamelenga katika maeneo ambayo ni muhimu na yanayostahili kushughulikiwa kwa kipaumbele maalum.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia katika maombi kuhusu fedha zaidi kwa elimu, rukuzu kwa Halmashauri, kupambana na njaa, umeme na ndege kwa matumizi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, kero ya elimu ni moja ya kero kuu kwa wananchi hasa kutokana na vijana wengi sana wanaokosa nafasi za kuingia kidato cha kwanza. Naunga mkono Wizara ya Elimu iongezewe fedha zinazoombwa ili iweze kuendelea kuboresha elimu. Hata hivyo kuna umuhimu kwa Wizara kufikisha fedha kwa ajili ya vitabu na kadhalika kama ilivyoahidiwa na kuwekewa kasma. Muhimu zaidi ni kuhakikisha kwamba shule za sekondari zinapata fedha za kutosa na wakati muafaka kwa ajili ya chakula. Hivi sasa shule nyingi za sekondari zina shida kubwa sana kuhusu kuwapatia wanafunzi chakula.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono azma ya kuzipatia Halmashauri za Wilaya fedha nyingi zaidi kwani nyingi za hizi Halmashauri zinashindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo hasa kuchangia katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, njaa tuliyo nayo hapa nchini hivi sasa siyo tu kero bali pia hatari kubwa kwa ustawi na maendeleo ya nchi yetu. Naunga mkono pendekezo la kuongeza fedha kwa ajili ya kupambana na njaa. Hata hivyo ni muhimu kuhakikisha mgao mzuri kwa maeneo yote yaliyoathirika. Muhimu zaidi ni kuwa na mipango na mikakati thabiti ya kuepusha kabisa janga la njaa miaka ijayo. Bila ya kuwa na mipango thabiti ya kilimo cha umwagiliaji na kutumia vifaa vya kisasa, kuondoa njaa Tanzania itakuwa ndoto na tutakuwa omba omba daima.

Mheshimiwa Spika, umeme ni nishati muhimu sana na hapana kuwa na mipango na mikakati ya muda mfupi na muda mrefu kupambana na kero ya umeme ingawaje naunga mkono hoja ya kuipatia ruzuku *TANESCO* ili ipambane na matatizo ya muda mfupi kwa kutumia umeme katika vianzio vmbadala kama vile mkaa wa Mchuchuma, jua, upepo na kununua mtambo wa *IPTL* badala ya kuendelea kukodi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ndege ya Rais ni muhimu kwa usalama, heshima na tija kubwa zaidi kwa utekelezaji bora zaidi wa misafara ya Kiongozi Mkuu wa Taifa letu. Naunga mkono mapendekezo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, Makatibu Wakuu na watumishi wote wa Wizara ya fedha kwa umakini na umahiri wao mkubwa katika kuandaa na kuwakilisha hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, kimsingi nakubaliana na maudhui ya Muswada ya kulitaka Bunge kuidhinisha matumizi ya ziada ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, balaa la njaa nchini ni kubwa sana na Serikali kukabiliana nalo ni lazima ifanye kazi kioperesheni. Serikali ihakikishe chakula cha kutosha kinamfikia wajibu wake awajibishwe ipasavyo ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi, hasa Wakurugenzi Watendaji na Wakuu wa Wilaya wataoshindwa kusomba chakula na huku wamekwishapewa fedha za kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuwa ombaomba wa chakula kama Wizara ya Kilimo na Chakula haitakuwa makini katika kusimamia kilimo. Haitoshi tu kuwa na mipango mizuri kama haisimamiwi ipasavyo. Miradi mikubwa kama ya *RUBADA* na *KBO* alazima sasa itekelezwe. Suala la kuendeleza mabonde makubwa lazimalipewe umuhimu wa pekee badala ya skimu ndogo ndogo. Wizara ya Kilimo ishirikiane na Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* ili kuvutia wawekezaji wakubwa katika kilimo na hasa baada ya kupitisha Sheria ya Ardhi (marekebisho).

Mheshimiwa Spika, Serikali isitegemee twakimu za hali ya njaa kutoka kwa watu wa nje badala yake ijenge uwezo wa watendaji wake na wawe wakweli katika kutoa takwimu sahihi. Inaelekea watendaji wengi wa Serikali wakiwemo Wakuu wa Wilaya ni waoga na waongo katika kutoa takwimu sahihi. Ni vema Waziri Mkuu akatoa tamko rasmi kuwa hakuna DC atakayefukuzwa kwa kuwa na njaa Wilayani kwake.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa lazima wawezeshwe ili waweze kutoa taarifa sahihi za kusaidia wananchi. Hali ya ukame pia inasababisha upungufu wa maji kwa ajili ya kufua umeme wa *TANESCO* na hivi kulazimisha T*ANESCO* kununua umeme toka *IPTL.* Kutenga fedha kwa ajili hiyo ni muhimu lakini ni vema menejiment ya *TANESCO* ikaangaliwa upya ili iwe na ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kupunguza *transmission losses.* Vyanzo mbadala vya upatikanaji umeme ikiwamo makaa ya mawe ya Kiwira na Uranium iliyoko Mkoani Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa ndege ya Serikali ni muhimu pia katika kipindi hiki kigumu hili lingeahirishwa hadi hali itakaporuhusu. Hata hivyo kumekuwa na malumbano makubwa sana ya ununuzi wa ndege hii hata kabla ya Bajeti ya Serikali ya mwaka huu. Hivi ni kwa nini matumizi haya hayakuwekwa katika bajeti ya 2003/2004? Hivi sasa ni nini kimetokea hata umuhimu ukawepo sasa hivi? Matumizi ya nyongeza yawe ni kwa ajili ya matumizi ya dharura ambayo ni *unforeseen* na kuyatengea fedha. Ununuzi wa ndege ya Serikali si unforeseen. Lakini pia hata bei imekuwa ya malumbano mengi na wala haijatamkwa bayana. Hivi kuna usiri gani wa bei halisi ya hiyo ndege? Kwani taratibu chini ya *Public Procurement Act, 2001* haikufuatwa? Kwa nini sasa Serikali isiwe wazi katika hili?

Mheshimiwa Spika, matumizi ya ziada ya vitambulisho vya Kitaifa nna daftari la wapiga kura ni muhimu. Serikali inaomba fedha ingawa Waziri wa Fedha hakuonyesha katika *Supplementary Expenditure No. 1* ya 2003/2004. Si vizuri kutaja tu bila Waheshimiwa Wabunge kupewa maelezo ya kina kabla kwa nyaraka husika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba kuwasilisha.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukupongeza kwa kuleta hoja hii muhimu sana. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imetenga shilingi 10,000,000,000/= kwa ajili ya kununulia chakula cha njaa. Naishukuru sana Serikali hata hivyo nashauri kwamba fedha hizo hazitoshi kwa hiyo ziongewe kwa kuwa hali ya ukame inaendelea. Mkoa wetu wa Dodoma hususan Wilaya ya Mpwapwa halin I mbaya sana wananchi wengi hawana kabisa chakula. Mabonde ya Matomondo, Godegode, yalipata mafuriko makubwa mimea yote ilisombwa na maji.

Pili, napenda kujua hadi sasa Serikali imetumia fedha kiasi gani kununua chakula cha njaa na imetumia kigezo gani hadi kufikia shilingi 10,000,000,000/=. Suala la njaa ni suala nyeti sana lishughulikiwe haraka iwezekanavyo maeneo yote yenye ukame hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba kwa umahiri wake wa kuiongoza Wizara hii nyeti na ngumu. Ndugu Mramba ameimudu Wizara hii vizuri.

Mheshimiwa Spika, nayaunga mkono maombi ya kuidhinisha bajeti ndogo hii kwa sababu mbili kuu:-

(a) Mahitaji haya ya ziada yametokana na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala kama vile ongezeko la idadi ya watoto wetu wanaokwenda sekondari na wale wanaoingia darasa la kwanza. Mafanikio pia yana gharama zake na ni sehemu ya maendeleo yetu.

(b) Dharura ya ukame imeilazimisha Serikali yetu kuyakabili kwa kutumia uwezo wa Taifa kupitia Bajeti yake. Naipongeza sana Wizara kwa kufanya marekebisho ya kibajeti bila kuongeza kodi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kuwa mradi wa umeme wa Handeni hadi Kwediboma Wilaya ya Kilindi umekwama kwa muda wa miaka mingi. Mradi huu umekwama kwa sababu ya fedha, basi namwomba Mheshimiwa Waziri amege fedha kutoka mafungu mengine akamilishe kiporo hiki ambacho sasa kinaitia Serikali aibu. Bajeti ya nyongeza itusaidie kuukwamua mradi huu wa maendeleo ya Wilaya mpya ya Kilindi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumpongeza Waziri na Wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hivyo naiunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa kuwasilisha hoja yake vizuri. Baada ya kumpongeza naomba nichangie kidogo katika maeneo machache. Lakini kabla sijasahau naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Naipongeza Serikai kwa kuona umuhimu sasa wa kuongeza idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza. Naiunga hoja ya kuongeza bajeti lakini kwa vile mpango madhubuti wa kuboresha elimu unaeleweka MMEM na hatimaye MMES ni vema Serikali ifanye projection ya idadi ya ongezeko la wanafunzina walimu mapema ili isiwe tena kial mwaka tunaombea fedha za ziada.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ndege ya Serikali. Naunga mkono, ni vema sasa taratibu zifanywe na zikamilike ili ifikapao hiyo Juni-Septemba, ndege iwe imeshafika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafao ya *PPF* kwa waliostaafishwa, naunga mkono hoja. Ushauri wangu ni kwamba imekuwa kawaida kwa wenye viwanda kutokuwakisha michang ya pensheni ambavyo wafanyakazi wanakatwa wakiwa kazini. Matokeo Serikali inajitolea kubeba mzigo ambao si wake. Kwa vile ni sheria kuwasilisha makato na wanaokiuka wanajulikana ni vema Serikali iwe makini kufuatilia tatizo hili, isingoje mpaka kiwanda kinafilisika, hivyo kuwa vigumu kumbana na kumchukulia hatua.

Naipongeza Serikali kwa kuleta ombi hili kwani kweli ni tatizo kubwa linawakabili wananchi wetu. Ushauri wangu ni kwamba bado ni muhimu kuweka utaratibu mzuri wa kuhifadhi chakula wakati wa mavuno na vile vile bado msisitizo na mikakati maalum ifuatiliwe ili kilimo chetu kiboreke na kuwawezesha wananchi walime kitaalam ili wavune na ziada. Pili, chakula cha njaa kinachelewa kuwafikia walengwa kwa sababu za kirasimu zisizo za msingi. Maelezo yawe *straightforward* na watendaji wazingatie ili kutosababisha kukwama kwa chakula kutoka bandarini hadi Vijijini. Wananchi hasa wakiwa mama na watoto wanakufa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuwapongeza kwa kazi nzuri na kuwatakia tena kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wote wawili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kwa Wizara kuelta jambo hili Bungeni. La msingi nyongeza hii inatokana na mapato yetu. Hongera *TRA* na vyombo vyote vinavyoshughulikia maduhuli katika sekta mbalimbali. Reallocations kama hizi ambazo haizhusishi nyongeza ya kodi ni nzuri maana ina katapua ili kuunga wajihi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya *Order Paper*. Kukubali hoja hii ni kuwatendea haki wananchi wa Tanzania. Hali ya njaa kali haifahamiki lini itaisha. Muhimu kwa Serikali makini. Huu ndiyo ustaarabu wa Serikali makini ndiyo huu kwa kujali wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri wote wa Fedha na hongera sana.

**MHE. ALHAJ SHAWEJ ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja. Hata hivyo nina mambo au jambo moja la kuchangia.

Mheshimiwa Spika, naomba nikupe taarifa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alifanya ziara katika Hospitali ya Missiru ya Berega Kilosa na sekondari ya mfano ya Mgugu.

Mheshimiwa Spika, katika ziara ile mbele ya Baba Askofu wa Kanisa la Anglikana pamoja na wananchi wengi alikubali kuwa angewaeleza Wizara ya Nishati na Madini kupeleka umeme katika eneo hilo kupitia Dumila, Maguha, Magubike na Berega Wilayani Kilosa.

Mheshimiwa Rais, Ofisi yake iliwaandikia Wizara ya Nishati na Madini. Wizara hiyo ikamtaka *Regional Manager* wa Mkoa wa Morogoro afanye analysis na kuandika write-up kama mradi huo ni viable na *Regional Manager* alifanya hivyo. Naibu Waziri wa Nishati na Madini Dr. Msabaha alifanya ziara ili kuchunguza kama maeneo hayo yanafaa. Alipofika aliongozana na mimi alikubali kuwa mradi wa umeme huo unalipa.

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi bado naendelea kuwa njia panda. Mheshimiwa Raisa ameagiza, Ofisi yake Mheshimiwa Rais imeiandikia Wizara ya Nishati na Madini. *Regional Manager* aliandikiwa afanye *study* ya *viability* ya mradi huo. *Regional Manager* ameandika na kupeleka Wizarani. Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Dr. Msabaha alitembelea maeneo hayo ili kujithibitishia mwenyewe. Dr. Msabaha alikubali kuwa umeme unahitajika kwa maeneo hayo. Linalonishangaza sasa tunatoa ruzuku kwa Kampuni binafsi ya *TANESCO* ambayo haiko tayari kutekeleza ahadi ya Rais kupeleka umeme Berega. Lingine linalonishangaza ni kuona *TANESCO* inashindwa kutoa nguzo za umeme katika Wilaya ya Kilosa. Hakuna nguzo za umeme na hivyo pamoja na wateja kufanya wiring bado *TANESCO* inashindwa ku-*provide* nguzo. Hivyo namshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha na menejimenti ya *TANESCO* kupeleka nguzo Kilosa na kutekeleza maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, *may be it is high time.* Sasa tuangalie uwezekano wa kuendeleza Mchuchuma tupate umeme toka mkaa wa mawe. *South Africa* wana *reserve* sasa ya 20-30,000 *Megawatts.* Kwetu itatusaidia sana hasa kwa *proper use of Hydropower.* Aidha, *since investment will be solely private.* Tuanzeni.

Mheshimiwa Spika, *naturally,* hoja naiunga mkono.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuchangia machache kuhusu Muswada ulio mbele yetu. Pamoja na sababu ambazo kwa ujumla sikubaliani na *principle* za kuomba Bajeti ya nyongeza *(Supplementary Budget),* naunga mkono Muswada huu ulioleta na Mheshimiwa Waziri wa fedha. Sababu zinazonifanya niunge mkono Muswada huu ni mbili; fedha za kununulia chakula cha njaa na matumizi ya ziada kwa Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, hali ya njaa katika Taifa letu sasa hivi ni mbaya sana na kwa maoni yangu ombi la shilingi bilioni kumi ni ndogo mno kwani sasa hivi katika Wilaya fulani fulani wananchi wameanza kupoteza maisha. Ningeomba Serikali ione umuhimu wa kuwa sahihi zaidi katika kusambaza chakula kwa wananchi walioathirika zaidi na njaa na wale ambao hawana uwezo kabisa kifedha. Wananchi wasio na uwezo kifedha, wazee, walemavu, wanawake wajawazito na watoto wa shule za msingi wapewe chakula bure kabisa na wala sio kwa bei yoyote. Ningeshauri kuwa kwa wanafunzi wa shule za msingi Serikali itoe chakula bure kwa shule za msingi kwa milo ya mchana na hii itakuwa motisha ya kuimarisha mahudhurio shuleni. Wilaya iliyoathirika sana na njaa sasa ni Wilaya ya Iramba hasa kwenye Kata za Kaselya, Urughu, Mtekente, Mtoa, Shelui, Ntwike, Tulya, Kidaru, Kyengege, Ulemo na Kinampanda. Urasimu katika kusambaza chakula cha njaa upunguzwe kama sio kuondolewa kabisa hasa

utaratibu wa kuwaachia wafanyabiashara wasambaze chakula una kasoro kubwa na mgao wa chakula hauwafikii wananchi walioathirika na njaa. Naomba chakula cha njaa sasa kipelekwe kwenye Vijiji vya Ntwike, Tulya na Kidaru katika Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa njaa inakuwa ni *permanent feature* kaitka Mikoa ya ukame kama Singida, Dodoma, Shinyanga na Tabora ingefaa sasa Serikali ione umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Njaa *(Famine Relief Fund)* na kwa kufanya hivyo Serikali itakuwa imejiweka vema zaidi kukabiliana na matukio ya njaa ya mara kwa mara. Mwaka huu 2004 kuna kila uwezekano kuwa njaa itaendelea kwani mvua mwaka huu ni ndogo na imechelewa na kunyesha kwake hakuna uhakika wa kuwezesha mazao kuku ana kutegemea mavuno ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa dhati ombi la matumizi ya ziada kwa Wizara ya elimu hasa kwa kuongezea wanafunzi watakoingia kidato cha kwanza. Mimi ningeshauri kuwa Serikali ihakikishe kuwa wanafunzi waliofaulu darasa la saba mwaka 2003 wote wapewe nafasi kuendelea na kidato cha kwanza. Kwa kufanya hivyo itakuwa kitu cha maana sana hata ikiwa matumizi ya miradi ambayo siyo muhimu sana iahirishwe. Kwa wanafunzi wa darasa la saba itakuwa dhambi kubwa sana kuwatelekeza vijana hawa wasiendelee na masomo (elimu) na Serikali ichague kuendeleza miradi ambayo siyo ya lazima sana na hata ikiahirishwa Taifa letu linaweza kungojea lakini wanafunzi wanaokatishwa elimu wataathirika kimaisha na Taifa litakuwa limewatelekeza viongozi wa kesho.

Mheshimiwa Spika, ombi la Mheshimiwa Waziri kwa matumizi ya ziada kwa umeme mimi nitaunga mkono tu kama matumizi haya yatendeleza pamoja na miradi ya sasa ya kuzalisha umeme na kusambaza umeme. Pia suala laMfuko wa Umeme Vijijini pia unufaike na Bajeti hii ya nyongeza ya shilingi 37,250,000,000/= na pia suala la kupunguza bei za umeme kwa watumiaji wadogo na kwenye taasisi za jamii kama hospitali, mashuleni na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu kwa dhati kabisa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia, pamoja na hoja zangu zilizotangulia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imefanya tathmini ya kina kuhusu gharama za kuendeshea ndege *G 550* inayotaka kununa kwa kuzingatia kuwa ndege hiyo imetengenzwa kwa masafa marefu na safari za Serikali yetu inategemewa kuwa zaidi za ndani.

Mheshimiwa Spika, iwapo itatumika zaidi kwa masafa mafupi madhara yake ni nini kwa *Eupine* na hivyo *duration* au *life span* ya ndege?

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, mimi kwa ujumla wake nakubaliana na naikubali hoja hiyo kwa ujumla wake sina matatizo nayo. Naomba kuchukua fursa hii kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote na Watendaji Wakuu na Wakurugenzi wa Wizara ya Fedha kwa jitihada wanazochukua kukuza mapato ya Serikali kiasi ambacho hivi sasa tunaongeza bajeti bila ya ongezeko la kodi pamoja na kwamba vyanzo vingi vya mapato hasa kwenye Halamshauri vimefutwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa siku za usoni (naelewa hili umeahidi tutalizungumza) tuone tunazingatia zaidi:-

Mheshimiwa Spika, moja suala la kilimo ili pasitokee tatizo la ukosekanaji wa chakula pawekwe mkazo maalum ikiwa tunamudu kutoa au kuomba fedha za dharura shilingi bilioni kumi kwa ukame basi pafanywe jitihada za makusudi kuongezwe bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa makusudi ili tuweze kujipanua kwa chakula. Endapo utakuwa na chakula cha kutosha kwa mipango mahsusi hapatakuwa na tatizola njaa. Tatizo la njaa tunalisababisha sisi kwa kutoweka mkazo wa kwanza kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, pili, Mheshimiwa Mramba anastahili pongezi, nimevutiwa sana na hatua anazotaka kuzichukuwa kuhusu masuala ya manunuzi ya magari ya wakuu mbalimbali mfano, Wakuu wa Mikoa, Wilaya na hata Makatibu Wakuu ni kweli kabisa ikiwa Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri wananunua magari waliyokopeshwa au kupewa kwa muda wa miaka mitano iweje leo Mawizara wawe wananunua magari ya fahari katika kipindi cha kila baada ya miaka mitatu, hilo haliwezekani kabisa.

Mheshimiwa Spika, nadhani pawekwe utaratibu maalum na namna watakayo bajeti kasma ya ununuzi wa magari yaende angalau kwa muda usiopungua miaka mitano. Wahakikishe kila mmoja wao wanayatunza ipasavyo, hilo likifanyika litasaidia sana kutunisha Mfuko wa Serikali. Hatua ya Mheshimiwa Waziri aliyoichukua ya kuhamisha fedha kutoka kasma za Wizara mbalimbali za safari na semina na kuzileta kushughulikia dharura iliyojitokeza ni jambo la kupigiwa mfano. Kwa siku za baadaye basi pamoja na mkazo wa kilimo nilioutaja paonekane vile vile suala la usindikaji wa vyakula na utafiti.

Mheshimiwa Spika, ningemwomba Mheshimiwa Waziri kuitupia macho sekta inayoshughulikia utengenezaji wa magari ya Nyumbu Jeshini. Naomba nayo pamoja na ukwasi wa fedha tulizo nazo lakini hii nayo ipewe uwezo na mtazamo wa makusudi, tuone inawezaje kutengeneza magari madogo madogo ya mizigo na usafiri Vijijini na hata ikiwezekana utengenezaji wa matrekta madogo madogo kusaidia msukumo wa kilimo. Endapo hilo litawezekana Watanzania waonekane wanajielekeza katika ukulima wa maeneo madogo madogo kwa kutumia vifaa vinavyotengenezwa hapa nchini, hili nalo litasaidia ajira kwa Watanzania na hasa vijana. Hapana shaka umaskini utapungua kama sio kuondoka kabisa. Hayo yanawezekana alimradi tutangulize nia na azma tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** *Honourable Speaker, let me first congratulate the Minister of Finance for his exemplary speech. Without forgetting TRA for their god job of collecting taxes form various business enterprises in our country.*

*Honourable Speaker, I support very much this supplementary expenditure request made by the Minister of about 40 billion shillings.*

*Honourable Speaker, since TANESCO spends a lot of money for buying fuels so as to avoid electricity rationing it means they have enough reason to be granted the funs lack of electricity will led us backward in our struggle for development and reducing poverty.*

*Honourable Speaker, our Government is always trying to improve something somewhere and I heartedly congratulate our Government for that move.*

*Honourable Speaker, the decision of our Government to buy food, by containing the shortage caused by drought is a very positive step. Will enable us to make sure that no one suffers form food shortage.*

*Honourable Speaker, it is a very encouraging thing that there is no new tax introduced in this supplementary budget.*

*Honourable Speaker, buying a more safer plane for our leader is a very promising decision. At a right time delays have dngarous end.*

*Honourable Speaker, I do not believe that you can do today's business, with yesterday's method and be in business tomorrow.*

*Honourable Speaker, right wrongs no man and no great thing was achieved without danger.*

*Honourable Speaker, finally, I would like to ascertain that I wholly support this supplementary budget at rate of hundred percent.*

*I beg to remain sincerely.*

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri wake wote pamoja na watendaji wao kwa kuwasilisha hoja hii mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la bajeti kwa ajili ya matumizi maalum kwa faida ya Watanzania wote ni suala muhimu na hatuna budi kukubaliana nalo kwa faida yetu.

Mheshimiwa Spika, kuongeza fedha kwa kazi ya kuwanusuru Watanzania katika hali hii ya njaa iliyotukumba ndani ya nchi ambayo imesababishwa na ukosefu wa mvua sio uzembe wa wananchi, ni lazima lakini kwa upande wa Serikali hili liwe ndio somo kwa kukaa na kusubiri mvua tu ndio tupate mazao, hilo ni tatizo kwa hiyo iko haja kuongeza nguvu kwenye kilimo cha umwagiliaji na kuhifadhi maji.

Mheshimiwa Spika, umeme wa *Net Group (TANESCO)* mpaka hivi sasa ni suala ambalo linashangaza sana katika utendaji wao hata Serikali inafika kugharamika sana na kutumia fedha nyingi kwa kuwaokoa Watanzania wasikumbwe na giza ambalo linaweza kutokea wakati wowote kama Serikali haitatia mkono wake katika kuisaidia *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, kama hivyo ndivyo naiomba Serikali itafute kitu mbadala cha kuweza kuzalisha umeme badala ya kutegemea njia moja tu na njia yenyewe kwa kiasi kikubwa tumekaa tu na kumsubiri Mwenyezi Mungu ateremshe mvua ndio tuzalishe umeme.

Mheshimiwa Spika, kama hatukupata mvua basi tunaingia kwenye matatizo ambayo kwa wakati mwingine itakuwa ni vigumu kuyatanzua kama hatutakuwa na fedha, tutajinusuru vipi tutakapopata maafa kama hayo?

Mheshimiwa Spika, hofu yangu kwa hivi tunavyokwenda isije ikifika wakati tukasema hali yetu sio nzuri na hivi sasa turejeshe tena kodi zote za Serikali ambazo zilifutwa juzi tu kwenye Bajeti iliyopita zisije zikarudishwa zitatuweka katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, suala la ununuzi wa ndege ya Rais hilo ni suala ambalo halina mjadala. Naungana nalo ili Rais wetu apate heshima yake kama Rais kwa kuwa na ndege yake ambayo ataitumia kwa shughuli zake za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, napenda kuunga mkono hoja hii, ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Wizara ya Fedha kwa kuwasilisha hoja ya Matumizi ya Nyongeza kwa mwaka 2003/2004 kwa lengo kuu la kutekeleza hoja za Wabunge na kudhibiti hali ya dharura iliyojitokeza katika maeneo muhimu kama elimu, chakula, umeme na fidia kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa hotuba ya Bajeti ya mwaka 2003/2004, Wabunge wengi walizungumzia sana mahitaji ya kuboresha maeneo mbalimbali na kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na watendaji wake wamejibu hoja hizo kwa utekelezaji ndani ya kipindi cha 2003/2004 badala ya kusubiri bajeti mpya ya 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba sehemu kubwa ya fedha hizi ni fidia ya hila makusudi na uzembe uliofanywa na mashirika mengi ya umma ikiwemo Mamlaka ya Mkonge Tanzania ambapo Pensheni na *PPF* halali za wafanyakazi hazikulipwa, licha ya sehemu ya michango yao kukatwa katika mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba kama hila na uzembe huu usingefanyika, fedha hizi leo zingeelekezwa katika mipango bora ya maendeleo kama vile elimu na maji.

Kwa kuwa mapungufu ya fidia za mafao, pensheni na *PPF* za wafanyakazi ni makubwa ingefaa Mheshimiwa Waziri afafanue kama fedha zilizoombwa zinakidhi madai ya wafanyakazi wote na kama zinahusisha pia adhabu *(penalty)* ambazo *PPF* inaidai Serikali kutokana na kucheleweshwa kulipwa kwa michango hiyo *PPF.*

Pili, Mheshimiwa Spika, naomba pia kuipongeza Wizara ya Fedha kwa kutenga fedha kwa ajili ya kufidia mapungufu ya mapato kwa Halamshauri zetu kutokana na kufutwa kwa kodi mbalimbali. Uamuzi huu pamoja na maamuzi ya Serikali kuongeza viwango vya fedha za ruzuku kwenda katika Halmashauri ni mwelekeo unaonyesha jinsi Serikali Kuu inavyotafakari na kutekeleza azma ya kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa njia gani Serikali inadhibiti bei ya mafuta *JET AI* yanayotumiwa na *TANESCO* kuendeshea mitambo ya uzalisha umeme wa *IPTL.*

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa kwamba ongezeko kubwa la gharama za kuzalisha umeme zinachangiwa pia na bei za mafuta ya kuendesha mitambo hiyo, bei ambazo ni za juu sana na kwa vyovyote zinabebewa na watumiaji umeme yaani wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha na mapendekezo yaliyomo kwenye maombi ya matumizi ya fedha za nyongeza. Yapo machache ningependa kuchangia, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara pamoja na uongozi mzima wa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, kwa sualala la umeme wa *IPTL*, ningeshauri kwa siku za usoni, *TANESCO* ione uwezekano wa kununua mtambo huo. Je, uamuzi wa Serikali wa kutaka kulitekeleza hilo, imefikia wapi? Je, suala la matumizi ya mkaa wa mawe kama njia mbadala wa umeme kwa siku za baadaye, zimeishia wapi?

Mheshimiwa Spika, suala la ndege ya Serikali ni muhimu kwa Taifa letu. Suala la bei, lisiwe kikwazo maana tunanunua ndege kwa ajili ya miaka mingi ijayo. Tungependa tununue ndege imara na ya kisasa na siyo ya mtumba kwa bei ndogo. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kuwa suala la chakula cha njaa ni budi kuchukuliwa kwa uangalifu. Tusingependa chakula kikawa chanzo cha maonevu, upendeleo na kuwa pia chanzo cha ubadhilifu wa fedha za umma. Tuangalie kuwa kidogo kitumike kwa uangalifu. Tusifuje kidogo kilichopo.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni jinsi ya usambazaji wenyewe unavyoendelea. Chakula kutolewa kwa wale ambao hata baadhi yao wana nafuu. Kila mmoja sasa analalamika! Hivyo wingi wa chakula siyo hoja, bali jinsi tunavyokigawa.

Lakini bado tatizo la Hifadhi ya Chakula cha Njaa au Maafa ni kitendawili. Kwa zaidi ya miaka 30, Serikali imekuwa ikishauriwa kuwa na akiba isiyopungua tani 150,000 (mia moja na nusu) ya nafaka kwa wakati wowote.

Lakini hadi leo, hakuna hata mwaka mmoja tulipowahi kufikia nusu ya tarajio hilo. Ndiyo maana kila mara tunapata tatizo la kuwahudumia wananchi kwa viwango vinavyoridhisha.

Nashauri, Serikali iandae utaratibu wa kuwashirikisha wafanyabiashara kuwa na *SGR* zao ambazo zitapewa unafuu wa kodi mbalimbali ili kusaidiana na Serikali, bega kwa bega.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono pia suala la kuwa na daftari la wapiga kura. Ni vizuri taratibu zianze kuandaliwa mapema ili daftari hili lisiwe chanzo cha migogoro ya kisiasa nchini.

Tayari baadhi ya maeneo nchini yameanza kutoa matamshi ya kuwataka baadhi ya wananchi warejee makwao kabla ya daftari hilo kuanza.

Mheshimiwa Spika, suala la fedha kutotumika kwa baadhi ya Wizara na taasisi, ni budi ufafanuzi wa kina ukatolewa ili kusiwe na wasiwasi kuwa baadhi yao wameshindwa kutekeleza majukumu yao waliyoahidi Bungeni.

Je, ni lini ufafanuzi huu utafanywa kama si wakati huu? Pia baadhi ya wahisani ambao hawakutoa fedha kama walivyoahidi, je, hili Wizara inalichukuliaje? Nashauri Bunge liwe linafahamishwa kwa kina.

Mheshimiwa Spika, mengine yote nayaunga mkono maana ni kwa faida ya Watanzania wenyewe. Tutafika, twende na wakati.

**MHE. LEPHY GEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri wa Fedha kwa kuwa makini, katika masuala mengi yahusuyo Wizara yake. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, suala la matumizi ya nyongeza *(Reallocation of Funds)* ni muhimu hasa kunapokuwa na matatizo kama haya ambayo yameikabili Serikali yetu kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko makubwa kuhusu ufuatiliaji wa fedha zinazotolewa kwa ajili ya Wizara nyingine. Mfano Wizara ya Kilimo kwa kiwango kikubwa inaonekana kushindwa mambo mengi.

Kumekuwa na lugha nzuri sana wakati wa uwasilishaji wa bajeti na wewe mwenyewe ukiwa unatupa matumaini ya mafanikio makubwa ya Serikali, mfano wakati wa uwasilishaji wa Bajeti hii tunayoendelea nayo ulipokuwa ukiiwasilisha ulisema nanukuu: “Bajeti hii ya safari hii imelenga na itawagusa sana watu wa kawaida Vijijini, hasa kwa suala la *subsidy* ya pembejeo katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini cha kusikitisha ni kwamba mambo yaliyojitokeza ni tofauti kabisa na maelezo yako, takwimu tunazo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara yako iweke utaratibu mahususi wa kufuatilia fedha zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Wizara mbalimbali, Wizara ya Kilimo inaonekana kushindwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

**MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku ya Sh.2.3m *USD* kwa *TRC.* Naunga mkono hoja hii. Hali ya reli zetu ni mbaya. Mabehewa mengi yameharibika kutokana na ajali mbalimbali, njia ya kupitia reli ni mbaya. Wafadhili wamesita kusaidia kwa vile *TRC* inaingia katika ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, ipo haja sasa kuweka mikakati ya makusudi ya kuifufua *TRC* kabla ya kufa ili mwekezaji atakayekuja kukodisha reli hii asije akachukua kwa fedha duni kabisa.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa wa kuona ni kwa namna gani *Road Fund* itasaidia kupewa *TRC* mgao au kasma fulani toka katika fund hiyo. Ikumbukwe kuwa reli zetu zinachangia mfuko huo kiasi kikubwa tu cha fedha ili kutengeneza barabara huku reli zenyewe zikinyimwa hata kasma chache za kukarabati reli zake.

Mheshimiwa Spika, kuboreka kwa reli na kuboreka kwa uchukuzi na usafirishaji kwa njia ya reli kutasaidia sana uhai wa barabra zetu kwa vile reli itabeba mizigo mizito ambayo barabara haitahitajika kuibeba.

Mheshimiwa Spika, engine za reli zetu ni za zamani sana na hata huko zilikotengenezwa hazitengenezwi tena. Sasa ni wakati muafaka kufikiria kununua vichwa vipya vya treni na mabehewa ya mizigo

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa Serikali imeziacha reli hizi zetu zote bila kuzisaidia muda mrefu *(TRC+TAZARA).* Dunia sasa ni ya ushindani. Ufanisi uliopatikana wa container terminal ya *THA* lazima uendane na ufanisi wa reli zetu ili tuhimili ushindani.

Mheshimiwa Spika, lengo la maelezo yangu yote sio tu kuunga mkono hoja hiyo ila ni kuonyesha namna gani reli zetu zikiwezeshwa zinavyoweza kuchangia katika uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, sasa bajeti ijayo ruhusa itolewe kwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kubajeti suala la ununuzi wa vichwa na mabehewa ya reli na *Road Fund* isaidie kasma fulani ya fedha ili zisaidie kukarabati vipuri na ununuzi wa mabehewa. Kwa ujumla Sh.2.3m *USD* ni chache lakini zitasaidia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kutoa bajeti ya nyongeza kwa ajili ya matumizi ya mambo muhimu ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana kutolewa fedha kwa ununuzi wa ndege ya Rais, naomba tena jambo hili lifanyike haraka na ikiwekekana zinunuliwe mbili ili zisichoke upesi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, naishukuru Serikali kutenga fedha kwa ajili ya janga la njaa Shilingi bilioni 10. Ninaomba fungu hili liongezwe kwani takwimu zinazotolewa na Watendaji wa Serikali siyo sahihi sana. Hata hivyo, takwimu hubadilika siku hadi siku, mfano Mkoa wa Singida njaa ni kubwa sana kuliko taarifa ilivyotolewa. Nashukuru sana kwa jitihada za Serikali kwa Mkoa wa Singida hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa fedha kuleta Muswada huu. Maeneo yote yanayoombewa fedha ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Wizara ya Nishati na Madini ijenge utamaduni wa kutoa maamuzi ya haraka kwa watu wanaoomba kuwekeza katika miradi ya umeme nje ya gridi ya taifa ili kutoa ongezeko la umeme nchini. Miradi midogo kama ya Kikuletwa Wilayani Hai, Mbalizi Wilayani Mbeya na kwingineko ipewe msukumo. Wizara ikishirikiana na *TANESCO* pia wafanye utafiti kuona uwezekano wa kupata maeneo mengine kama vile Kiwira huko Wilayani Rungwe na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme unaotumia makaa ya mawe wa Mchuchuma ni wa siku nyingi mno. Serikali imeangamiza fedha nyingi mno. Ni vizuri sasa watu waone vitendo. Vijiji vilivyoko Wilayani Songea, Ludewa na kadhalika wangeweza kufaidika kwa haraka. Umeme wa mkaa wa Kiwira Wilayani Ileje, Rungwe na Kyela ni mfano wa kuigwa. Mradi wa Mchuchuma pia ungeendelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chakula cha njaa, napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa inayofanya katika kuwasaidia wale walio na matatizo ya njaa. Serikali imejitahidi sana kutoa chakula na mbegu za mazao yanayokomaa haraka. Naamini hata wale ambao hawalimi na kula mtama au muhogo kwa hali iliyopo sasa watakula.

Napenda pia kuyapongeza Mashirika binafsi na ya dini yanayosaidia kusambaza chakula hapa nchini. Baadhi yao wametoa kama msaada. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri suala la upatikanaji wa fedha za kununulia mbegu za mazao yanayostahimili ukame liendelee kutiliwa mkazo hasa katika maeneo ambayo wakulima wamehamasika kulima mazao kama muhogo na viazi.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kutoa Shilingi milioni tano (5,000,000/=) kwa Wilaya za Mkoa wa Kilimanjaro kununua mbegu ya muhogo. Limetumwa ombi lingine la kuongezewa fedha kiasi cha Shilingi milioni tano nyingine kwa madhumuni hayo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri huo, naunga hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Ningependa kwanza kumshukuru Waziri wa Fedha kwa kuchukua hatua ya kuhakikisha Taifa letu pamoja na matatizo ya ukame yaliyopo nchini hakuna Mtanzania atakayekufa kwa njaa. Kwa hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali nawapa pongezi sana. Hivi sasa hali ya upungufu wa chakula ipo nchi nzima kwani hata wale ambao walikuwa na hali nzuri kipindi kilichopita hivi sasa wana upungufu. Nashauri chakula kitakachoagizwa sasa kisambazwe nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, katika hoja ya ununuzi wa ndege ya Rais, naunga mkono hoja na napongeza sana jinsi suala hili linavyozungumzwa kwa uwazi. Huu ni utekelezaji wa vitendo wa sera za CCM za ukweli na uwazi.

Mheshimiwa Spika, tatizo langu kubwa lipo katika suala la fedha za kulipia umeme, sina maana kuwa siungi mkono, isipokuwa malalamiko yangu ni namna Serikali inaposhindwa kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu ni wapi umeme wa Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara utatoka. Kitendo cha Serikali kushindwa kutumia fedha zilizobaki katika mkopo wa mradi wa Songo Songo ambapo zaidi ya Shilingi bilioni 64 zimebakia na wakati huo huo gharama za mradi wa kupeleka umeme kutoka Songo Songo kwenda Mikoa ya Kusini ni Shilingi bilioni 35 tu Serikali bado haioni umuhimu huo na badala yake kila jitihada zinafanyika ili fedha hizo zitumike katika maeneo mengine ya nchi yetu na kutuacha watu wa Kusini tukiwa hatuna umeme. Kwa lugha yoyote ile hii siyo haki.

Raslimali iliyopo Mkoani Lindi ishindwe kutusaidia sisi wenyewe, huu ni uonevu. Wananchi wa Kusini tunahitaji na kupenda maendeleo kama walivyo Wananchi wa Mikoa mingine, tatizo la barabara ya Kibiti - Lindi limetufanya tubaki nyuma sana kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa jitihada zake za kukamilisha ujenzi wa daraja la Mto Rufiji pamoja na miradi ya ujenzi wa barabara inayoendelea hivi sasa, lakini barabara pekee haitoshi, nishati ni kitu muhimu katika kuvutia wawekezaji. Hivi unawezaje kumshawishi mwekezaji kuja katika eneo ambalo halina umeme wa uhakika? Au katika suala la kuvutia wawekezaji sisi wa Mikoa ya Kusini hatumo? Kama tumo kwa vivutio gani na miundombinu gani? Tunaomba maelezo ya kina juu ya kigugumizi cha Serikali kutupatia umeme Wananchi wa Kusini kutokana na gesi ya Songo Songo kinatokana na nini?

Hoja ya umeme wa gesi ya Mnazi bay haina nguvu yoyote hasa ukizingatia kwamba hata kiasi cha gesi kilichopo hapo Mnazi bay hakuna mwenye hakika nacho. Kwanza, ufanywe uchunguzi wa kujua kiasi gani cha gesi kilichopo, uandikwe mchanganuo mzuri wa mradi, zitafutwe fedha za kuendeleza mradi huo na kisha taratibu za kutupatia umeme zikamilike.

Mheshimiwa Waziri, hivi kwa utaalam wako unadhani inaweza kuchukua miaka mingapi hadi mradi wa gesi ya Mnazi bay kukamilika? Je, ni kweli Serikali ipo tayari sisi tuendelee kusubiri kwa muda wote huo?

Mheshimiwa Waziri, kwa heshima kubwa naomba suala la umeme wa Kusini lipatiwe majibu yanayoeleweka kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao, vinginevyo itatuzushia hoja nzito wakati wa kampeni.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema tena kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri wa Fedha kwa kuleta Hoja ya Muswada wa Nyongeza ya Matumizi ya shilingi 87,250,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea juu ya matumizi kwa ajili ya kununua chakula. Suala la njaa lilijulikana tangu mwaka jana kabla ya kupitisha bajeti ya 2003/2004. Hali hiyo ilibainika kutokana na tabiri za hali ya hewa zilizokuwa zikitolewa na Idara ya Hali ya Hewa. Aidha, kama Serikali ingekuwa na utaratibu wa kupata taarifa za maendeleo ya kilimo hususan hali ya mazao mashambani, hali ya kutabiri uzalishaji wa chakula ingebainika mapema zaidi na hivyo kuiwezesha Serikali mapema kabisa kuweka bayana mahitaji ya chakula ili kuziba pengo la chakula hapa nchini na hivyo kuachana na kuleta *Supplementary Estimates.*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuuliza uko wapi mradi wa *Early Crop Monitoring* ulioanzishwa na Serikali kwa msaada wa *UNDP* na Benki ya Dunia? Mradi huu ulibuniwa kwa uadilifu kabisa na kama ungetekelezwa vizuri Tanzania ingeachana kwa sehemu kubwa kubaki na kubabaika katika ukadiriaji wa uzalishaji wa mazao ya kilimo na hasa mazao ya chakula. Tatizo kubwa hapa, mtindo unaoendelea wa kubuni miradi mizuri ambayo inatekelezwa ghafla bila maelezo au mapitio ili kubaini matatizo kama yapo kuliko kuleta mlolongo wa miradi iliyobuniwa vizuri yenye majina yanayovutia na pengine kama ingetekelezwa kwa umakini isingesababisha hali hii inayotupata sasa. Ni bora ijulikane kuwa si rahisi kupata mabadiliko ya haraka haraka katika kilimo kama ilivyo katika Sekta ya Viwanda, imechukua muda na dhamira endelevu ili kuleta mageuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha zinazoombwa ili kununua chakula, kwa bahati mbaya hata chakula kikipatikana haitakuwa rahisi kuwapelekea chakula hicho walengwa kwa vile wakati huu si muafaka ukizingatia hali ya barabara zetu zilivyo. Wakati huu wa masika barabara nyingi zimeharibika na mvua zinazoendelea hivi sasa. Ni vema utaratibu wa kugawa chakula cha njaa ufanywe wakati wa kiangazi hususan pale hali hiyo inapobainika mapema kama ilivyokuwa katika msimu huu kutokana na maelezo yangu ya awali.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ninawapongeza mno Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri wanayofanya hasa katika kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Waziri, ninaomba ufafanuzi kwa hizi fedha Shilingi bilioni 10 ulizoomba juu ya kilimo kulipia gharama za chakula umetumia kigezo gani? Ufinyu wa fedha, kipaumbele ama takwimu ya idadi ya wahitaji wa chakula?

Mheshimiwa Spika, naomba takwimu ziangaliwe upya ili kiwango hiki kiongezwe kuhakikisha tunapata chakula cha msaada na cha kupunguza bei ya chakula sokoni.

Mheshimiwa Waziri, pamoja na nia nzuri ya kuanzisha daftari la wapigakura; je, huoni ni vema ingekwenda pamoja na vitambulisho vya Watanzania? Ni gharama kiasi gani kuwa na daftari pamoja na vitambulisho?

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu umeme. Ni kwa nini tumeshindwa kuwa na mpango wa kutumia makaa ya mawe?

Mheshimiwa Waziri, hata hivyo, ninaunga mkono. Endelea kuchapa kazi.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, hali ya njaa Singida Kaskazini ni mbaya. Ninaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za ziada Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya njaa. Naomba chakula kipelekwe Singida Kaskazini mapema iwezekanavyo kuokoa maisha ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ndege ya Rais, naunga mkono hoja. Napendekeza inunuliwe ndege ya pili *(Presidential Fleet)* kuwezesha viongozi wengine kutotumia ndege ya Rais kwa safari za mbali. Ndege ya pili inunuliwe 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza, nawashukuru.

**MHE. DR. IBRAHIM S. R. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kujumuisha Wilaya ya Kibaha katika mpango wa chakula cha njaa. Kibaha ilipata tani 250 na hivi karibuni imetengewa tani 300.

Mheshimiwa Spika, hali ya chakula ni mbaya kuliko taarifa zinazotoka Wilayani na Mkoani zinavyoeleza. Siyo tu watu hawana chakula cha kutosha, lakini hata uwezo wa kununua chakula kilichopo madukani hawana. Kuna maeneo mengi tu ya Wilaya ya Kibaha watu wanashindwa hata kulipia Sh.50/= kwa kilo. Kuna haja kubwa ya kuongeza chakula, tani 300 hazitoshi. Aidha, ni vema kipelekwe pia chakula cha nguvukazi, hasa kwa vijana ambao hawana pesa, lakini wana nguvu za kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupeleka chakula kuna tatizo kubwa sana la ukosefu wa mbegu za muhogo, viazi, kunde na kadhalika. Bila ya kuweka mkazo kwenye upatikanaji na usambazaji wa mbegu, tatizo la njaa Kibaha litajirudia katika msimu ujao. Watu wengi wamejitahidi kulima, lakini hawana mbegu za kupanda hasa baada ya mbegu za awali kuungua na ukame.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kutuwasilishia hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza hoja hii kwa sababu suala la matumizi ya ziada (Mini Budget) ni suala la kawaida katika dunia. Aidha, Serikali haiwezi kuwaacha Watanzania wakiwa wanakufa katika janga la njaa lililosababishwa na hali ya hewa. Aidha, ninaipongeza Serikali kwa kutumia uwezo wa nidhamu ya kitaalam kwamba pamoja na bajeti hii ndogo, lakini haitaathiri kwa kuongeza kodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya ununuzi wa ndege ya Serikali hili halina hoja kwa sababu Bunge letu Tukufu tumekubaliana nalo mapema. Nashukuru Serikali hasa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutokuonyesha kutokuwa na matumizi au ufahari wa mambo tangu awapo madarakani mpaka kuelekea kustaafu kwake. Hivyo, hili tunalipongeza kwa niaba ya Watanzania wote. Hivyo, kimsingi hii siyo ndege ya Rais Mkapa, bali ni ndege ya Serikali itakayotumika kwa safari za Rais ikiwa ndani au nje kwa shughuli za Serikali ya Watanzania.

Mwisho, ninaipongeza *Mini Budget* hasa kwa mpangilio wake mahsusi. Ahsante.

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kuunga mkono hoja hii na kutamka kuwa matumizi haya yaidhinishwe yote bila ya kuchelewa. Haya ni matumizi ya kuokoa uhai wa Wananchi wetu ambao sasa wamekumbwa na jaala la njaa. Huu ni mtihani wa nchi yetu kwani kwa kuwa haya yanatukuta na angalau akiba tunayo basi namuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali isione kiwewe kutoa fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa masuala ya ununuzi wa ndege nataka nitamke kwa udhati wa moyo wangu hiki chombo kinunuliwe kwa umuhimu wake. Hii ndege si mali ya mtu na wala haitamfaa mtu maalum, ila itatufaa sote na Viongozi wetu na watakaojaaliwa wakiwa wazima na wagonjwa. Ninarejea tena kuomba Serikali itoe fedha kwa kuipa uwezo nchi hii kukabili majanga ambayo yametufika na hii ndiyo jaala pamoja na kununua ndege yetu.

Kwa kuwa janga la ukame limeleta uchache wa mvua na kushusha chanzo cha maji umeme kiasi cha kusababisha Serikali kutafuta njia ya gharama zaidi ya kupatikana umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umuhimu wa umeme sote tunautambua ni muhimu sana na lazima kwa maisha yetu sote na kwa maana hiyo Serikali imelazimika kutoa gharama ya mafuta ambayo tunatumia kwa kuendeshea mitambo ya kuwashia umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba fedha hizi ipewe Serikali kwa kutumia kama Wizara ya Fedha ilivyoomba.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na hasa zile fedha zitakazotumika kununulia chakula cha njaa. Nashauri fedha hizo zianze kutumika mara moja baada ya kupitisha tu bajeti hii ili kuokoa maisha ya Wananchi kutokana na baa la njaa. Serikali ichukue hatua za dhati kufuatilia kwa karibu na kwa haraka zaidi upatikanaji wa chakula ili Wananchi wasipoteze au kuendelea kupoteza maisha kutokana na njaa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukame Wananchi hawakuvuna mazao ya biashara, hivyo hawana fedha. Kuwategemea kununua chakula sio rahisi kwa sababu hawana fedha. Hivyo, chakula kitolewe bure kwa waathirika wote. Kama Serikali itaendelea kuwa na utaratibu mrefu au urasimu mkubwa wa upatikanaji wa chakula cha njaa nina wasiwasi kwamba hata baada ya kupitishwa kwa bajeti hii ya nyongeza maisha ya waathirika yatakuwa hatarini kwa kupoteza maisha kabla chakula hakijawafikia.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Liwale hali ni mbaya sana. Habari hazisikiki, ni kwa vile hakuna vyombo vya habari wala simu zinazoweza kuelezea hali halisi ya njaa Jimboni kwangu. Vijiji vilivyoathirika sana ni Nahoro, Nangano, Kibutuka, Mtawatawa, Minu, Kipelele, Kimambi, Mkutano, Kikalyungu, Ndapata na kadhalika. Hivi ninavyochangia hoja hii, ujumbe unaofuatilia chakula kutoka Liwale umefika Ofisi ya Waziri Mkuu; Dar es Salaam. Tumeahidiwa tani 100 za chakula ambazo mbali na kuwa hazitoshi, lakini pia upatikanaji una urasimu na kwamba hawajapata chakula hicho hadi sasa. Naomba sana chakula hicho kipatikane haraka. Liwale haifikiki kirahisi kwa wakati huu wa masika, hivyo ni muhimu chakula hicho kipatikane haraka kisafirishwe.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Basil P. Mramba, watendaji wake na wadau wote walioshiriki kukamilisha Muswada wa Nyongeza ya Matumizi 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye suala la kiasi cha fedha kinachoombwa cha Shilingi bilioni kumi (Sh.10,000,000,000/=) kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa chakula. Kiasi hicho ni kidogo kwa sababu sehemu kadhaa za nchi yetu wala bado hazijapata mvua za kutosha hata kwa msimu wa masika uliotarajiwa kuwa na mvua, hivyo hali ya ukame njaa itaendelea kuwepo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, zaidi, katika sehemu nyingine zenye njaa kwa sasa mvua zinazoendelea kunyesha zimeharibu barabara na kusababisha gharama za usambazaji chakula kupanda. Kwa msingi huo, naendelea kusisitiza kuwa kiasi cha fedha kinachoombwa hakitatosheleza mahitaji. Hivyo, nashauri fedha zaidi ziongezwe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine katika Muswada huo kuhusu fedha za chakula cha njaa ni kwamba, hata kama fedha zitatosheleza, lakini bado kuna tatizo la mfumo wa ugawaji chakula hicho katika maeneo husika kwa vile usimamizi wa maelekezo ya Serikali unalegalega kiasi kwamba walengwa hawapati huduma ipasavyo hasa wale ambao hawana uwezo wakiwemo, wazee, watu wenye ulemavu na kadhalika. Ninaishauri Serikali iweke msukumo zaidi juu ya maelekezo iliyotoa awali ili Wananchi wasifikie hatua ya kuilaumu na kuichukia Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, naunga mkono hoja kwa mategemeo kwamba fedha za chakula cha njaa zitaongezwa.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta makadirio haya ya nyongeza baada ya kuona upungufu wa hapa na pale.

Kuhusu chakula cha njaa, napenda niipogeze Serikali kwa kuonyesha nia ya kuwajali Wananchi wake hasa katika janga hili la njaa kutokana na ukame ulioikumba nchi yetu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuishi ni haki ya kila binadamu, lakini anahitaji (pamoja na vitu vingine) chakula na chakula hicho kiwe ni chakula bora na kiwe cha kutosha.

Kutokana na hotuba za Wabunge wengi waliochangia, inaonyesha wazi kuwa chakula kinachotolewa hakitoshelezi wala kukidhi haja ya kuitwa chakula bora. Hali hii inatokana na kwamba Serikali haina takwimu sahihi za watu wenye shida ya chakula na kiasi cha chakula kinachohitajika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, naunga mkono hoja za Wabunge kwamba ziundwe Kamati zinazojitegemea ili kufanya uchambuzi na uchunguzi ili kupata taarifa kamili za waathirika wa njaa na kiasi cha chakula kinachohitajika ili waweze kupata huduma inayolingana na tatizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, chakula si mahindi tu, mahindi tu hayatoshelezi bali vyakula kama maharage, kunde na karanga vinahitajika ili angalau kusaidia kukamilisha lishe. Ikumbukwe kwamba, miongoni mwa wenye njaa wamo watoto wanaokua. Sasa, kwa hayo mahindi tu yanayotolewa, watoto hawawezi kupata afya na kukua vizuri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maoni ya Wabunge ni wazi kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 10 zinazoombwa hazitatosha maana inaonyesha wazi kuwa Watendaji wa Vijiji, Kata na hata Wakuu wa Wilaya hawajatoa takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA SAID ALI MCHUMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake na hasa alipotuambia tupae kiuchumi badala ya kutembea. Hivyo, ni lazima Waheshimiwa Wabunge wote waunge mkono Bajeti hii ndogo ili kumudu kutekeleza yale yote yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Walimu kuajiriwa, suala la elimu halina mjadala, hivyo ni lazima Walimu wengi waongezwe kuweza kukidhi haja ya wanafunzi walioongezeka.

Mheshimiwa Spika, ndege lazima inunuliwe ili Rais wetu asidhurike anapotaka kutekeleza shughuli zake anazopangiwa hasa kufuatilia kutekeleza ahadi zake alizozitoa Mikoani, Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa chakula ni lazima kwa ajili ya kukabiliana na kupunguza njaa. Hii hoja ni muhimu kwa sababu itasaidia kutuliza Wananchi na kuweza kubakia na amani na utulivu nchini mwetu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe, Viongozi wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Viongozi wa upande wa Upinzani na kwa wewe kusimamia Bunge hili vizuri na kuhakikisha kwamba mambo yalikuwa salama hapa wakati wa mjadala. Nakushukuru sana na hawa viongozi kwa kukubaliana nasi kimsingi ila kama kawaida lazima wasionyeshe kufilisika kokote.

Kwa hiyo, lazima wachangie. Kwa hiyo, walichangia na michango yao tumeichukua na tutaifanyia kazi ikiwa ni pamoja na ile ya upande wa upinzani. *(Makofi)*

Pili, niwashukuru Wasaidizi wangu, Katibu Mkuu na Wataalam wake na Manaibu Waziri wangu kwa kazi nzuri waliofanya ya kusaidiana nami katika kukamilisha hoja hii.

Naomba nipokee kwa moyo mkunjufu shukrani, pongezi, hongera mlizomwaga ndani ya Wizara ya Fedha na hasa kwenye Mamlaka ya Kodi kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya ya kuongeza mapato. Wale waliosikiliza redio leo asubuhi kwenye kipindi cha Majira na kwenye magazeti ya leo mtaona ukusanyaji wa mapato unazidi kuboreka na nilikuwa nimesema kwenye hotuba yangu jana kwamba nusu ya kwanza ya mwaka huu wa fedha walikuwa wamekusanya ziada kwa 2% hivi sasa imefikia 3%.

Wiki hii wamekuwa wakikutana mpakani na Kenya kuzungumza na Mamlaka ya Mapato ya Kenya ni jinsi gani kwa pamoja wanaweza kusimamia ukusanyaji wa kodi. Taarifa ya awali inaonyesha kwamba ushirikiano huu wa Mamlaka ya Mapato Kenya na Tanzania utaongeza sana ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kupambana na magendo. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishieni tu kwamba tutaendelea kujitahidi kwa lengo la kukusanya mapato na kuweka akiba ili siku ya njaa kama leo tuweze kutumia akiba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda kidogo niongezee kwa kuwashukuru waliozungumza kwa haraka haraka nitaisoma tu walikuwa Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Profesa Dimon Mwaga, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Daniel Yona, Mheshimiwa Joseph Mungai na Mheshimiwa Charles Keenja. *(Makofi)*

Wale waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Abdullatif Esmail, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Sijamini Shaame, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Phillip Magani, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Fatma Said Ali na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, kama kuna mtu nimemsahau naomba msamaha.

Naomba kuwashukuru sana hawa wote waliochangia kwa msisimko mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nifunge kabisa mlango wa mjadala juu ya ndege. Kufunga kabisa mlango, maana ndege inaingia. Kwa ajili ya kumbukumbu zenu, kwa kifupi niseme kwamba kulikuwepo na namna ya kusema kwamba labda hii ndege ililetwa kwa haraka haraka, bila uwazi wa kutosha, bila utaalam wa kutosha na kwamba haikuwa na udharura. Yale mengine Profesa Mark Mwandosya, amenisaidia jana.

Lakini nasema ndege hii ilichaguliwa kwa utaalam na umahiri mkubwa kwa sababu iliundwa Kamati maalum ndani ya Serikali. Kamati ile ya wataalam wakiwemo wa ndege, wa Usalama wa Taifa, Makatibu Wakuu na watu wa namna ile wakapendekeza Serikalini katika mtiririko mkubwa wa ndege nyingi aina ya ndege ambayo ingefaa na ndege zile alizitaja Profesa Mark Mwandosya, jana. Serikali ikaamua tunataka kununua hiyo ndege inayoitwa *G5* ambayo ni *Gulfstream 5* siku hizi inaitwa G550, Serikali ikaamua hiyo ndio inaitaka.

*Next,* tulikwenda kuzungumza na watengenezaji wa ndege hiyo, ni mmoja tu, Kampuni ya *Gulfstream Aerospace Corporation* ya Marekani. Hawa tumekwenda kuzungumza nao, kupatana nao bei ndio zikatoka zile bei alizotaja Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, jana. Kusema kweli bei ile ilikuwa ya chini kuliko ilivyokuwa inanunuliwa kwenye soko wakati ule kwa sababu sisi tulikwenda moja kwa moja kwa mtengenezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ndege za *Gulfstream* za viongozi hazipatikani kwenye maduka sio za kutungua. Huwezi kwenda ukatungua ukachukua, zinatengenezwa kama vile unavyokwenda kushona suti kwa fundi, anakupima urefu upana na mambo yote yale yanayotakiwa ndio anakuletea ya kwako, ile uliyotaka na rangi na kila kitu kwa hiyo inachukua muda.

Kwa hiyo, ingawa tulipatana nao mwaka jana lakini sisi kwa sababu ya tatizo la fedha tuliwaambia tutalipa kwa mikupuo mitatu, mkupuo wa kwanza shilingi bilioni 9 ile iliyokuwa kwenye Bajeti, mkupuo mwingine mwezi huu wa tatu, mkupuo mwingine siku ya kuchukua. Siku ya kuchukua ni kati ya mwezi wa sita na tisa mwaka huu. *(Makofi)*

Mimi na Katibu Mkuu wangu tulikwenda *California Longbeach* juzi mwezi Desemba tuliona inakotengenezwa.*(Makofi)*

Aaah, ndio *California Longbeach* ndiko inakotengenezwa jinsi tulivyotaka sisi. Nina hakika inatengenezwa na nina hakika itafika kwa wakati tena kwa bei ya chini kuliko zote zilizokuwa zinauzwa wakati ule kwa watu wengine kwa sababu wanajua kwamba Tanzania ikinunua kitu na wengine watakuja kuiga kununua, maana sisi ni maarufu kwenye eneo hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ndege ina sifa gani, labda mjue pia, maana wala hii sio ya kwenda vijijini ina sifa gani? Hii inaitwa *Large Cabin Ultra-long Range,* ndio tuliyoichagua. Ndege yenye sifa hiyo katika makundi yote yaliyochaguliwa ni *Guldstream 5.* Ndege hii inaweza kwenda kilomita zaidi ya 11,000 bila kusimama kujaza mafuta yaani inaweza kutoka hapa ikaenda Ulaya, Japan bila kutua na kujaza mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale wanaojua habari za kujazajaza mafuta kwa viongozi wa nchi watajua kwamba mara nyingine anapita mkubwa hapa sisi Mawaziri au Waziri Mkuu au hata Rais anaamka saa nane usiku kwenda kumpokea, maana ndio time yake ya kupita pale Dar es Salaam. Haya mambo yamekwisha, hayako tena namna hiyo. Wewe ukishaingia hewani ni moja kwa moja mpaka huko unakokwenda, hapana kutuatua unakuja ku-*disturb* wenye usingizi na wewe ni Rais wa nchi, haitakiwi mambo ya namna hiyo, ndio hiyo tuliyoitaka. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuambieni hadithi nyingine. Kuna siku Rais wetu alikuwa anakwenda Namibia akatua pale Lusuka kujaza mafuta ndio ndege yetu ilivyo sasa hivi Rais wa Zambia akampokea kisha akamuaga kisha na yeye akaingia kwenye ndege yake akamtangulia tena kule Namibia. Rais wa Tanzania, Tanzania yetu hii kweli tunaweza kushindwa kumsafirisha Rais namna hiyo? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inakwenda kasi, inaruka mpaka umbali wa futi 51,000 juu ya usawa wa bahari, juu kabisa, ikipita huko ni kutulia tu, ni poa huko juu hakuna tena mtu kutizama hata mwenye mshale hajaribu, hakuna. Kwa hiyo, ni ndege ya heshima inastahili Rais yeyote. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nataka mjue la pili, ni hili ambalo linaambatana na *radar.* Mnakumbuka mjadala wetu hapa juu ya *radar.* Aliyesoma gazeti la *The East African* la wiki iliyopita na *The East African* ya wiki hii ataona wanavyotusifu Tanzania kwa sababu anga zetu hapa ni salama na ndege zinaweza kupita kwa umbali wowote bila wasiwasi. Lakini wanaisema nchi fulani, sitaki kuitaja kwenye dude hili. Kule ni hatari ndege zinanusurika kila siku kugongana kwa sababu *radar* yao ni mbovu, vifaa vyao ni vibovu, utaalam hakuna.

Wanasema matokeo ya Tanzania kujulikana duniani kwamba kuna *radar* inayoaminika ndege za dunia nzima zinatua hapa sasa bila wasiwasi kabisa usiku, mchana, wakati wa mvua, wakati wa mawingu na maana yake ni kwamba biashara inaongezeka na uchumi utakua. Mambo haya ya uchumi sio lazima moja kwa moja kama unavyolima kwa jembe. Yanakuja kwa mlango wa nyuma, kwa mlango wa mbele kwa kila njia ili mradi mazingira ni sawa. Ndio mambo tulikuwa tunazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba habari ya ndege tuimalizie hapa leo, tulale salama tusubiri ije na mambo yetu yaende vizuri. Wala hakuna hila, wala hakuna lolote lililofanyika ambalo haliko kwenye taratibu za kisheria za Tanzania ambalo halina utaalam na ambalo limefanywa tu kwa rojorojo na legelege,

hapana. Nashukuru kwamba sasa tumefunga mlango wa ndege tunazungumza yajayo labda, ndege ya pili, lakini sio hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hili la dhahabu nalo lilizungumzwa, ooh, unajua haliwezekani, uwazi huu, namna gani na hivi. Kwanza niwaelezeni kulinganisha dhahabu na almasi ni sawa na kulinganisha jogoo na dume la ng'ombe. Wewe unapochinja ng'ombe unatoa ngozi, unakata vipande yote ni madume lakini jogoo huchuni, jogoo hana ngozi ya kuchuna unakwenda haraka haraka unamaliza ni kazi ndogo hii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, dhahabu inachimbwa, inachemshwa. Kule ndani kuna madini ya aina tatu. Kuna shaba, kuna fedha na dhahabu yenyewe kwa *proportions* tofauti. Kazi hii ni ya kuchambua dhahabu kiasi gani ipo, *silver* kiasi gani, shaba kiasi gani na zinauzwa kwa bei gani kila siku na hizo fedha zinaenda wapi na kule zinatumikaje. Lakini almasi ni jiwe gumu tu peke yake halina cha kuchambua wala kuchemsha zinakuja. Pale ni kwenda kukata tu na ku-*polish* na kuuza, vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, huwezi kukadiria namna ya kutambua dhahabu na namna ya kutambua almasi kitaalam kwa lugha hiyo ya wataalam.

Mheshimiwa Spika, tunachotafuta ni gharama za uzalishaji wa dhahabu kwa sababu watu wanaweza kurundika ile gharama wakaja kukataa kulipa kodi yangu kwa sababu wataonyesha hasara bandia. Kwa hiyo, kodi ya mapato hawatalipa. Hii sheria nitakayoileta kipindi kijacho inaangalia jambo hilo. Usijidai ulipata hasara eti kwa sababu ulifanyafanya ujanja, tutakutambua. Kazi mojawapo ya hii ni kuhakikisha kwamba yale makampuni yasijidai yanapata hasara. Sisi kwa kufuatilia mtiririko wa uzalishaji na mauzo na bei za dunia wakati ule tutajua huyu ni mwongo tutamfanyia *investigation* ndio kazi ya watu wa kodi.

Mheshimiwa Spika, pia tunatafuta fedha hizi zinapokwenda mtiririko wake uko vipi. Kuna nyingine zinawekwa kwenye *Escrow Account* kulipa madeni ya haya makampuni, kuna nyingine zinatumika huku, je, ziko namna gani. Kwa hiyo, ni kazi inayofanywa kwa kujenga maabara kubwa za kitaalam na ni kazi za siri sio kila mtu anaweza kwenda pale na wale wanaofanya kazi hii wanafanya kwa usiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaambia ingawa ni mapema mno lakini tayari kazi ambayo inaendelea imetuonyesha kwamba eeh kumbe kidogo tungechelewa kuajiri watu hawa. Kuna kitu tunachotaka kuonaona lakini ni mapema mno kukisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa asilimia zake ni 1.9% ndio namna ya kuwalipa hawa. Wameajiri watu chungu nzima na wanakagua migodi yote hii kwa umahiri huo wa kutumia *laboratory,* sheria, utaalam wa madini na hesabu.

Mheshimiwa Spika, namna ya kuwapata ilibidi tufanye matangazo yale ya kwenye Sheria ya *Procurement* sio yale ya kutangaza kwenye *Daily News* ile ya kujua maana watu hawa sio wengi duniani. Sisi tulijua watu wanane tukawapelekea barua, haya leteni mapendekezo. Tukachambua nani kati ya hawa wana ukoo na wenye madini maana kama wana ukoo watawapendelea, sisi hatutapata nafuu. Kwa hiyo, tukagundua kati ya hao wanane, watatu walikuwa na ukoo, *bye, bye,* tukawaondoa kwenye orodha tukabaki na watano. Kati ya wale watano watatu wakasema hii kazi ni ngumu hatuiwezi, tukabaki na wawili. Kati ya wawili mmoja akachambuliwa na Wanasheria wa Tanzania na wataalam wetu wa Benki Kuu Tanzania wakaja na mmoja ambaye *technically and financially* alitoa masharti nafuu kuliko mwingine yeyote. Tukamwajiri, akaanza kazi na ndio hiyo nimesema kwamba tumeanza kuwa na matumaini kwamba anafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kazi hii inafanyika kwa usiri fulani, umahiri fulani lakini lengo letu ni kujibu ile hoja yenu hapa. Ninyi hapa ndio mlimsumbua sana huyu ndugu yangu hakulala wakati ule wa Bajeti ya madini, hakulala huyu bwana huyu. Nikamwambia nitakusaidia ndugu yangu mimi nitakutafutia watalaam watakusaidia kazi. Nikamletea wataalam, nimemkabidhi yeye, sasa ndio anapokea taarifa zile, ni vitabu vikubwa vitatu tu ni urefu wangu, makubwa, anayasoma huyo bwana na kutufanyia *summary* na kutuletea sisi tunaohusika. Anapeleka nakala kwangu, Benki Kuu na yeye anabaki na nakala kwa sababu pia ni siri.

Kutokana na ile sasa sisi ndio jukumu letu kuripoti Serikalini mambo yanavyokwenda. Kwa hiyo, mimi nilifikiri mtupongeze kwa sababu kwa kweli hakuna lolote ambalo ni la kutia wasiwasi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya naomba mtupe muda sisi wenyewe tuweze ku-*draw conclusions,* hatuna *conclusions,* ni faida gani, ni hasara gani hata sisi hatuwezi kujibu hilo kwa sababu hatukujua ni kitu gani kilichokuwa kinafanyika ndani ya migodi hiyo, tutajua baadaye. Tukiona kwamba hasara ya kufanya kazi hii ni kubwa kuliko faida tutaacha na tutawaeleza tukiona kwamba faida ni kubwa kuliko athari tunayopata. Sasa tutaendelea kufanya na tutawaeleza.

Kwa hiyo, naomba mtuamini kwamba tumejibu hoja yenu ni Serikali sikivu, inajibu hoja za Wabunge. Hili la dhahabu naomba mtupe muda kwa sababu tunataka kuangalia na uwezekano wa kusogea kwenye aina nyingine za madini, sio dhahabu tu, hatujamaliza tunaendelea kufikiria. *(Makofi)*

Kuhusu njaa, ndugu yangu amelieleza vizuri, haya ya kutawala njaa mimi siwezi kujua. Mimi nataka kusema hivi tumesikia mlivyosema hapa. Kwa kifupi ni kwamba njaa bado ni kali, inahitaji fedha zaidi na inahitaji utawala bora zaidi, ndivyo mlivyokuwa mnasema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesikia, Mheshimiwa Charles Keenja amesikia na ameeleza. Mimi kazi yangu ni kutoa fedha. Rais alitoa ahadi hakuna upungufu wa fedha na mimi nasema ni kweli. Fedha ziko wapi? Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, fedha ninazozitoa kati ya sasa na mwezi wa sita siyo shilingi bilioni 10, shilingi bilioni 10 ni zile ninazoomba kupitia Muswada huu. Ni shilingi bilioni 24.5 yaani wastani wa shilingi bilioni 5 kwa mwezi, hela nyingi sana hizi. Hebu fikiri shilingi milioni 5,000 kwa mwezi kulisha Watanzania hao ni hela nyingi, zikienda vizuri, zikitawaliwa vizuri, zitaponyesha watu njaa, hakuna ulazima wa kula mizizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia ni shilingi bilioni 24.509 ndio hela kati ya sasa na mwisho wa mwezi wa sita. Itapatikana hata kama nitakuwa nimekufa atateuliwa mwingin.*(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hela iko hata kama sina ziada ndani ya Benki Kuu au mifuko yangu mingine nina uwezo wa kukopa, sheria inaniruhusu. Angalieni Kifungu cha 5(1) ndani ya Muswada huu kinaniruhusu kukopa na nimesema, huu Muswada unaofuata hapa, nimesema endapo itatokea bahati mbaya kuliko zote hela ikaisha mimi naruhusiwa kwenda kukopa hela na naomba mniruhusu na sheria inaniuhusu kukopa.

Kwa hiyo, hakuna wasiwasi watu walale, wasali mvua zije, ndio jambo kubwa zaidi, wasali sasa mvua zije. Namshukuru yule Sheikh Mkuu wa Tanzania, aliyeanzisha jambo hili la kusali. Tusali, salini mvua ije na fedha ziendelee kupatikana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wake ukoje? Shilingi bilioni 2.2 ziko kwenye Bajeti ya Serikali ya sasa hivi, shilingi bilioni 10 ziko kwenye Hati ya Matumizi ya Nyongeza ambayo ndio nimeileta, shilingi bilioni 10 nyingine zimetengwa kwa njia ya uhamisho wa ndani kwa ndani hii hata Baraza la Mawaziri nililieleza wanajua, shilingi bilioni 2.3 zinatolewa kwa Mamlaka ya Reli isafirishe vyakula. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Charles Keenja inatoka Mpanda, Tabora, Dodoma, Singida, Shinyanga na katika kasma ya dharura chini ya Wizara ya Fedha kuna mapendekezo mengine ya shilingi bilioni 10 ambazo kati ya hizo naweza kutumia pia kwa chakula.

Kuna wahisani kama alivyosema Mheshimiwa Charles Keenja, ambao wameahidi kuendelea kuleta vyakula na vinakuja kama alivyosema Mheshimiwa Charles Keenja na kama nilivyosema kama haya yote hayatatosha ndani ya miezi hii minne inayokuja basi ndio tutaangalia nini tena kifanywe ili tuweze kukabiliana na hali hii. Kwa kweli nina hakika na natumaini kwamba Waziri Mkuu atakapozungumza anaweza kutoa kauli zaidi juu ya utawala wa njaa.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* mnawapa mkopo ama msaada? *Point* tunaichukua, tutaifanyia kazi, kwa sasa hivi tusizungumze hayo. *TANESCO* ni Shirika la Serikali mia kwa mia bado halijabinafsishwa. Ni Shirika la Serikali sasa kazi yetu kubwa ni kuliwezesha kufanya kazi iliyopo baada ya hapo tutazungumza. Mimi naona ipo hoja ya kuzungumza habari za mkopo lakini siwezi kuitamka maana ni lazima niende nikazungumze na wenzangu tuelewane lakini hoja hiyo naichukua.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja iliyotoka hapa Walimu mbona wanazidi kudai *arrears* hazijatoka na kadhalika. Jibu, Walimu watulie tulikuwa tumeshaanza kutoa tayari zile *arrears* ambazo tayari zilikuwa zimekaguliwa kukatokea balaa kidogo tukasimamisha lakini jambo hili likishaisha tutaendelea tena kutoa fedha kwa Walimu kama ilivyokuwa imepangwa. Walimu wenyewe wanajua kwamba kuna jambo lililotokea kutokana na malipo haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *PPF,* kwa nini tusichukue hatua za kisheria. Tayari sheria tuliyoileta hapa mwaka juzi inampa Waziri wa Fedha mamlaka ya kuchukua hatua kwa watu wanaochelewesha fedha za makato ya wafanyakazi badala ya kuzipeleka *PPF.* Hilo tayari liko kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, je, uhamisho huo wa ndani kwa ndani hautaathiri tena Bajeti yenyewe, jibu ni hapana. Uhamisho wa ndani kwa ndani kama nilivyosema unagusa kasma ambazo hata tungeahirisha kwa miaka miwili hakuna madhara yatakayotokea makubwa ndani ya Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, vifupisho vile alivyosema Mheshimiwa Dr. Talala Mbise, ni sawasawa lakini sisi tulitaka kuonyesha vyanzo vile lakini vyanzo vile maana yake ni kwamba fedha zilizopatikana kwa njia hizo zilikuja wakati ambapo tulishamaliza bajeti ya mwaka 2003/2004.

Kwa hiyo, hatukuzihitaji tena na kwa hiyo, ni kama *bonus* na tunazitumia lakini zote ni fedha zilizokuja kwa njia hizo kwa ajili ya kuimarisha bajeti ya Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie fidia kwa Serikali za Mitaa. Nafurahi kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa kazi kubwa waliofanya wataalam wa Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Fedha baada ya kuajiri Chuo Kikuu cha Georgia ambacho ni Chuo cha Andrew Young yule Balozi mashuhuri, chuo kile kimetuletea *formula* ya namna ya kugawa mapato haya Halmashauri kwa Halmashauri. Tuna *study* ambayo imetupa *formula* na Serikali imekubali *formula* hiyo na ndio tunayoitumia sasa kugawa hizo fedha kwa njia ile ya haki toka Halmashauri moja mpaka Halmashauri nyingine. Kwa hiyo, hatugawi kwa matakwa ya ile Halmashauri wala kwa hisia za Halmashauri fulani wala kwa mahitaji ya Halmashauri ni kwa *formula* inayohakikisha kwamba mfuko uliopo unaweza kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, nafikiria kutumia *formula* hiyo hiyo baada ya wataalam tena kuingalia kwa undani kama inawezekana kwa ajili ya ile hoja nyingine iliyo hapa ya namna ya kugawa mapato baina ya Mikoa. Ni *formula* nzuri na tunafikiri kwamba inaweza kutusaidia sana. Kwa hiyo, hilo kama nilivyosema tulishaanza kutoa fedha. Mkupuo ujao ni mwezi Machi na tutapeleka zote ili zikafanye kazi huko Wilayani mwetu mpaka mwisho wa mwezi Juni.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kusema kwamba kwa kweli jambo hili la njaa na umeme katika uchumi wetu na elimu ya watoto wetu walioshinda mitihani ya darasa la saba ni makubwa kwa jamii, Taifa letu na kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania. Sisi kama Serikali hatungeweza kukaa kusubiri Bunge hili, tulianza kutumia, tulianza kutafuta hela kwa imani kwamba ninyi mna imani na sisi, kwa imani kwamba hatukuiba, kwa imani kwamba hatukufanya ubadhirifu, kwa imani kwamba tutasimamia fedha hizi tukishirikiana na wenzetu katika Wilaya, katika vijiji na katika Mikoa.

Naomba mrudi nyumbani kwenu kifua mbele mkijua kwamba mmepata nguvu ya ziada ya shilingi bilioni 176 bila kuingia mfukoni mwa mtu. Sio rahisi, inaonyesha kwamba utawala wa uchumi na fedha ndani ya nchi hii sasa umekwenda kama Rais alivyokuwa anataka. Kidogo mtaona ndege ikiruka, hii ndio njia ya kuelekea kwenye ndege kukwea kama Rais alivyoahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba hoja niliyotoa hapa ikubalike ili tuweze kuendelea na kazi iliyobaki, ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa mjadala sasa tunahitaji uamuzi wa Bunge na hoja ni kwamba Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza kwa mwaka 2003/2004.

Hii ni Bajeti ndogo na wakati fulani niliwasomea Kanuni inayosema kwamba masharti yanayotawala Bajeti kubwa vile vile yatatawala na Bajeti ndogo isipokuwa sharti moja nalo ni la namna ya kupiga kura.

Katika Bajeti kubwa Kanuni inasema: "Ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 90(2)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kura zitapigwa kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja." Ili kukidhi matakwa ya Katiba, matakwa hayo ya Katiba hayatawali *Supplementary Estimates* kwa hiyo tutapiga kura kama kawaida yetu kwa kuwahoji wanaoafiki waseme Ndio na wasioafiki waseme Sio, hatutaita majina mmoja mmoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Nyongeza kwa mwaka 2003/2004 yalipitishwa na Bunge)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo nayo niwafafanulie kwa mujibu wa Kanuni zetu zinasema: "Baada ya Bunge kuwa limekamilisha kazi yote ya kufikiria Makadirio ya Matumizi au Matumizi ya Nyongeza basi ule Muswada wa Matumizi ambao ndiyo unaitwa *Appropriation Bill,* utawasilishwa Bungeni na kupitishwa kwa mfululizo katika hatua zake zote.

Kanuni inasema Muswada wa aina hiyo hautapelekwa katika Kamati inayohusika yaani ile Kamati ya Mheshimiwa Njelu Kasaka na wala hautapelekwa kwenye Kamati ya Bunge Zima. Unapitishwa tu kwa mfululizo. Kwa sababu kama nilivyoeleza inaidhinisha kisheria tu yale ambayo tumeshayakubali kama Bunge. Kwa hiyo, sasa Muswada usomwe Mara ya Kwanza.

**Muswada wa Sheria ya Nyongeza ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2003/2004** ***( The Supplementary Appropriation for Financial Year 2003/2004 Bill, 2004)***

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Nyongeza ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2003/2004** ***(The Supplementary Appropriation for Financial Year 2003/2004, Bill, 2004)***

*(Kusomwa mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya shilingi 87,250,000,000/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Ziada ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada ulioko mbele yenu ni kuomba Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 ili kuiwezesha Serikali kugharimia mahitaji ya dharura yaliyo nje ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2003/2004, lakini ambayo ni lazima Serikali iyatafutie fedha kwa manufaa ya Taifa na ustawi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pamejitokeza hali isiyokuwa imetarajiwa wakati wa kuandaa Bajeti ya sasa ambayo imesababisha matumizi yasiyotegemewa, na hivyo kuilazimu Serikali kuyaombea kibali kipya kwa vyanzo na matumizi yenyewe. Shilingi 87,250,000,000/= zinahitajika kuziba mapengo katika Wizara

tatu, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Hizi imebidi zitokane na vyanzo vipya.

Kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula tumetumia shilingi bilioni 6.8 zaidi ya Bajeti iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya chakula cha njaa. Inakadiriwa kwamba dharura ya chakula kwa ujumla kabla ya mavuno yajayo itahitaji shilingi bilioni 24.5 kama nilivyokuwa nimeeleza hapo awali. Lakini kwa Wizara ya Kilimo na Chakula naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe shilingi bilioni 10 kwa utaratibu huu.

Kwenye Wizara ya Nishati na Madini Serikali ililazimika kuongeza ruzuku kwa *TANESCO* ili kuiwezesha kununua umeme wa mtambo wa *IPTL* na kuendesha mitambo yake ya Ubungo. Hadi mwisho wa mwezi Desemba, 2003 shilingi bilioni 16.3 za ziada zilikwishakutumika kwa ajili hii na shilingi bilioni 12 nyingine zilitolewa mwezi Januari, 2004 na kufanya jumla ya shilingi bilioni 28.3. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 15 ambazo *TANESCO* ilikuwa inadai Serikali ya Muungano na sasa Serikali haina tena deni la umeme kwa *TANESCO*.

Hata hivyo, kwa kuwa mabwawa ya maji yanayozalisha umeme hayakujaa vya kutosha kama tulivyoambiwa leo asubuhi. *TANESCO* inaendelea kununua umeme kwa *IPTL* na kwa kuwa hakuna uhakika wa lini tatizo la uhaba wa maji ya kuzalishia umeme litakwisha Serikali inaomba idhini ya Bunge hili Tukufu ya kutenga kiasi cha shilingi 37,250,000,000/= kwa ajili ya kusaidia *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Serikali ilifanya mazungumzo na Kampuni ya *Gulfstream Aerospace Corporation* ya Marekani ambayo ndiyo ilishinda mchunjo wa zabuni. Ndege iliyonunuliwa ni kwa bei ya dola za Kimarekani milioni 46.2 pamoja na programu ya matengenezo, mafunzo, huduma za matibabu ya dharura na sifa nyingine nyingi. Malipo ya awali ni dola za Kimarekani milioni 9 kutokana na fedha zilizokuwa zimetengwa katika Bajeti na ndege inatarajiwa kuwasili kati ya mwezi Juni na mwezi Septemba, 2004. Kiasi kinachoombewa matumizi ya ziada ni sawa na dola za Kimarekani milioni 37.2 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 40.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sijapata maombi yoyote ya kuchangia. Kwa hiyo, sasa nitawahoji kuhusu hoja iliyotolewa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa Muswada hauendi kwenye Kamati ya Bunge Zima kwa mujibu wa Kanuni, sasa Mheshimiwa Waziri atatoa hoja kwamba Muswada huu ukubaliwe. Mheshimiwa Waziri. Lazima ipite katika hatua zote tatu.

**Muswada wa Sheria ya Nyongeza ya Matumizi ya Fedha kwamwaka wa Fedha 2003/2004** ***(The Supplementary Appropriation for Financial Year 2003/2004 Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, baada ya kuwasilisha Muswada wa *The Supplementary Appropriation Bill for Financial Year 2003/2004* na Waheshimiwa Wabunge kutohoji, inaonekana wameukubali bila mabadiliko. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Muswada huo ukubaliwe rasmi.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hatua hiyo imekamilika. Sasa tunakwenda kwenye *agenda* inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

## HOJA YA KUJADILI HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA BENJAMIN W. MKAPA

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuijadili hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliyoitoa ndani Bunge lako Tukufu tarehe 12 Februari 2004.

Kabla sijaendelea na maelezo ya hoja yangu, naomba na mimi nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuliwakilisha Bunge na nchi yetu kwa ujumla katika Bunge la Afrika. Nao ni Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Getrude Mongella, Mheshimiwa Dr. Amani Walid Kabourou na Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi. Sote tuna imani kubwa nao kuwa wana uwezo wa kusukuma mbele na kutetea maslahi ya Bara letu katika mazingira ya utandawazi na mabadiliko makubwa ya kiteknolojia na Demokrasia Barani Afrika.

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kuwa mwakilishi wetu katika Bunge la *SADC.* Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara baada ya hotuba ya Mheshimiwa Rais wewe uliielezea hotuba hiyo kuwa ni *authoritative, comprehensive and inspiring.* Mimi naungana na wewe na ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu pia wataungana nawe katika usemi huo. Hotuba ile inatuonyesha tulipotoka, tulipo na tunapotarajia kwenda na kufika. Kwa kweli ni hotuba iliyojitosheleza na haihitaji maelezo marefu sana ya ufafanuzi.

Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri sana ambayo imegusa karibu sekta zote katika utekelezaji wa Serikali, ujenzi wa demokrasia na mahusiano yetu na nchi jirani zetu na mengineyo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi sana hotuba ya Mheshimiwa Rais imegusia vipengele muhimu vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya siasa kama alivyosema Mheshimiwa Rais, tumefanikiwa kujenga nchi yenye umoja wa Kitaifa ambao umesaidia kulinda na kuendeleza amani na utulivu. Aidha, Muungano wetu umeendelea kuwa kielelezo cha matumaini ya Umoja wa Bara letu la Afrika. Ni vyema mazingira haya ya kisiasa nchini yakaendelezwa na kwamba kushauriana na kuelewana ndiyo msingi mkubwa wa mwelekeo wa siasa tunazopaswa kuzijenga. Hata hivyo, ameeleza kuwa udhaifu wa Vyama vya Siasa vya Upinzani na kauli za baadhi ya Viongozi wa Kisiasa na wanachama wao wasiojali amani ndiyo vitu viwili vinavyotia dosari katika maendeleo yetu ya kisiasa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali za Mitaa sote tumeshuhudia mabadiliko makubwa yanayotokea katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Rais ameeleza jinsi Serikali inavyozijengea Mamlaka hizi uwezo wa kimapato, kielimu na kiutendaji. Haya yote yamewezekana kwa vile Serikali imetekeleza kwa vitendo matakwa ya Katiba ya kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakuwa kweli vitovu vya madaraka ya wananchi. Maboresho mbalimbali yanayoendelea chini ya

Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ni kielelezo cha dhamira ya Serikali kuziimarisha Serikali hizo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine alilolisisitiza Mheshimiwa Rais ni lile la kuwataka viongozi na watendaji wa Serikali Kuu na wale wa Serikali za Mitaa kubadilika kifikra na kuchukua hatua za dhati zenye mwelekeo wa kuvutia wawekezaji katika Sekta mbalimbali na katika maeneo yao. Lengo la hoja hii ni kututaka Watanzania tutambue kuwa chanzo cha maendeleo ni uwekezaji, uzalishaji, huduma na biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya uchumi sisi sote ni mashahidi wa jinsi uchumi wetu unavyoendelea kuboreka. Mheshimiwa Rais ametueleza kwa takwimu zenye kuonyesha ongezeko la uwekezaji, ongezeko la ukuaji wa Pato la Taifa, ongezeko la ukusanyaji wa kodi na kupungua kwa mfumuko wa bei.

Aidha, Serikali imeweza kurejesha mahusiano mazuri na nchi wafadhili na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa ambao mchango wao umesaidia sana katika kutujengea mazingira ya kukopesheka na kuweza kupata misaada mbalimbali. Hatua mbalimbali pia zimechukuliwa kuimarisha nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali na Utawala Bora.

Uchumi mpana na tulivu ni nyenzo muhimu sana ya kuvutia uwekezaji, kuchochea ukuaji wa uchumi, kupanua nafasi za ajira, kuongeza mauzo ya nje, kuongeza mapato ya Serikali na kuongeza misaada ya nje pamoja na mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amezungumzia pia vita dhidi ya umaskini. Lengo kuu la Dira ya Taifa ya mwaka 2025 ni kupiga vita umaskini. Mheshimiwa Rais ametoa changamoto kwetu sote kuwa umaskini wa kipato kupigwa vita na kila mtu kwa kujituma kufanya kazi. Serikali itajitahidi kuweka mazingira bora ya kidemokrasia na kiuchumi ili kuwawezesha wananchi kujiendeleza, lakini haiwezi kugawa fedha kwa wananchi. Ni jukumu na wajibu wa wananchi kutumia fursa zilizopo ili kujiletea maendeleo na kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ushirika kama Waheshimiwa Wabunge wanavyoelewa tunayo sheria mpya ya Ushirika yenye lengo la kutuwezesha kujenga Ushirika imara, unaosimamiwa na kuendeshwa na wanachama wenyewe. Mheshimiwa Rais amesisitiza nia ya Serikali ya kuvisaidia Vyama vya Ushirika kimitaji kupitia utaratibu wa udhamini wa mikopo kwa mauzo ya nje. Ni muhimu kwa Vyama vya Ushirika kujijengea uwezo kimtaji kwa njia ya hisa na akiba zitokanazo na utaratibu wa kuweka na kukopa.

Aidha, Serikali itaweka mkazo kwenye ukaguzi ili kulinda mali na fedha za wanachama. Hata hivyo, ametutaka sisi Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na wananchi ili kuwawezesha wajiunge na Ushirika na wausimamie vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu ya Msingi yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Sekta ya Elimu ya Msingi katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Tumeanzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ambao umetupa matumaini makubwa kuwa tutaweza kuyafikia malengo ya dunia ya Elimu ya Msingi kwa wote ambayo yamepangwa kufikiwa mwaka 2015 sisi kuyafikia katika muda mfupi wa miaka miwili ijayo yaani mwaka 2006.

Mheshimiwa Rais aliwaalika na kuwatambulisha kwetu watoto wa Kitanzania waliofanya vizuri katika mitihani ya kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita. Aliwatumia vijana hao kutoa ujumbe kwa watoto wote wa Kitanzania kuhusu dhamira ya Serikali yake ya kuendeleza elimu na kuwaandaa vijana wetu ili wawe viongozi bora wa baadaye.

Mheshimiwa Spika, katika Elimu ya Juu Mheshimiwa Rais alitueleza kwa takwimu kupanuka kwa elimu hiyo kwa ongezeko la Taasisi na idadi ya wanafunzi hususan wa kike na umuhimu wa Mfuko wa Elimu kama nyenzo ya kuwezesha elimu kwa Watanzania wote bila ubaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Afya Serikali imeweza kuleta mabadiliko makubwa ya Mfumo wa Huduma za Afya, Ukarabati wa Taasisi za Afya na upatikanaji wa chanjo. Kwa mfano, hali ya chanjo nchini imefikia asilimia 83 na hivyo kuzidi kiwango cha asilimia 80 ambacho kinakubalika Kimataifa.

Mheshimiwa Rais ametoa changamoto kuwa kutokana na dhamira yake ya kupeleka madaraka zaidi kwa wananchi katika utoaji wa huduma za afya ni vyema Bodi na Kamati za Afya zianzishwe nchini kote katika muda mfupi iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ukimwi, suala la Ukimwi si geni tena kwa Watanzania na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais alieleza kuwa mwamko katika jamii kuhusu Ukimwi umeongezeka. Hata hivyo, vita dhidi ya Ukimwi vinahitaji ushiriki wa kila mmoja wetu hasa sisi viongozi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji utekelezaji wa sera ya Taifa ya Maji ambayo imesisitiza umuhimu wa kuwashirikisha wananchi katika kupanga, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi ya maji imeanza kuonyesha mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Rais ametueleza mafanikio yanayoonekana kwa wakazi wa mijini na vijijini na kubwa linalojitokeza ni ongezeko la wananchi wanaopata maji safi na salama hasa ikiwemo miji yetu minne Tanzania Bara na jitihada za pekee zinazofanywa kwa Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo hali ya kilimo chetu hivi sasa imepata matatizo kutokana na ukame unaoendelea. Hata hivyo, katika mwaka wa 2002 kilimo kilikua kwa asilimia 5.

Aidha, kuna ongezeko la uzalishaji wa mazao makuu ya biashara na lile la mazao mapya ya biashara hasa maua. Mheshimiwa Rais ametukumbusha kuwa ubinafsishaji na uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya biashara umeonyesha mafanikio makubwa.

Aidha, kwa kuelewa umuhimu wa kilimo kwa ustawi wa maendeleo ya Taifa letu hatua za uboreshaji katika maeneo ya umwagiliaji maji, huduma za utafiti na uwekezaji wa wakulima wa kati na wakubwa zinaendelea kuchukuliwa.

Kwa upande wa mifugo, Serikali imechukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuwawezesha Watanzania kuingia kwenye ufugaji wa kisasa na wa kibiashara. Kwa kutumia maeneo ya ranchi za Taifa wananchi wenye nia na uwezo wa kufuga kibiashara watamilikishwa ranchi ndogo ndogo kwa madhumuni hayo. Lengo la Serikali ni kujenga sekta ya mifugo iliyo bora na iliyo na tija.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miundombinu kama Waheshimiwa Wabunge wanavyoelewa Serikali imefanya kazi kubwa katika sekta ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko. Mheshimiwa Rais ameelezea umuhimu wa kufanya kazi hizi za gharama kubwa, lakini ni muhimu kwa kutumia fedha zetu wenyewe na kwa kutumia mikopo na misaada kutoka nje ya nchi. Aidha, ameeleza mabadiliko makubwa kwa upande wa simu na kwenye mifumo na matumizi ya *Internet.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara ya nje, ameeleza kuwa sekta hiyo bado haijakua kwa viwango vikubwa vinavyostahili. Ongezeko linaloonekana limechangiwa kwa sehemu na mauzo ya madini hususan dhahabu. Changamoto iliyoko mbele yetu Watanzania ni kuuza nje na kuongeza kasi katika kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa kwa soko la nje. Watanzania tutumie kikamilifu fursa zinazotolewa kama zile za utaratibu wa *AGOA* na *EBA* na tusafirishe bidhaa zingine kama mboga mboga, maua, matunda na viungo vya vyakula ili kuongeza mauzo yetu nje ya nchi. Pamoja na kutoa changamoto hiyo kwetu.

Mheshimiwa Rais alielezea mwenendo wa majadiliano na mazungumzo kuhusu mfumo wa biashara duniani na dhamira ya Tanzania kuona kuwa mfumo huo unakuwa wa haki na unatoa fursa kwa nchi maskini kusaidiwa ili kutumia biashara kujiendeleza badala ya kuzidi kutegemea misaada ya wahisani hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utandawazi kama tunavyoelewa Mheshimiwa Rais ni Mwenyekiti Mwenza wa Tume ya Kimataifa Kuhusu Masuala ya Kijamii katika Utandawazi. Kama alivyoeleza ripoti ya Tume hiyo itazinduliwa tarehe 23 na 24 mwaka huu huko Geneva na Mjini London. Ni wajibu wa Watanzania kutumia ripoti hiyo ili tutumie utandawazi kwa faida yetu na siyo kulalamikia utandawazi. Tujue hatma ya nchi yetu ipo mikononi mwetu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusu mambo ya nje. Suala la amani katika nchi za majirani limezungumzwa kwa uzito unaostahili na Mheshimiwa Rais katika hotuba yake. Nchi yetu imefanya juhudi mbalimbali za kuleta suluhu kwenye migogoro katika eneo lote la Maziwa Makuu na imebeba majukumu mengi katika harakati hizo. Hivyo ni muhimu nchi yetu iendelee kushiriki kikamilifu katika jitihada hizo ili kulifanya eneo lote la Maziwa Makuu kuwa Ukanda wa Amani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ulinzi na Usalama, kwa kuelewa kuwa majukumu ya msingi ya dola yoyote ile ni ulinzi na usalama wa raia wake, Mheshimiwa Rais ameeleza kwa takwimu hatua zilizochukuliwa kuimarisha Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama na kuwajengea mazingira bora ya utendaji kazi. Hivyo, Watanzania tujivunie mafanikio yetu na tusifumbe macho hata pale ambapo yapo mabadiliko ya dhahiri yanayoonekana. Tusifiche kasoro wala mapungufu yetu, lakini tusidharau wala kupuuza mafanikio tuliyoyapata.

Mheshimiwa Spika, mwisho, hotuba ya Mheshimiwa Rais katika Bunge lako Tukufu imetupa muhtasari wa kazi zilizofanywa na Serikali yake katika kipindi cha uongozi wake wa miaka minane sasa. Sote tunakubaliana kuwa hoja alizojenga Mheshimiwa Rais katika hotuba yake zinatokana na dhamira yake ya dhati ya kueleza kwa ukweli na uwazi mafanikio ya Serikali yake, matatizo au mapungufu yaliyojitokeza, matarajio katika kipindi kifupi kijacho cha takriban miezi 20 ya Serikali anayoiongoza na dira ya huko mbele zaidi baada ya uongozi wake.

Jambo moja muhimu linalojitokeza ni kuwa amejenga msingi imara wa uchumi endelevu ambao sisi viongozi na wananchi tunahitajiwa sana kuendelea kutimiza wajibu wetu ili tuzitumie kikamilifu fursa zinazojitokeza kusukuma kwa kasi zaidi ukuaji wa uchumi wetu. Kama mwenyewe Mheshimiwa Rais alivyosema sasa lazima tupae kwani vigezo muhimu vya kufanya hivyo vipo.

Bunge hili ni sehemu ya mafanikio hayo makubwa aliyoyaorodhesha Mheshimiwa Rais. Sisi ni wadau wakuu katika kuweka misingi imara ya uchumi unaokua na endelevu. Wito wangu tunapoanza kuijadili hotuba ya Mheshimiwa Rais ni kuwa tusaidiane kutoa mawazo ambayo yataiwezesha Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa majukumu yake ili tuweze kuimarisha mazingira yatakayotuwezesha kupaa kiuchumi katika sekta zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo linamkera Mheshimiwa Rais na amelizungumzia kwa mifano mbalimbali ni tatizo la baadhi yetu kukosa uzalendo na hivyo kuibeza nchi yetu ndani na nje. Tatizo hili katika ulimwengu wa kisasa wa teknolojia ya mawasiliano na utandawazi ni baya, huenea kwa haraka na madhara yake ni vigumu sana kuyafuta kwa haraka. Wapo wanaoeneza sifa mbaya kwa sera yetu ya uwekezaji japo faida ni dhahiri wanaiona. Wapo wanaobeza mafanikio katika huduma za jamii japo wanazitumia huduma hizo na kadhalika. Kuidhalilisha nchi yako makusudi na kwa jambo la uongo ni sawa na usaliti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi ikipata sifa mbaya uwekezaji utashuka, uchumi nao utashuka na wananchi watashindwa kupata huduma wanazostahili. Haya yakitokea si kwa faida ya yeyote awe mwanasiasa wa Chama Tawala au wa Chama cha Upinzani. Baya zaidi madhara yake yanamuelemea zaidi raia wa kawaida ambaye hana hatia.

Mheshimiwa Rais amewaasa Watanzania sasa tuwe wazalendo na tupende nchi yetu. Kuwe na mambo ya Kitaifa ambapo maslahi ya Watanzania yatakuwa mbele kuliko maslahi yetu binafsi au ya Vyama vyetu vya Siasa. Tukumbuke mwisho wa yote Tanzania ni yetu wote sisi tulioko leo na watakaokuja baada yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Rais kuwa bado anayo miezi 20 tu ya uongozi wa nchi yetu. Bunge hili nalo bado lina miezi 18 tu kabla ya kuhitimisha shughuli zake rasmi. Kwa hiyo, kama tulivyoweza kuisaidia Serikali katika kipindi cha zaidi ya miaka mitatu iliyopita, tufanye vivyo hivyo katika kipindi kifupi kijacho ili tuache historia iliyotukuka kwa vizazi vijavyo ya kazi nzuri ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na lijadili hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 12 Februari, 2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nieleze kwamba tulifanya kikao cha dharura cha Kamati ya Uongozi na tukakubaliana kwamba kwa uzito wake hoja hii isipewe chini ya siku mbili kamili za kujadiliwa.

Kwa ajili hiyo, tutaendelea kuijadili mpaka siku ya Alhamisi. Lakini maombi niliyokwishakupata mpaka sasa ni 29 bado orodha haijafungwa kwa sababu hawa watamalizika kabla ya Alhamisi. Kwa hiyo, mwenye nia ya kuchangia bado anayo nafasi ya kujiandikisha jina lake. Kwa kuwa tumefanya kazi kubwa asubuhi hii ya kupitisha Bajeti ya ziada.

Nafikiri sasa Waheshimiwa Wabunge, wanayo haki ya kupumzika na kujiandaa kwa mjadala mkubwa zaidi. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 Jioni. *(Makofi)*

*(Saa 6.30 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais mchana huu kama mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa mchango wangu naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika.

Vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba kwa kuchaguliwa kuwakilisha Tanzania katika *SADC Parliamentary Forum.* Mwisho, napenda kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kujiunga katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Rais. Hotuba ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni hotuba nzuri sana yenye uchambuzi wa kina na imesheheena takwimu na vielelezo vya uhakika.

Kwa kweli hotuba ya Mheshimiwa Rais inaelimisha, inataarifu na inahamasisha na kuchochea maendeleo. Kwa hakika ni vizuri tukajivuna kwamba mengi yamefanyika na yamefanikiwa kwa kipindi cha muda mfupi sana. Ukiangalia katika kila sekta utaona kwamba mafanikio ni makubwa sana. Kwa mfano, elimu imeboreka kwa kiasi kikubwa. Sekta yetu ya afya imefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana ukilinganisha na nchi zote za Afrika ya Mashariki na ya Kati. Mtandao wa barabara pia umeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais nitajitahidi kujielekeza katika maeneo Makuu manne ambayo Mheshimiwa Rais ameelekeza maeneo matano, lakini mimi nitazungumzia maeneo manne ambayo Mheshimiwa Rais ameeleza kama ni sura kuu za mwelekeo katika kipindi cha miezi 20 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ambalo Mheshimiwa Rais amelizungumzia ni umuhimu wa Serikali kuwasaidia na kuwawezesha wananchi kujiendeleza. Ili wananchi waweze kutumia fursa zinazotokana na mafanikio ya sera zetu na hususan mageuzi ya kiuchumi ni budi Watumishi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa kutambua kuwa kazi wanayoifanya ni kazi ya biashara, wanafanya kazi ya biashara ya kutoa huduma. Hivyo utendaji na uendelezaji wa shughuli zao uendane kama ule unaofanywa na watu katika *corporate governance.* Ni budi basi kujenga tabia ya nidhamu, uaminifu, umakini na uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwawezesha wananchi kujiendeleza naomba kwa furaha kubwa kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutambua umuhimu wa uwakilishi wa wanawake katika vyombo vya kutoa maamuzi. Ongezeko la asilimia isiyopungua 30 ya wanawake kuingia katika Bunge ifikapo mwaka 2005 linaipandisha Tanzania daraja na sitashangaa kama Tanzania itaongoza Afrika yote kuwa na wawakilishi wengi wanawake katika Bunge. *(Makofi)*

Vile vile ili kuwawezesha wananchi kuchukua au kujua fursa zilizopo kutokana na mafanikio ya sera zetu za CCM ni budi kuwepo na mfumo mzuri wa utoaji au upashanaji wa habari. Hivyo ni budi kuimarisha na kuipa kipaumbele kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Serikali sasa itoe mfano katika utumiaji wa *ICTs* yaani ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika utoaji wa huduma zake.

Vile vile ni kuviwezesha vikundi vya kijamii kuanzisha vituo vya Habari vya Mawasiliano yaani *Community Tele Centres.* Vituo hivi vinaweza kusaidia sana kwa kutoa habari. Maeneo mengi sasa hivi baadhi ya maeneo vijijini bado hawajui kodi zile za kero ambazo zilifutwa na wengine bado wanaendelea kukatwa. Kwa hiyo, kukiwa na mfumo mzuri wa habari mambo haya yatarekebishwa.

Vile vile ni budi kuongeza usambazaji na upatikanaji wa redio zinazokidhi hali halisi ya vijijini. Nazungumzia mfano wa redio ambazo hazitumii umeme wala hazina betri, redio ambazo zinatumika kwa kuweka ufunguo. Vile vile ni kuhamasisha uanzishaji wa vituo vya redio za kijamii na wananchi waweze kutayarisha vipindi vyao vya redio huko huko vijijini. Kwa kushirikiana na makampuni binafsi na vyama vya kijamii naomba Serikali isaidie ongezeko na upatikanaji wa kompyuta ili kutumia mtandao uliopo wananchi waweze kutandaa kupata masoko na hata kufanya biashara kwa kupitia tovuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu wa jimbo moja la India nadhani ni Andra Pradesh, nilimkariri akisema kwamba India wao hawachagui kati ya *pentium* au *penicillin.* Wao wanatoa kipaumbele kwa vitu vyote viwili yaani masuala ya afya na *ICT.* Kwa hiyo na sisi tusiangalie tu suala la *penicillin* tukasema *pentium* sio ya kwetu. Naomba basi kwamba tuweze kuiweka sekta ya mawasiliano na uchukuzi katika maeneo yale matano ambayo nchi yetu imetoa kipaumbele yaani tuongeze sekta hii katika zile sekta za afya, elimu, maji, barabara na Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo Mheshimiwa Rais alilizungumzia ni umuhimu wa kujenga na kufikiria upya haki ya wanyonge wakiwemo wananchi walio katika sekta isiyo rasmi. Nakubaliana na hili kabisa na napongeza jitihada za Serikali na Serikali za Mitaa katika kuwatengea maeneo ya biashara wananchi wanaofanya kazi katika sekta hii ya biashara isiyo rasmi. Kwa mfano, Jiji la Dar es Salaam, ningependa Halmashauri zingine ziige mfano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa basi wanawake na vijana ndio wenye asilimia kubwa katika sekta hii isiyo rasmi basi ipo haja ya kuboresha na kufufua utaratibu wa utoaji wa mikopo. Vile vile kupitia viwanda vilivyoanzishwa kwa utaratibu wa *EPZ.* Mfano *NIDA Textile, Sunflag* ya Arusha vianzishe *outlet stores* au *factory shops* ambazo maduka haya yawe yanauza bidhaa ambazo hazikidhi hadhi ya soko la nje *(rejects goods). Rejects goods* hizi zitafanya wamachinga waweze kupata bidhaa bora zaidi kuuza huko mitaani yaani bidhaa ambazo zimezalishwa humu humu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kutoa kipaumbele kwa mazao nje ya nchi. Je, jinsi gani tunaweza kuongeza mazao ya bidhaa nje ya nchi. Katika kuboresha mazao nje ya nchi ni vizuri tukazingatia yafuatayo:-

Kwanza ni kuwepo na kuimarisha mfumo mzuri wa miundombinu inayohitajika katika biashara ya kuuza nje bidhaa na huduma. Miundombinu ninayoizungumzia ni ile inayosaidia katika kutoa taarifa ya masoko. Tayari tuna *Tanzania Investment Centre.* Kituo hiki yaani *one stop centre* vilitakiwa vianzishwe vituo kama hivi karibu kila Mkoa au ofisi za Kanda. Kwa hiyo, jambo hili halijafanywa na ni vizuri basi hawa *Tanzania Investment Centre* wakaweza kuwepo katika maeneo mengine ili kurahisisha wananchi wanaotengeneza bidhaa zao wakapata taarifa za masoko na wakauza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuimarishwa kwa Reli. Mtandao au mfumo wa miundombinu ya Reli, Bandari na Viwanja vya ndege. Naipongeza Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi katika kuzingatia hili katika Bajeti wanayoitayarisha. Suala lingine la umuhimu ni ukuaji wa mfumo mzuri wa mawasiliano. Sasa hivi kuna mtandao mzuri wa simu na ni vizuri basi kupitia vyombo hivi vya udhibiti vikaweza kusimamia vizuri ili kukawa na huduma bora na kwa bei nafuu.

Suala lingine ni mtandao mzima wa barabara za Mikoa *(Inland Roads).* Hili litasaidia sana mfumo mzima wa uchukuzi na hivyo kumpunguzia gharama ya usafiri yule ambaye anataka kusafirisha bidhaa zake nje ya nchi. Upatikanaji wa umeme wa uhakika ni jambo lingine muhimu linalotakiwa kuzingatiwa katika kuinua na kuongeza mauzo yetu ya nje. Lingine ni kuharakisha na kurahisisha yaani ku-*accelerate* na ku-*simplify* ulipaji wa ushuru na vile vile taratibu nyingine za kiutawala. Hii itasaidia sana kwa wale wanaotaka kusafirisha bidhaa zao nje. Mwisho ni viwango vya kitaalamu yaani kuzingatia ubora *(quality)* masuala ya afya, pamoja na yale ya kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kutayarisha sera ya biashara. Sera hii imejitahidi sana ku-*create* au kuonyesha zile *linkages* kati ya sekta kuu za biashara kama kilimo, uzalishaji na huduma pamoja na sekta kama ile ya viwanda pamoja na zile taasisi zinazohusika na masuala ya ushindani.

Mwisho katika kipaumbele hiki ni kujiimarisha zaidi katika sekta ya huduma yaani utalii. Katika sekta ya huduma utalii Tanzania ina nafasi kubwa sana ya kuongeza Pato lake kuweza kufidia mazao ambayo tunauza nje zaidi, mazao ya kawaida kama vile dhahabu na mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nchi yetu inatakiwa sasa kuangalia masuala au mazao ya sanaa na utamaduni. Kwa mfano, baadhi ya miziki ya vijana wetu *Bongo Flavour* ni miziki ambayo inakubalika sana nje ya nchi. Wasanii kama akina Saida Karoli, *TID* na wengine wengi akina *Lady Jay Dee, Unique Sisters* wale wanakubalika nje na wanaweza wakauza *CDs* zao, *DVD* na hata *cassettes* na hii inatakiwa sasa Serikali iweze kuwa-*promote* hawa watu ikawasaidia katika mafunzo na vile vile katika kusimamia masuala ya hati miliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda, nitaongelea suala moja lingine la mwisho nalo ni kujenga na kuimarisha uwezo wa Kitaifa wa udhibiti, uratibu na usimamizi wa uchumi wa soko.

Kwanza naipongeza *TRA* kwa kurekebisha utaratibu wa kodi ya mafuta yaani *fuel levy.* Utaratibu huu mpya waliouanzisha utaondoa ukopaji na ujanja ujanja uliokuwa ukifanyika. Lingine ni utoaji wa elimu kwa jamii. Ni muhimu sana sasa hivi tukawa na elimu kuhusu ubinafsishaji, umuhimu wa soko la hisa na hisa katika makampuni.

Pendekezo langu ni kuwa elimu hii itolewe kwa wananchi wote na hususan kwa baadhi ya Waandishi wa Habari ambao ni wazuri tulionao hapa pamoja na viongozi wa vyama vya wafanyakazi. Najua aina ya kozi ambayo inatolewa kuhusiana na maeneo hayo ya ubinafsishaji na masoko ya hisa ni kozi ambayo inafanywa huko *Washington DC* na hii kozi iko kuanzia mwezi wa Juni.

Hivyo basi, mimi naomba kupitia kwako nimwombe Waziri mwenye dhamana hii ya ubinafsishaji kwa kushirikiana na wenye vyombo hivi na viongozi wa wafanyakazi, waone umuhimu wa upatikanaji wa elimu hii kwa faida ya umma na Watanzania wote.

Kama alivyosema Mheshimiwa Rais namnukuu: "Sifa ya nchi si ya mtu au sifa ya chama au sifa ya Serikali ni sifa ya nchi." Kwa hiyo basi, ni vizuri taarifa zinazotolewa zikatolewa taarifa za uhakika na kutokana na uelewa ambao utapatikana. Kama mtu atapata kozi hii na kupotosha taarifa basi itakuwa ni kwa hasara yake na sio kwa kupotosha wananchi walio wengi wakizingatia kwamba sifa ya nchi ni sifa ya nchi na sio sifa ya mtu, ya chama au ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais namwombea afya njema na maisha marefu. *Inshallah.* Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika kujadili hotuba ya Rais.

Kwa kuwa hii ndiyo mara yangu ya kwanza kuzungumza katika kipindi hiki, napenda niwapongeze wenzetu tuliowachagua kuingia kwenye vikao vya *SADC* na katika Bunge la Afrika. Vile vile kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kurudi tena hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Rais wetu kwa hotuba yake ambayo imekuja wakati muafaka kabisa. Ni hotuba yenye kina ya kuvutia na kutia moyo lakini papo hapo inatoa changamoto kwetu sisi ambao tumepewa dhamana ya kuwatumikia wananchi hasa kwa kushiriki katika kuendeleza mafanikio yaliyokwishapatikana kutokana na mageuzi ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu bado ni maskini. Tumejulishwa kwenye hotuba kuna umaskini wa kauli yaani kukosa kauli na umaskini wa kipato ambao ndio tumezoea kuuzungumzia mara nyingi. Pia tumekumbushwa kwamba katika vita dhidi ya umaskini lazima tuelekeze nguvu zetu kwenye maeneo muhimu ambayo ni elimu, afya, maji, barabara vijijini, kilimo na Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo hayo yote tutaona kwamba suala la msingi kama tunataka tufanikiwe ni kuwashirikisha wananchi kwa ukamilifu. Tumeona mafanikio tuliyoyapata kwenye MMEM yameonyesha dhahiri mafanikio ya kuwashirikisha wananchi. Kwa hiyo, tunachotakiwa katika nyanja zote za kuinua uchumi ni kuwashirikisha wananchi katika kupanga, kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo na lazima wananchi washikishwe kwa ukamilifu.

Vijijini kikwazo kimoja tunachokiona ni mawazo tegemezi kwamba mambo yote lazima yatekelezwe na Serikali. Maendeleo yategemee Serikali na hayo ndiyo maswali tunayoyapata majimboni kwetu vijijini. Serikali itatufanyia nini, Mbunge tuambie Serikali itafanya nini kutupatia maji, elimu, afya. Kwa hiyo changamoto moja tuliyonayo ni kuwahamasisha wananchi watokane na mawazo haya tegemezi. Vile vile viongozi tuwahamasishe waelewe kwamba wao wenyewe ndio wana jukumu kubwa la kujiletea maendeleo.

Kama ilivyo katika mambo yote ambayo mtu unapanga kuyafanya, mkakati mkubwa ni kuweka malengo na hii inatukumbusha msemo unaosema kwamba: "Mwendo hauwi mwendo hadi uwe na lengo na lengo ili liwe lengo halina budi kuwa na ukingo au ukomo." Katika vita dhidi ya umaskini lengo ni kujitoa katika lindi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la Ukimwi. Wote tunakubali kwamba tumo katika janga la Ukimwi Kitaifa. Vita dhidi ya Ukimwi ni ngumu kwa sababu tunapambana na maumbile ya binadamu, utashi wa binadamu, tabia, mila, desturi na tamaa ya kujamiiana. Kwa maumbile ya binadamu kama wanyama wengine kujamiiana ni jambo la kawaida kwa madhumuni stahiki yaliyokusudiwa na Mola wetu. Tatizo ni pale tendo hilo la kujamiiana linapochukuliwa kama ni starehe na kwa njia ya ngono zembe.

Katika hotuba ya Rais amesisitiza na kuweka kama ni kanuni kwamba kwanza wale ambao hawajaambukizwa wabakie bila kuambukizwa na wale walioambukizwa wasiambukize wenzao na vile vile

wajitunze waweze kuishi kwa muda mrefu yaani waishi kwa matumaini. Lakini jambo la kwanza ni kujiuliza utamtambuaje mtu ambaye ameambukizwa na asiyeambukizwa. Huwezi kumgundua mtu aliyeambukizwa kwa kumtazama tu.

Kwa hiyo, hatua ambayo inastahili ichukuliwe ni kupima damu. Bahati mbaya katika hali tuliyonayo hivi sasa sehemu za kupimia damu kwa ajili ya Virusi vya Ukimwi ni chache. Kwa hiyo, kwa kweli inakuwa vigumu kugundua wale walio na Virusi vya Ukimwi katika jamii yetu. Ingefaa Serikali kwa kusaidiana na wahisani waongeze maeneo ambayo watu wanaweza kupimwa virusi vya Ukimwi.

Mimi napendekeza vituo vyote vya afya na hospitali zote viwe na nyenzo na wataalamu wa kuweza kupima virusi vya Ukimwi ndipo hapo tunaweza kujua mwelekeo halisi wa Ukimwi hapa nchini kwetu.

Tunasema kwamba maambukizo yanaongezeka lakini kwa kutumia takwimu gani ikiwa wengi hatuwezi kuwapima na kujua kama wameambukizwa au la. Vile vile bahati mbaya bado tunasema kwamba watu wapimwe kwa hiari, bado nasema watu waendelee kupimwa kwa hiari lakini tuwahamasishe na tuwafikishe mahali waone kwamba kupimwa damu ni jambo la kawaida tu na kwa hiyo, wajue hali ya afya zao. Mimi sioni ugumu wowote wa kuweza kupimwa na ukagundulika kwamba una Ukimwi kwa kuelewa kwamba Ukimwi maana yake ni upungufu wa kinga ya mwili kwa magonjwa mbalimbali. Nani asiyetaka kujua hali yake ajione kama ana upungufu wa kinga ya mwili au hapana. Lakini bahati mbaya ugonjwa huu tumeupa sifa mbaya, tunawahusisha walioathirika na tabia mbaya ya uzinzi, tunatisha watu kwamba ukishaupata utakufa tu kama vile watu hatutakufa. Yako magonjwa mengi ambayo yanaua watu lakini hatuyapi uzito huo wa kuwatisha watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tujitahidi tufikishane mahali kwamba wote tuone kwamba ugonjwa wa Ukimwi ni ugonjwa kama magonjwa mengine. Ni ugonjwa wa kuambukiza na unazuilika. Juhudi ziwe kuwaelimisha wananchi waelewe namna ya kuepukana na maambukizi. Liko suala la unyanyapaa. Vile vile mimi sioni kuna msingi gani wa kumnyanyapaa mtu mwenye upungufu wa kinga ya mwili. Inaonekana tu kwamba huyu afya yake sasa sio kamili anastahili kusaidiwa anastahili kuelekezwa na kwa kweli tumeona kama mtu anajilinda anakula chakula bora hanyanyaswi anaweza kuishi kwa matumaini. Tufikishane hapo ili tuweze kupambana na ugonjwa huu kwa mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizunguzie suala la ushirika. Tumepitisha hapa Sheria ya Ushirika ambayo inauweka ushirika katika msimamo mzuri wa kuwezeshwa kufufua tena ushirika. Kama ilivyosemwa kwenye hotuba ya Rais ushirika ndio ukombozi wa wanyonge, umoja wa wanyonge vijijini. Maendeleo yao ya uchumi yanapatikana kwa kupitia ushirika. Kuhusu mitaji wanaweza kuipata mitaji kwa kuingia kwenye vyama vya kuweka akiba na kukopa. Bahati nzuri mimi katika jimbo langu tunacho chama kimoja cha akiba na mikopo na tunafikiria tuanzishe na vyama vingine kwa kuwa tunaamini kwamba hiyo ndiyo njia ya hakika ya kuwaendeleza wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kubeza mafanikio yaliyopatikana. Kwa kweli jambo la busara ambalo tunatakiwa tulifanye, kama umepata mafanikio kwa jambo lolote unachotakiwa ni kuongeza juhudi upate mafanikio zaidi na hili ndilo tunalotakiwa tulifanye, tuwahamasishe wananchi wazidi kuongeza nguvu zao kuwawezesha watokane na umaskini.

Waheshimiwa Wabunge kwa kufanya hivyo tutakuwa tunapata mafanikio katika dhamana tuliyopewa na kazi tuliyopewa ya kuona kwamba katika maeneo yetu hali ya uchumi inakuwa bora zaidi, hali ya maisha ya wananchi inakuwa bora zaidi na tutakuwa na cha kueleza hapo itakapofika wakati wa kuulizwa je, umetufanyia nini katika Jimbo letu na wewe unaweza kusema kwamba kwa kushirikiana na wananchi mafanikio yaliyopatikana ni kadhaa, kadhaa. Hiyo ndiyo changamoto iliyo mbele yetu.

Sina haja ya kusema maneno mengi zaidi kwa kuwa yaliyo kwenye hotuba ni mengi mazito yenye maelekezo, tunachotakiwa ni kuisoma hotuba hii kila wakati na tuzidi kuielewa zaidi na kupeleka uelewa wetu kwa wananchi wetu na kwenye majimbo yetu. Naunga mkono hoja ya hituba ya Rais kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchana huu.

Kwanza nachukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa kuingia katika Bunge la Afrika, Mbunge aliyechaguliwa kutuwakilisha katika *SADC Parliamentary Forum* na nampongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Mheshimiwa Rais. Nadhani sasa Mheshimiwa Rais amefunga orodha yake ya Wabunge kumi. Kwa hiyo, waliokuwa wanazengea basi orodha imekwisha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitangulie kusema naunga mkono hotuba hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nianze kwa kujiuliza kwamba tunapongeza kila wakati hotuba anazotoa Mheshimiwa Rais wetu na kwa kweli ni nzuri, ni maelekezo yanayofaa kuwa dira kwa ajili ya utendaji wa kazi katika Taifa letu. Hotuba zake zina kila sifa inayohitajika. *(Makofi)*

Mimi nina wasiwasi kama kweli tunamsaidia Rais kutekeleza hayo anayotuagiza tutekeleze katika hotuba zake. Hotuba hii nina hakika tukitathmini utekelezaji wake baada ya mwaka mmoja, tutakuta iko vile vile.

Naomba nitoa mfano wa maagizo ambayo amewahi kutoa Mheshimiwa Rais katika hotuba zake ambayo kwangu mimi katika eneo ninalotoka hazijashughulikiwa. Kwa mfano, alipozungumza na Viongozi, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi Watendaji tarehe 16 Agosti, 2002 hapa Dodoma, alitoa tathmini ya utekelezaji wa utawala bora na utekelezaji wa uboreshaji wa utendaji katika Halmashauri 38 zilizoteuliwa kama mfano. Nikitoa mfano kwa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, nadhani ndiyo kati ya Halmashauri iliyoshika mkia katika utekelezaji wa mambo fulani katika uboreshaji wa Halmashauri. *(Makofi)*

Kwa mfano Mheshimiwa Rais alisema: “Ipo tofauti kubwa sana ya hali ya utawala bora kwa vigezo hivi katika Halmashauri 38. Kigezo kimojawapo kwa kigezo cha ushirikishwaji wa jamii, Halmashauri inayoongoza ni ya Singida, Halmashauri ya mwisho ni ya Simanjiro kwa asilimia 1. Kwa kigezo cha utawala wa sheria Halmashauri inayoongoza ni Kasulu ya mwisho ni ya Simanjiro. Katika kigezo cha kuzingatia jinsia Halmashauri ya kwanza ni Manispaa ya Tabora na ya mwisho ni Simanjiro.”

Mheshimiwa Naibu Spika, toka siku hiyo, mimi nilitafakari hizo hotuba za Mheshimiwa Rais kwa sababu kuna watendaji waliokabidhiwa utekelezaji na uongozi bora katika Wilaya na Halmashauri zinazohusika. Mimi naomba niulize Serikali waliotathminiwa na Rais na kuonekana wako dhaifu kiasi hicho imechukuliwa hatua gani? Sasa kama haichukuliwi hatua kwa hao ambao Rais amebainisha, je, wale ambao Mbunge atalalamika huyu, hatekelezi wajibu wake vizuri si ndiyo kabisa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hotuba hii ya Rais na hotuba zake anazozitoa ni za maelekezo ambayo tungeyatekeleza tungeondoa Taifa letu katika hali ya unyonge iliyoko sasa, lakini hatumsaidii sana katika utekelezaji. *(Makofi)*

Mfano mwingine Mheshimiwa Rais, siku nyingi ametoa agizo kwamba kutokana na hali hii ya ukame hakuna Mtanzania atakayekufa kwa ajili ya njaa. Kuna Wabunge wamesema maeneo yao kuna watu wamekufa kwa njaa. Simanjiro hakuna aliyekufa kwa njaa, lakini kutokana na utendaji na utawala wa usambazaji wa chakula kuna watu wengi walioumia kwa njaa. Naipongeza Serikali ngazi za juu kwa sababu kuna wakati walituletea tani 500 kile chakula cha bei nafuu, pia tumepata chakula cha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimweleze Waziri Mkuu kwamba chakula hicho ambacho Serikali imetoa iuzwe kilo kwa shilingi 50, gunia shilingi 5,000 kuna mahali wananchi wameuziwa gunia kwa shilingi 18,000 kwa nini? Huyu anayehusika kusambaza anamweka ofisa, anamwambia bora watu wasipate chakula, lakini uwe na fedha. Hawatoi taarifa chakula kitafikishwa lini kijiji fulani na akifika

anasema anataka sasa hivi fedha na sishushi chakula bila kupata fedha zote. Ikabidi wananchi wawaambie wafanyabiashara nunueni kuliko chakula kurudi. Hawa wakaja kuuza kwa shilingi 18,000 sijui kama yeye ana uwezo wa kubadilisha maelekezo ya Serikali? Hapana ni utendaji mbovu. Hicho chakula kimegawanywa kwa muda wa miezi sita.

Mheshimiwa William Lukuvi naye ni shahidi siku moja nilikwenda kumuuliza kwa nini hatujapata chakula? Nilimwuliza tarehe 22 Januari, 2004 akanipa taarifa tarehe 23 Januari, 2004 kwamba mpaka jana Simanjaro mna akiba ya tani 233. Lakini niliwauliza huko Wilayani Mkurugenzi aliyehusika kugawa hakujua hata bado tuna tani ngapi ambazo zinahitajika kugawanywa kwa wananchi. Sasa hiyo ndiyo kumsaidia Rais katika utekelezaji wa maagizo yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo basi, siwezi kueleza uhaba wa chakula nchi nzima kwa sababu Wabunge wengi walichangia hilo, lakini nasema chakula kwa Wilaya ya Simanjiro, kuna hali mbaya sana. Wananchi wengi wana uwezo wa kununua chakula kwa bei hiyo iliyowekwa na Serikali na Serikali ingepeleka hicho cha kuuza hata gunia shilingi 15,000 hata kama ni 20,000 wananchi wengi bado wangeweza kununua na wangeshiriki kula na wale ambao hawana kabisa, hiyo ndiyo jadi yao. Ndiyo maana huwakuti ombaomba, wanasaidiana. *(Makofi)*

Sasa watendaji wanaibebesha Serikali mzigo, watendaji wataifanya Serikali ionyeshwe kidole na wananchi kwamba haitujali. Lakini mbaya zaidi tumesikia kuna haya mahindi ya kuuza, wananchi wamekwenda kutafuta vibali vya kununua na baadhi ya Serikali za Vijiji inakusanya fedha wanakwenda kuomba kibali ili wanunue haya mahindi, hawakupata hivyo vibali, kwanza si maajabu!

Nashukuru kwa sababu kati ya Madiwani walioshughulikiwa mmoja yupo pale ilibidi aje huku kuuliza wapi apate kibali cha kununua chakula hiki cha Serikali wananchi wakanunue siyo wakapewe bure. Sasa hiyo ndiyo kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais? Hao tunawafahamu na Serikali Kuu imewapa fedha za kusambaza hicho chakula, mara ya kwanza tulipewa shilingi milioni kumi na mbili nashukuru Serikali ya Rais Benjamin Mkapa. Nimeambiwa jana au leo zitakwenda shilingi milioni 11, kusambaza tani 230 tulizopata tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie tunapotekeleza majukumu ya wananchi kwa kweli hawa tunaowapa wawakilishe watende kwa ajili yenu wanatimiza wajibu wao inavyotakiwa? Kama hawatekelezi unachukua hatua gani? Au tuseme wengine wana *God Fathers* na *God Mothers? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumze haraka haraka ni suala la umeme. Tuliahidiwa toka mwaka 1996 kwamba Makao Makuu ya Wilaya zote itapata umeme, mpaka leo Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro, hakuna umeme. Leo kwa hotuba hii tuelezwe tunajua umuhimu umeme, tuelezwe ni lini tutapata?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili la umeme Nyumba la Mungu kuna mahali panapoanzia umeme na upande wa pili wa Bwawa ya Nyumba ya Mungu vijiji vyote vina umeme, lakini upande wa pili wa Wilaya ya Simanjiro hakuna hata kijiji kimoja chenye umeme. Kijiji chenyewe cha Nyumba ya Mungu hakuna umeme, Ngorika hakuna umeme, Magadini hakuna umeme, Kiruani hakuna umeme, Msitu wa Tembo hakuna umeme. Kutoka *TPC* mpaka Msitu wa Tembo ni kilometa 7 kuna *transformer* mnaweza kuvuta umeme pale. Sasa hawa wananchi waeleweje? Watanzania wale wale, nyumba hizo hizo za aina hiyo hiyo,wa ng’ambo ya pili hawana umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais pia alipotembelea Wilaya ya Simanjaro, alitupa ahadi tatu, aliahidi kwamba Kituo cha Polisi kitajengwa Simanjiro na Serikali. Wananchi wamejenga mpaka kupaua, jamani malizieni hiyo kabla ya Rais kumaliza muda isiwe ni kiporo! Aliahidi kwamba itajengwa Sekondari ya Bweni katika Wilaya zote za wafugaji, madhali tumepata fedha za MMES jengeni kwa miezi 20 iliyobaki ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie lingine la utawala huu kutambua viongozi mpaka ngazi ya vijiji kwamba Maafisa Watendaji wa Vijiji wanalipwa sasa mishahara, lakini tunawaacha watu muhimu Madiwani. Madiwani ndiyo Wabunge katika Kata zao. Yeye ndiyo anamwajiri huyu Afisa Mtendaji wa

Kijiji, lakini yeye hapokei chochote na kuna wengine wenye Kata kubwa kutoka kijiji mpaka Makao Makuu ya Kata kilometa 70 atafikaje? Kila siku auze mbuzi wake kwenda huko? *(Makofi)*

Tulikuwa tunasema wanaweza kukopeshwa na Halmashauri vifaa vya usafiri, lakini sasa tumefuta baadhi ya kodi na wananchi wanafurahia na sisi tunafurahia, kwa hiyo, ni Serikali sasa inahudumia Halmashauri na hawa Madiwani wao wataendelea kusononeka hivyo mpaka lini? Hao ndiyo viongozi wa kwanza kupeperusha bendera ya Chama cha Mapinduzi. Kama ni wa Upinzani ndiyo wa kwanza kupeperusha bendera zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli wao ndiyo hatua ya kwanza ya kuona utumishi wa watu waliochaguliwa. Afisa Mtendaji wa Kijiji hata apokee mshahara ni mdogo, lakini walau nafuu. Lakini Diwani ambaye amemwajiri hapokei chochote. Posho za vikao mmemwambia kadri mtakavyokusanya na vyanzo vingi tumeambiwa hizi hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naishauri Serikali na namwomba Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa Bajeti hii alivyofikiria katika miradi mbalimbali na viongozi mbalimbali, hata juzi viongozi wachache kama Ma-*DC* na Wakuu wa Mikoa tumewafikiria vizuri hapa. Lakini kwa kweli wanaofanya ile *donkeywork* ni Madiwani. Lini na wao watafikiriwa? Naamini ni sasa.

Kwa kweli tutaunda madaraja ya watu watakaoneana wivu bila sababu. Kwa kweli Madiwani hata wakiwaonea wivu wengine wana sababu, wana haki. Hakuna mtumishi wa Serikali ambaye halipwi. Sasa tunalipa mpaka hata vijiji kwenye Kata watalipwa na Serikali, kwenye kijiji atalipwa na Serikali, tarafani atalipwa na Serikali, Wilayani ndiyo kabisa, kwenda juu ndiyo kabisa. Lakini kwa viongozi wanaochaguliwa na wananchi, waliopewa ridhaa na wananchi tunaelekea kuwanyanyasa Madiwani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nieleze hilo. La mwisho kabisa Wilaya ya Simanjiro, tuna uhaba wa maji kuna mradi wa Maji ya Mto Pangani. Imezungumziwa toka mwaka 1980 mpaka leo inazungumziwa, tumeshaona miradi mikubwa sana ya maji na naipongeza Serikali kuleta maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo mradi wa maji Pangani ufikiriwe kuletwa Orkosmet. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushukuru kwa kupata nafasi hii kwa ajili ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 12 Februari, 2004 kama hoja ilivyowasilishwa leo na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kabla ya kufanya hivyo, naomba na mimi pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuwapongeza Wabunge wafuatao kwa matukio yaliyotokea.

Kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuungana nasi hapa kuwa Mbunge. Naomba pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, tuliowachagua kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika. Nawapongeza sana kwanza watakuwa na sifa moja ya ziada ambayo wengine hawatakuwa nayo (watakaokuja) wao ni Wabunge waanzilishi wa Bunge hili la Afrika, hongereni sana. Pia nampongeza Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa na Bunge lako pia kutuwakilisha katika Bunge la *SADC. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kazi hiyo, basi naomba nijielekeze sasa katika kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais. Naomba nimpongeze kwa hotuba yake, kwa kweli ni hotuba makini, ndefu lakini isiyochosha yenye kutaka kusikilizwa kila wakati na hata sasa hivi ikianza kusikilizwa watu watakuwa na hamu ya kuendelea kusikiliza. Hotuba iliyojaa kila kipengele tena kwa uwazi na kwa ufasaha sana. Ni wazi kwamba hotuba hii imetuelimisha walio wengi sisi Wabunge, wananchi wa kawaida, viongozi mbalimbali wa kila sekta. Namshukuru sana kwa hotuba yake hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais mara nyingi amekuwa akitutaka viongozi kwamba jamani eeh, haya yanayotendeka mbona hamyasemi kwa wananchi wakaweza kuelewa? Sasa inawezekana amechoka na kuona kwamba hatumsaidii katika kuwaeleza wananchi wajue yanayotendeka, hatua

zinazopigwa, imefika mahali amefika kwetu kuja kutueleza na kueleza wananchi yeye mwenyewe moja baada ya jingine katika yote ambayo ameyafanya katika uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika yote hayo naomba nijielekeza katika machache ambayo ameyaongea na ambayo nafikiri nikiyaeleza tunaweza tukasaidiana ili kama alivyosema yeye mwenyewe katika miezi iliyobaki tuweze kusaidia kupaa kwa jahazi hili au kwa ndege hii ambayo iko katika mkondo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ambao yeye pia aliuzungumza kwamba nchi yetu, ni nchi bado yenye wakulima wengi kuliko makundi mengine yote. Wakulima ni asilimia zaidi ya 85 ambao bado tunategemea kilimo. Watu hawa katika miaka ya 1970 wakulima watu wengi walikuwa wanapenda kilimo. Walikuwa wanapenda kilimo kwa nini? Kilimo kilikuwa kinapendwa kwa sababu wakulima waliweza kupata pembejeo, mbegu na vitu vingine wanapokuwa wanazitaji kwa uhakika. Wakulima waliweza kupata zana za kilimo kwa uhakika. Wakulima waliweza kupata masoko baada ya kulima kwa uhakika. Vyama vyetu vya Ushirika na wanunuzi mbalimbali wengine.

Kwa hiyo, kilimo kilikuwa kinapendwa na watu wengi hakikuwa kinasumbua. Lakini katika kuhangaika namna ya kwenda mbele tumefika katika kipindi kilimo kikawa na matatizo na wote nafikiri tunajua na tunakumbuka. Tumefika katika mabadiliko haya pia ndiyo tukawa na matatizo zaidi. Zana za kilimo zikawa tatizo, mbegu zikawa na matatizo na masoko yakawa na matatizo. *(Makofi)*

Wakulima wakakopwa mazao yao, wapo wakulima ambao tunasema wakati huo, wakati wa vyama vile vya ushirika bado wengine wanaendelea kudai pesa kutoka kwenye Vyama vya Ushirika ambavyo vingine vimekufa. Ikafika mahali watu wakachukia wakaanza kuchukia kilimo na ndiyo tukaanza kuona, pakaanza kuzuka na wamachinga hatukuwa na Wamachinga, wakaanza kuzuka Wamachinga, watu wakaanza kukimbilia mijini wakifikiria kwamba kule ndiyo kuna maisha mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri katika kusaidia ili tuweze kupaa kwa miezi michache iliyobaki hatuna budi kuangalia wakulima maana ndiyo kundi kubwa, asilimia zaidi ya 85 ni wakulima. Ili uweze kupaa mzigo mzito kama huu lazima ujizatiti na kuhakikisha kwamba unauchukua katika hali inayotosheleza. Wakulima tuwaandalie hali nzuri, tuwaandalie kama ilivyokuwa.

Tumefika mahali wanalima mazao yao kama hali inakuwa nzuri, tuchukue kilimo tu cha kawaida ambacho mkulima mpaka sasa analima, inatokea wakati wa kulima wanapata mazao mengi na wanakuwa na akiba ya kutosha, wanakosa mahali pa kuuza. Leo gunia tunasema ni shilingi 30,000/= na sehemu zingine zaidi. Lakini baada ya miaka miwili hali ya hewa ikiwa nzuri mvua zikija vizuri, gunia hilo hilo ambalo leo tunasema shilingi 30,000/= litanunuliwa kwa shilingi 3,000/= nani atakayerudi kwenda kulima mwaka unaofuata? Mkulima analima bila ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuangalia kundi hili kubwa kulirekebisha katika hali hizi kilimo chake, masoko yake hatutakuwa na uwezo kwa kweli wa kuruka. Mheshimiwa Rais, amelizungumza sana hili na amezungumza na mageuzi ya kilimo pamoja na umwagiliaji. Naomba tutilie mkazo lakini umwagiliaji utakuja taratibu maana tunaangalia sasa hivi hata eka zinazosemwa zile za umwagiliaji ni kidogo, lakini eka nyingi ziko kwa mkulima mdogo. Naomba tumjali mkulima, tumpe pembejeo, tumwahidi soko la uhakika ili mkulima huyu asikate tamaa. Kwa kweli tukifanya hivyo tutawarudisha wengi hawa wamachinga walioko mijini, kwa sababu wamekata tamaa wanaona hata kama nikilima ni biashara moja mbovu sana. Anaona afadhali aende kule akauze shati moja mchana kutwa lakini atajua baadaye namna ya kufanya, akimpania Mheshimiwa mmoja naye atakuwa amepata fedha ya kula kitu ambacho haikuwa lazima wao wafanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mkulima huyo huyo, sisi wakulima wa Singida au wananchi wa Singida hatukuwa na tabia ya kupata njaa kwa mfano kama mvua haikunyesha msimu huu na tusipate chakula msimu huu mwaka ujao tujisikie eti tuna njaa hatukuwa na tabia hiyo, kwa sababu gani hatukuwa na tabia hiyo? Ni kwa sababu tulikuwa tunahakikisha kila kaya inajitosheleza kwa chakula cha zaidi ya miaka mitatu. Kila kaya inaweka akiba inayoweza kutosheleza zaidi ya miaka mitatu endapo njaa itatokea.

Endapo mvua haitanyesha mwaka huu, mwaka ujao watu wana chakula, mwaka unaofuata wana chakula, mwaka wa tatu wana chakula, mwaka wa nne ndiyo watu wataanza kuhangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo sasa. Sasa hivi mvua ikitetereka mwaka huu, mwaka ujao watu njaa pale pale kwa sababu tabia ambayo tulikuwanayo tumeacha kuifanya hivyo na siyo kwa makusudi. Visumbufu vya nafaka vimekuwa ni sugu. Tulikuwa na dawa ambazo zilikuwa mtu ukiweka visumbufu hivi haviendelei. Lakini sasa hivi sijui hizi dawa imekuwa ni vipi?

Kwanza hazipatikani, pili, zikipatikana inakuwa tatizo, unaweka kama hujaweka. Tumeeleza hili mara nyingi na hata wakati mmoja mwaka 2003 au mwaka 2002 Waziri wa Kilimo alitembelea Singida tulimwambia, tukaambiwa kuna dawa aina mbili, moja *fake,* moja ndiyo dawa halali. Lakini zote hizo ukiweka baada ya miezi miwili, miezi mitatu unakuta hakuna kitu. Imewafanya wakulima wetu wauze kila wanachopata kwa sababu akiacha hana faida nacho. Baada ya miezi miwili, mitatu ni unga mtupu hakuna akiba inayowekwa na wakulima hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi niangaliwe katika hayo kama kweli tunataka wakulima wetu wawe na akiba ya chakula ya miaka zaidi ya miwili, zaidi ya mitatu. Hili ndilo linalotupa shida. Leo tunagombana hapa sijapata chakula kwangu, sijapata hiki kwangu kwa sababu ya njaa. Hatua kubwa ambayo tulikuwa tumeipiga katika miaka hii, ambayo yote haya Rais anatueleza leo hii tunarudi nyuma. Tulipiga labda hatua kumi kwenda mbele lakini tunarudi hatua tano tena nyuma kwa sababu ya kitu njaa. Pesa ambazo ilikuwa tuendelee kushughulikia matatizo mengine, tuendelee kujizatiti katika kuhakikisha kwamba tunafanya hili na lile tunarudi kununua chakula cha njaa. Tunagombana sasa hivi kwa ajili ya njaa. Kwa nini hatujifunzi?

Njaa siyo mara ya kwanza, njaa siyo labda mara ya kwanza, tumeanza kupatwa na njaa muda wa miaka mingi. Kwa nini hatujifunzi na kuchukua hatua zinazostahili ili kuepuka hivi? Bilioni zaidi ya 23 nina uhakika zitatumika zaidi ya hapo au 27 na kadhalika, lakini je, bilioni hizi kama tungekuwa tunajielekeza katika hii mianya ambayo nasema inayoweza kutusaidia katika hifadhi ya chakula, inayoweza kutusaidia katika kilimo, inayoweza kutusaidia katika umwagiliaji. Kila mwaka tukatenga fedha hizo, je, tungekuwa wapi sasa hivi, tunakuwa tunahangaika suala la njaa na kunyang'anyana chakula hapa?

Naomba basi tuangalie ndugu zangu kwa kweli tusije tukaendelea kurudi nyuma hatua nyingi ambazo tulikuwa tumezipiga. Ni kama mgonjwa au ni kama mtu ambaye sasa hivi hali yake ni nzuri, lakini ukipatwa na ugonjwa afya inatetereka na kuja kurudisha afya ilivyokuwa inachukua muda, inahitaji dawa, chakula na kadhalika. *(Makofi)*

Mimi yangu yalikuwa ni hayo ni kilimo tu ambacho tutaweza tukikazania hali yetu kwa kweli inaweza kutupeleka mahali pazuri. Juzi nilikuwa na Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, tulikwenda Hombolo kuangalia muhogo pale ili angalau tuweze kupata mbegu, laa! Ilikuwa ni hatari Naibu Waziri alinichukua kwa sababu nilimweleza nililokuwa nalo. Lakini tunafika Hombolo kwa sababu ya njaa ndugu zangu ule muhogo umeharibiwa, hata mbegu pale imeharibiwa. Watu wanaingia usiku wanang'oang'oa na kutupa huko. Sasa hata mbegu tunayosema ya muhogo kwa ajili ya kujisaidia wakati wa njaa haipo hata sasa hivi. Nasikitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo yote kwa kweli naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Tuitekeleze basi ili tuweze kusaidia miezi hii inayobaki tuweze kupaa. Kwa kweli namtakia afya njema aweze kupona maradhi yake haraka ili aweze kututembelea Mkoa wa Singida.

Tangu mwaka 2000 kwa kweli kwa bahati mbaya au bahati nzuri kwa sababu anasongwa na mambo mengi hajatutembelea, ninaomba Mungu amponyeshe haraka ili aweze kututembelea Mkoa wa Singida. Nafikiri wana hamu sana ya kutaka kumwona na kuongea naye ili aweze kuwapa mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, basi naomba kuunga mkono hoja tena na ninashukuru sana kwa kupata nafasi hii kuongea leo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba nzuri kabisa ya Rais wetu aliyoitoa tarehe 12 Februari, 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu na mimi ni mara yangu ya kwanza kusimama humu kwa muda wa miezi kadhaa, kwanza naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, nimerudi Bungeni nikiwa salama salmini, lakini nimejifunza mengi na kwa kweli baada ya kutoka hapa nilienda kuchapa kazi kweli kweli Jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii kwa kweli ni nzuri sana. Nami nimtakie Rais wetu afya njema, Mwenyezi Mungu amjalie ili apone haraka zaidi ili aweze kusimamia yale ambayo ndani ya miezi 20 yaweze kutimilika. Lakini nitakuwa mchoyo wa fadhila au kama sitasema neno moja la kumwomba Mwenyezi Mungu amjalie sana Mheshimiwa Bujiku Sakila, ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni maradhi aliyonayo apone ili twende kwa pamoja tukasimamie Majimbo yetu kwa maana ya Wilaya yetu ya Kwimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu hiki Mheshimiwa Rais ametutaja sisi kama wadau au wabia na ametuomba mara kadhaa katika hotuba yake, naomba nimnukuu kidogo: "Ningependa Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono katika kuweka kipaumbele juu ya mambo haya yaliyomo humu ndani."

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini akaendelea mbele ukurasa ule wa 50 akasema, "Sisi wote hapa ni viongozi" (sisi humu ndani Wabunge) lakini akaendelea zaidi akasema: "Nasema sisi ni viongozi, tuoneshe ujasiri wa kupeleka mbele Taifa si ujasiri wa kuweka Taifa *break."* Hayo ni maneno mazito kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi viongozi kama Bunge ndio tunaambiwa na Mheshimiwa Rais kwamba tusiwe kichocheo cha kuleta maendeleo. Tuondoe ile *break,* tuachie kama ni gari liende bila matatizo. Ndio maana ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo mimi kwa kweli hotuba hii nimeifurahia sana na hii ndio iwe dira yetu sisi kama viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulioingia Bungeni mwaka 1995 na wengine walioingia miaka ya nyuma, haya mafanikio yanayotajwa humu ndani si madogo hata kidogo. Ni mafanikio makubwa kweli kweli! Nchi yetu haikuwa hivi jamani! Ukisoma viambatanisho vilivyoambatanishwa humu, tulipoingia mwaka 1995 kama ni Mbunge wa Jimbo ulikuwa huna hata sehemu ya kuanzia. Kila ukigusa maji ni tatizo, barabara tatizo, Zahanati tatizo, dawa tatizo, majosho tatizo, leo kila kitu kimenyooka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo sasa niruhusu tupongezane kwanza sisi wenyewe Wabunge humu ndani kwa kazi nzuri. Tuwapongeze wananchi kwa kupokea miradi ambayo ilikuwa inapelekwa na Serikali na kwa sababu wao walikuwa ndio wadau wazuri. Kama sio wananchi kuitikia na kupokea haya ambayo tunayazungumza humu na ngumu kuyapeleka kwao, nafikiri ingekuwa ni kazi kweli. Lakini wananchi wa Tanzania wameitikia vizuri lakini kwa maelekezo na utawala bora na siasa safi ya Chama cha Mapinduzi. Naomba tujipongeze sisi wenyewe kwa kazi nzuri tuliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nisiwasahau ndugu zangu Waandishi wa Habari. Yote tunayoyafanya humu wao ndio wanapeleka taarifa kule kwamba jamani kinachofanyika ni hiki na kinachotegemea kufanyika ni hiki. Nawapongeza sana ndugu zangu wataalam hawa, naomba waendelee kwa kuandika, kwa kuelimisha jamii kwa yale mazuri sio mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mengi yamefanywa na Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, mimi nina maombi tu kwa kweli. Mheshimiwa Waziri Mkuu asubuhi kama sikosei, alisema jamani hotuba hii ni nzuri sana. Kuinyambuanyambua haifai! Tunachotakiwa sasa hivi kama alivyosema mwenyewe Rais, kama tulikuwa *gear* namba moja, basi tuweke *gear* namba mbili, tatu na nne ili twende mbele kwa kasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upande wa umwagiliaji, tukitaka kwenda vizuri zaidi Wizara ya Kilimo na Chakula, sisi bahati nzuri tunatoka Kanda ya Ziwa. Tunalo Ziwa Victoria. Katika kipindi cha Bajeti tuliambiwa kwamba kuna pampu zitapelekwa kwa ajili ya umwagiliaji, lakini bado kuna kusuasua.

Naomba sana Serikali hasa Wizara ya Kilimo na Chakula, zile pampu ziende haraka iwezekanavyo ili tatizo hili la njaa lipungue kama sio kwisha. Lazima muainishe maeneo mawili au matatu, msipeleke yote kwa pamoja, mfanye kama mlivyofanya kupeleka mbolea ya majaribio Kusini na ninafikiri imefanikiwa. Kama haijafanikiwa ni bahati mbaya, lakini nia ya Serikali ilikuwa nzuri na bado nia ya Serikali ni nzuri.

Lakini ombi la pili kwa Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Serikali ina mipango mizuri kabisa ya kuweka miundombinu hasa kwenye viwanja vyake vya ndege, nasikia Arusha na sababu inajulikana wala hakuna pingamizi, Mbeya, sababu inaeleweka kabisa hakuna pingamizi, lakini bado Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, *Mwanza Airport,* Kongo kwao ndio pale, Rwanda kwao ndio pale, Burundi wako pale, Kenya wako pale na nchi nyingine.

Nakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri anajibu swali la Mama Janet Kahama alisema kwamba hakuna haja ya kujenga kiwanja kikubwa Kagera kwa sababu tunacho kiwanja cha Mwanza. Sasa rai yangu na ombi langu kiwanja kile ni kidogo hakitoshi. Naomba katika utaratibu wa Serikali ikiwezekana katika mpango wa Bajeti ijayo liwepo fungu la upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukurani kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Kwa kweli nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sitatoa shukrani. Nilikuwa na matatizo na sehemu zangu mbili, Malya na Sumve. Nashukuru sana Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo imepeleka maji katika maeneo hayo, nashukuru sana. Lakini vile vile naomba nishukuru Wizara ya Nishati na Madini. Nilikuwa na tatizo la umeme Sumve, nakumbuka nilishapiga kelele sana hapa.

Naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, sasa wameshaanza na wanapima na nimwombe sana Bwana mdogo Ibrahim Msabaha wasiishie kupima tu, kazi hiyo ikamilike kama ilivyopanga, kwa sababu yapo maeneo mengi ambayo wanaishia kupima tu, lakini kwa kweli hatutakuwa tumewatendea haki wananchi wetu. Tunawapelekea miradi lakini miradi hiyo inaishia njiani. Naomba Serikali yetu sikivu yale ambayo tunayaazimia ni vizuri tukayatekeleza. *(Makofi)*

Lakini nimalizie kwa kunukuu tena hotuba ya Rais ukurasa huo huo wa 50. Unapozungumzia viongozi na bahati nzuri kama sikosei, ukituacha sisi tuliopo nyuma huku, walengwa wakubwa walikuwa ni Mawaziri. Mheshimiwa Rais anasema hivi: “Zipo sifa za kiongozi bora. Upeo mpana, uwezo wa kupima na kuamua na ujasiri wa kutenda na zipo sifa za kiongozi asiye bora, upeo finyu...” Naomba wengine muendelee. Sasa mimi nina uhakika hii ni *challenge* kwamba tunatakiwa tutende, tuwe na maamuzi, tusisubiri mpaka tuamuliwe na mtu mwingine. Tuamue sasa tufanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana lakini nimalizie kwa nukuu ya leo. Nukuu yangu ya leo baada ya kusikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu hasa katika mambo aliyozungumzia Rais, mimi nasema hivi, Rais Benjamin Mkapa ni Rais wa Watanzania wote na sio Rais wa watu wa Mtwara au wa Kusini. Kuna maneno yalisemwa hapa sitaki niyarudie kwa sababu taratibu na Kanuni zetu hazituruhusu kurudiarudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana jioni hii kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii muhimu ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwanza nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wale watano tuliowachagua juzi, Wabunge wa Bunge la Afrika na pia ndugu yangu yule tuliyemchagua kwa ajili ya Bunge la *SADC.* Tunawaomba wakatufanyie kazi nzuri kama tunavyowaamini na tulivyowachagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa juzi, kusema kweli ni hotuba ambayo kila mmoja angeweza kutoa maneno ya namna yake ya kuisifu anavyoweza. Kama mwenzangu mmoja alivyosema hivi ndiyo namna hotuba za Rais Benjamin Mkapa, zinavyokuwa lakini hii ya juzi imezidi kidogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Rais kumaliza kuzungumza, alitoa maneno matatu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa niaba yetu. Maneno yale aliyatoa kwa lugha ya Kiingereza. Alisema: "Hotuba ya Rais ilikuwa *authoritative,* ilikuwa *comprehensive* na ilikuwa *inspiring."* Kwa maneno hayo, mimi sina maneno zaidi ya sifa ya hotuba ya Rais ile kuliko haya aliyotoa Mheshimiwa Spika. Namshukuru sana kwa kuyatoa maneno hayo kwa niaba yetu. *(Makofi)*

Hata hivyo, naomba niseme moja tu kwamba hotuba ya juzi ya Rais Benjamin Mkapa, kusema kweli naomba iwe kigezo na pengine kipimo cha ngazi ya ndugu zangu hasa wale ambao wanatarajia kuomba nafasi ya Urais mwaka kesho wakati Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa anastaafu hasa kutoka Chama cha Mapinduzi, wanaonuia wajipime kwa sifa za utendaji kazi na hotuba nzuri kama hii ili ijulikane kwamba wana-CCM wanaopenda kutuongoza basi ngazi yao iko katika maeneo hayo, kiwe ni kipimo hicho muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena niseme kwamba katika hiyo hotuba ya Mheshimiwa Rais, pamoja na kwamba alielezea mafanikio mengi ya Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tatu, Rais alishangazwa kusema kweli na wale watu au mtu yeyote ambaye bado hajaona hata mwanga wa mafanikio ya kazi kubwa ambayo Serikali ya Awamu hii imefanya. Rais Benjamin Mkapa ameshangazwa sana na hali hiyo ya wale ambao hawaoni na kusema kweli mifano ile aliyoitoa Rais Benjamin Mkapa pale juzi ilikuwa ni mifano ya kusikitishwa na watu wa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wenzangu walivyoifuatilia kwa makini hotuba ile na mimi nilifuatilia kwa makini na wakati nimekaa hapa nilikuwa nawaangalia hata viongozi wa Vyama vya Upinzani waliokuwa pale juu, wakati wote na wao walikuwa wanamshangilia Rais Mkapa kama sisi tulivyokuwa tunamshangilia. *(Makofi)*

Sasa la kusikitisha tu ni kwamba baada ya hotuba ile, basi maneno yakawa mengi kwamba Rais Mkapa aliwatukana watu, Rais Mkapa aliwakejeli, Rais aliwadharau. Sasa kitabu hiki nimekirudia kukisoma mara mbili mimi sikuona matusi ya Rais Mkapa kwa mtu yeyote, sikuyaona kabisa! Nimesoma nikarudia, nikasoma nikarudia na mifano yote ya walevi ile lakini mimi sikuona kwamba mifano ile ilielekezwa kwa Chama cha Upinzani au kwa mtu fulani, mimi sikuona ile. Sasa ninachoamini, kilichofanyika hapa bila shaka ni tafsiri. Sasa kama ni tafsiri ya hotuba hii ya Mheshimiwa Rais, kila mtu akitaka kuitafsiri, basi kila mtu ataandika kurasa zake anazoweza. Lakini kusema kweli kwamba Rais katika hotuba yake ilijaa matusi na nini, mimi sikuyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mifano ile aliyoitoa Rais kwa kweli Rais alikuwa anashangaa, alikuwa anasikitika. Kazi kubwa imefanyika, nani aeleze? Ameshaieleza kwenye kitabu chake. Kodi za kero zimeondolewa, mwaka huu tu, kwenye Bajeti ya mwaka huu, kodi zote zimeondolewa pamoja na kodi ya maendeleo. Ratiba na maendeleo ya MMEM yanafanyika, kuna mipango mingine inayokuja ya kuinua ubora na kiwango cha Elimu ya Sekondari na mipango mingi, barabara Vijijini, Mikoani. Sasa kama si jitihada za kupunguza umasikini wa Watanzania, basi ni nini?

Sasa mimi nasema, hotuba ile na maneno yale ya mifano hayakumlenga kiongozi yeyote wa Chama cha Upinzani wala mwanachama wake wala mwana-CCM, wala nani, lakini kwa yeyote ambaye hakuona mafanikio haya ya Serikali ya Awamu ya Tatu ambayo imefanya, kusema kweli anastahili kupuuzwa hata kama ni mwana-CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya kumlaumu Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ile, mimi naona wenzetu wa Vyama vya Upinzani wangeichukua ile kama changamoto. Rais Benjamin Mkapa amekuwa mkweli kweli kama alivyosema mwenyewe. Yeye ni mkweli na muwazi. Kusema kwamba Vyama vya Upinzani ni dhaifu, nadhani amekuwa mkweli kweli kweli! Mheshimiwa Rais sisi wengine

ndugu zake wa Chama cha Mapinduzi tungesema, huyu mzee vipi huyu? Mwaka kesho anastaafu, sasa anawachochea hawa jamaa wapate nguvu watumalize! Tungeweza tukasema hivyo. Lakini Mheshimiwa Rais amesema, ameona umuhimu wa kuwa na Vyama vya Upinzani, kwamba Vyama vya Upinzani vina maslahi kwa Taifa. Alivyozungumza kwenye hotuba yake na si kwenye Vyama tu, lakini vina maslahi kwa uwezo na maendeleo ya Taifa.

Kwa hiyo, nilidhani wenzetu hawa waichukue hiyo kama changamoto ili waweze kujiweka vizuri wawe na nguvu basi watoe ushindani unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo ambayo pengine hayakusemwa, Rais hakuyasema lakini nina hakika anayo. Kwa hiyo, nina mambo matatu ambayo nitayagusia kabla sijakaa. Moja, ni suala la rushwa. Suala la rushwa wote tunafahamu kwamba Rais Benjamin Mkapa na Serikali yake alianza kuweka msingi mzuri sana wa kupambana na rushwa mapema alipoingia kwenye madaraka yake. Wote tunakumbuka Tume ya Mheshimiwa Jaji Joseph Warioba na misingi yake ambayo imewekwa. Wote tuliona na tunafahamu jinsi ambavyo hatua mbalimbali zilikuwa zinachukuliwa hasa katika kutekeleza mapendekezo yaliyokuwepo kwenye Tume ile ya Jaji Warioba.

Lakini napenda niamini na kuungana na wale waliosema kwamba hatua za kupambana na rushwa bado hazijatosha. Rushwa ni kitu hatari! Rushwa ni jambo ambalo linaweza likaua na kumaliza mafanikio yote yaliyopatikana ya kiuchumi. Rushwa ikiendelea hata Rais Mkapa mwaka kesho akiondoka nchi inapaa kwa uchumi, basi yale mafanikio ya uchumi yanaweza yasiwakute watu walio wengi kama rushwa itashamiri.

Mimi naomba tumshauri Rais Benjamin Mkapa, aongeze vita dhidi ya rushwa ili anapoondoka mwaka kesho Rais ajaye anaanzia pale. Rushwa ni hatari! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa na pengine punde kidogo kampeni zimeanza kule kwenye Majimbo, sijui kwa wenzangu. Yako mambo yanafanyika huko ni ya ajabu kabisa, tena Chama cha Mapinduzi wenyewe wala si mtu mwingine. Yako mambo yanafanyika ni ya ajabu huwezi kabisa kuyaamini! Tena wengine tuna wasiwasi sijui hata kama mwaka kesho nitafikia mwisho au nitakufa njiani. *Is terrible* sijaamini! Kuna rushwa ya ajabu inatoka huko. Rushwa ya madaraka, rushwa ya fedha, rushwa ya kila kitu.

Najua kwamba Chama chetu kipo, kitafanya hiyo kazi, lakini jambo hili ni la hatari, tulichukulie kwa uzito wote wala tusilinyamazie. Tumekuja Dodoma hapa, tumesikia manung'uniko na mambo yaliyofanyika hapa katika Mkutano wa akinamama uliopita wa Uchaguzi. Harufu zinanuka za rushwa! Watu wamepambana, watu wanahonga waziwazi, leo rushwa haiogopewi, watu wanaona ni kitu cha kawaida. Hivi ninavyolalamika rushwa watu wengine wanaweza kuniona kama mtu wa ajabu hivi, kama siishi nchi hii. Lakini hili ni jambo la hatari. *(Kicheko/Makofi)*

Namshukuru sana Ndugu Wilson Masilingi. Juzi juzi nilisoma *statement* kwenye magazeti, baadhi ya viongozi wetu wapo wanasema jamani tutakwisha kwa rushwa, wanatangaza. Mheshimiwa Wilson Masilingi, akasema na sikuamini kama amejibu, lakini alisema kama Waziri kwa nafasi yake kwamba: "Jamani, viongozi tusizungumzie rushwa kama vile tunavyozungumza kwenye ngonjera hivi. Tusifanye ngonjera na suala la rushwa." Hata mimi ningependa maneno yake Mheshimiwa Wilson Masilingi, niyarudie kwamba rushwa tusiifanye ngonjera, ni hatari, lazima tupambane nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la pili ninalotaka kuzungumzia ni suala la ukabila. Mwalimu alituachia mambo haya, ukabila haujafa. Mimi nazishukuru zile Wizara ambazo zimetupa nafasi kwenye Kamati zetu za Kisekta kutembelea maeneo mbalimbali kujifunza juu ya Wizara zenyewe. Katika kujifunza huko tunajifunza mengi. Bado ukabila upo, unaweza ukakuta msururu wa watu wamewekana hapa mpaka kule kabila moja.

Mimi naomba ukabila upigwe vita. Jambo hili bado! Tukiacha mambo haya, kwa muda mrefu sana yatatumaliza. Wapo watu ninaowafahamu wameshakamilisha ukabila, sasa wanaulizana wewe ni ukoo

gani? Mimi naomba mambo haya tusiyaangalie kama utani, yatatumaliza, yatatuchoma moto kwenye Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ninalotaka kumalizia ni la udini. Bado tuendelee kupiga vita udini. Tuendelee kabisa kuelezana, kushauriana na kuonyana. Bila hivyo kwa kweli hatutafika. Tanzania ikianza kuwaka moto, tutakimbilia wapi kama hiyo mipaka yote imeharibika? Jambo la udini, napenda hapa kusema kweli nichukue nafasi hii pengine hata kwa niaba ya wenzangu Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili kumshukuru na kumpongeza Ndugu Rajab Yussuf Makamba, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mimi niko mbali, lakini namshukuru, amefanya kazi kubwa sana. Leo yuko Kanisani, keshokutwa yuko Msikitini, anapambana na mambo haya kwa niaba yetu. Juzi Dr. Salim Ahmed Salim, alikuwepo kwenye Shule moja pale aliitembelea, alisema Dar es Salaam ni Tanzania na mimi nakubali Dar es Salaam ni Tanzania. Mtu anayeweza kufanya kazi akaiweka Dar es Salaam katika hali ya ushwari na usalama, anaisaidia nchi yetu.

Mimi napenda tumpongeze Mheshimiwa Rajab Yussuf Makamba, kwa kazi nzuri anayoifanya na inawezekana tu akapewa hata kamisheni kidogo, wangapi wameporwa mapesa mengi wala hawajafanya kitu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kusema kweli naomba tusiyanyamazie hayo na kwa kipindi kilichobaki cha Mheshimiwa Rais, pamoja na vita dhidi ya kuinua uchumi na kuboresha maisha ya wananchi, haya matatu yaangaliwe kwa macho yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa, ukabila, udini, bado vipo na ni hatari. Yakifanyika haya na jitihada hizi zinazofanyika, kuinua uchumi wa Taifa letu, nina hakika kabisa kwamba Rais Mkapa mwaka kesho ataiacha nchi ikiruka kiuchumi na huku haya yakididimizwa kwenye kaburi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hiyo ya kuchangia jioni hii.

Mheshimiwa NAibu Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao tumewachagua kwa ajili ya kutuwakilisha kwenye *Pan African Parliament* pamoja na Mheshimiwa Mbunge ambaye tumemchagua kwa ajili ya Bunge la *SADC* pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninayo machache tu matatu. Lakini kabla sijaanza nitakuwa kidogo tofauti labda na michango mingine. Kabla ya hayo napenda kabisa niseme kwamba hii hotuba ni ya aina yake kabisa ambayo Rais wetu ameitoa, imekuwa ni kama mwongozo na maelekezo kwa watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu mimi katika shughuli zangu, hii miezi iliyobaki nikiwa Mbunge nitajitahidi sana kutembea na vitabu viwili. Biblia Takatifu na kitabu hiki kama miongozo. *(Kicheko/Makofi)*

Kabla sijachangia naomba nitoe *quotations.* Naomba mnisikilize kwa makini. Kuna *quotation* moja inasema hivi: *"No person can be a great leader unless he takes genuine joy in the success of those under him." Quotation* ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *quotation* ya pili: *"Nothing will divide this Nation more than ignorance and nothing can bring us together better than an educated population." Quotation* ya pili.

Ya tatu inasema hivi: *"Intelligence without ambition is a bird without wings." (Makofi)*

Naanza kufafanua walau kwa kifupi ili tuelewane. Nasema kwanza ile ya kwanza ni kwamba, kuna utaratibu ambao nimeushuhudia, nimeuona na nimejaribu kusema mara kwa mara, utaratibu wa ugawaji wa *National Cake,* wakati unapofika wa kugawana *cake* kuna kitendo kimoja ambacho kinafanyika kama tunavyojipanga wakati wa kukimbia, *on your marks, get ready go.* Atakayewahi mwenye nguvu, mwenye mabavu ya kusukuma mtu pembeni ndiye atakayefanikiwa. Sasa hili tutalifuatilia kwa makini mpaka utakapofikia wakati wa uchaguzi liwe limeshaondoka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kwamba, nchi hii ni moja, ni ya wote, kusiwepo na kitu chochote kwamba huyu ana nguvu, huyu ana uwezo, huyu ana *influence* mahali popote pale. Sisi sote hii ni nchi yetu, kila mmoja lazima aelewe hivyo. Kwa hivyo, kwa upande wa elimu, wakati tutakapoanza ule mpango wa MMEM ni lazima Mheshimiwa Waziri, awe makini kuhakikisha *plan* inafanyika kila Wilaya, ije na mahitaji na yafuatiliwe, kinyume na hapo, mimi naomba niseme tutakuwa wakali. Kwa hiyo, naishia hapo. *(Makofi)*

Nakuja kwa upande wa *intelligence without ambition is a bird without wings.* Ni kwamba kila kitu tunacho, yale yote yameshasemwa, maagizo yameshatolewa, makabrasha yapo. Lakini *without ambition,* watendaji, Watanzania wote tukafanya kazi, tukawa wabunifu, tukawa watundu, waaminifu, tusiwe wabinafsi, wenye nafasi katika sekta watimize wajibu wao kwa manufaa ya wote kwa kweli tutafika mahali pazuri sana. Lakini kwa pamoja tuhakikishe kwamba, nchi hii ni moja. *(Makofi)*

La pili, ni kuhusu migongano ya chakula. Tunaona kwamba nchi yetu ina kila hali ya kujivunia pamoja na kwamba mvua hazitoshi, lakini tunatakiwa tufanye mapinduzi katika kilimo. Tuhakikishe sasa tunaachana na ule utaratibu wa kuchukua takwimu kutoka kwenye nchi. Sijui nchi fulani inafanya hivi. Sasa hatuna budi kwenda kujifunza, yale waliyoyafanya kuanzia hatua ya kwanza mpaka kufikia mahali walipo, sasa wakati wa takwimu kutaja mafanikio ya wengine, umeshapitwa na wakati. Lazima sasa tujifunze namna wao walivyofikia haatua hiyo.

Nimesema kwamba, kutembea nitatembea na vitabu viwili. Yaani Biblia Takatifu na Kitabu cha Hotuba ya Rais. Naomba ni-*quote* maneno mazuri sana katika Kitabu cha Biblia Takatifu, ambacho kinapiga vita kuomba omba chakula na kitabu hiki ni cha hekima ya Yoshua Mwana wa Sara, Sura ya 40, mstari wa 28 mpaka 30. Naomba kunukuu kwa ruhusa ya Mheshimiwa Naibu Spika. Sikiliza kwa makini.

"Kuomba omba, mwanangu usiishi maisha ya kuombaomba, ni afadhali kufa kuliko kuomba omba. Mtu anapomtegemea mwingine ampe chakula, anaishi maisha ambayo hayastahili utu, kutegemea chakula cha mwingine ni kujiaibisha. Mtu mwenye akili, aliyefunzwa vema, ataepa kuishi hivyo, kwa mtu asiye na aibu kuomba omba ni kutamu. Lakini ndani yake kuna moto unamchoma". *(Makofi)*

Kwa hiyo, haya ni maneno matakatifu ambayo yanatuonya sasa wakati wa kuombaomba uishe. Tunatakiwa kabisa tulete mapinduzi ya kilimo. Tuone wengine wamefanya nini? Nilikuwa nasoma mabadiliko yanayotaka kufanywa na Serikali ya Zambia, wanasema wanataka kuleta mabadiliko kwa kuwapa wakulima ambao wameshachaguliwa tayari wawe ni mfano, wakulima 1,500 ambao watakuwa wanalima chakula kwa kufuatiliwa kwa karibu, waone kama kweli hicho chakula kinaweza kikasaidia kuondoa tatizo na aibu ya njaa kuliko sasa hivi tunavyokwenda kwa jumla. Kwa hiyo, lazima sasa tulete mapinduzi ya kilimo. *(Makofi)*

Lingine nataka kusema kwa kifupi, kwa sababu muda wenyewe hautoshi ni suala la Vyama vya Upinzani au kwa jumla vyama jinsi vilivyo. Ni kwamba, kabla sijaelea naomba tena nitoe *quotation* moja inayosema hivi, nanukuu: *"The line separating good and evil, pass not through scope no between political parties, either but right through every human heart".* Ni kwamba kinachosababisha hata mtafaruku, vurugu, kutokuelewana ndani ya Vyama vya Upinzani ni kukosa tu kuheshimu demokrasia ndani ya vyama vyao. *(Makofi)*

Watu wanang'ang'ania madaraka, viongozi wanataka kufanya yale wanayoyaona yanawafaa wao, siyo yanayowafaa wanachama. Kwa hiyo, ili sasa kuondokana na tatizo linalolikumba Vyama vya Upinzani na kukituhumu Chama Cha Mapinduzi, ambacho kwa kweli lazima mje mjifunze sasa, mjifunze

Chama Cha Mapinduzi kinafanyaje wakati kinapotaka kumpata mgombea. Kinamchekecha kuanzia ngazi ya chini, anachekechwa, anachambuliwa, anasema akina Saida kwamba anachambuliwa kama karanga, kuanzia kule chini, anachambuliwa na akishaingia kwenye ushindani anashindana hasa akijua kwamba atashinda.

Lakini kila leo imekuwa ni kukituhumu Chama Cha Mapinduzi, ndiyo kimesababisha matatizo. Matatizo ni ninyi wenyewe ambao mmeyasababisha, si Chama Cha Mapinduzi. Chama Cha Mapinduzi msikione kwamba labda kuna wachawi. Chama Cha Mapinduzi kimeshajiwekea utaratibu ambao unaeleweka. Mnachotakiwa kufanya msione aibu, njooni tuwafundishe na sisi tuko tayari kuwafundisha na kuwaelekeza na kuwaonyesha njia ya kufuata. Sisi siyo wachoyo. Tutawafundisha na mtakwenda na mtafanikiwa vizuri kuliko sasa hivi mnaposhindwa kwenu mnaanza kukibebesha Chama Cha Mapinduzi matatizo. Kwa hiyo, naomba sasa watendaji sasa ni zamu yenu kuhakikisha mnafuatilia kila hatua, haya makabrasha tunayoyaandaa, semina zote ambazo tunaziendesha, lazima sasa tuzifanye kwa vitendo kuliko vyote kuvirundika mahali ambapo ni kwenye makabati kesho na kesho kutwa tunakuta vimeshaota hata na utando wa buibui.

Baada ya kusema hayo, nasema kwamba, ninaunga mkono hoja kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache juu ya Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote, kwa kuwa ni mara ya kwanza safari hii kuchangia, naomba nichukue nafasi hii kuwapa pongezi wenzetu wote tuliowapigia kura hapa kuingia katika Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Nampongeza vile vile Mheshimiwa Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kujiunga na sisi na vile vile Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kuingia katika Bunge la *SADC. (Makofi)*

Vile vile naomba tujipongeze Wabunge Wabunge, kwa kupitisha ile Bajeti ya Nyongeza leo. Nadhani tutafanya kazi vizuri sasa na kukabiliana na tatizo hili la njaa. Naamini kabisa kwa nguvu ya pamoja sisi wote tutashirikiana katika kuhakikisha kwamba, wananchi wetu hawafi iwapo tutasimamia vizuri majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja niseme kwamba, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia moja. Kama alivyo Rais wetu ni mkweli na muwazi na vile vile hotuba yake ni ya wazi ni ya ukweli, tena ni ya ukweli kabisa. Mimi nafikiri sisi sote tumepata changamoto hapa kwamba pale penye mafanikio hata ya kwako mwenyewe nyumbani ni vizuri ukajisifu, ni vizuri ukasema wazi kwa wenzio, hakuna mtu wa nje ambaye atakuja kwako na kusema wewe unafanya vizuri ndani ya nyumba yako. Jisifu mwenyewe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais ametuonyesha mfano. Tuisifu nchi yetu na mafanikio yake yote, hakuna mtu mwingine ambaye atatusifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi katika mafanikio aliyoyazungumzia Mheshimiwa Rais tunaona vijijini na hakuna mmoja wetu hapa ambaye atabisha kwamba sasa elimu ya msingi ni bora kabisa kuliko miaka ya 80, hakuna. *(Makofi)*

Hakuna atakayesema hapa kwamba huduma za afya hazijaendelezwa. Hakuna atakayebisha kwamba hali ya barabara ni nzuri sana katika maeneo yetu, maji, mtandao wa mawasiliano, simu kila mahali. Hivi sasa ukisafiri kutoka hapa labda unakwenda Dar es Salaam, hata kama umesahau mfuko wako huko nyuma, utaupata baada ya muda mfupi kwa sababu utakuwa umewasiliana na hao uliowaacha nyuma. Kwa kweli napenda kupongeza kwa mafanikio haya yote ambayo nchi yetu imejitahidi kufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua kama hii tuliyoifikia hivi sasa, naamini kabisa, inaweza ikafikia katika hatua ya juu zaidi iwapo tutajenga taratibu nzuri za Utawala Bora katika ngazi za Vijiji na Kata. Ni lazima huko tuanze nako, kuna matatizo makubwa. Tujenge yafuatayo:-

Kwanza, viongozi wenzetu katika maeneo haya niliyoyataja wawajibike vizuri kwa wananchi, wawe wazi kwa wananchi na kuwa karibu na wananchi. Pili, wawe na uwezo wa kuwahamasisha wananchi wao kufanya kazi kwa bidii kuwahamasisha, tofauti na hali ilivyo katika vijiji vingi. Viongozi hawana hata ubavu, hawana hata uwezo wa kufika mbele ya wananchi na kuwaambia tufanye hivi, hawana uwezo. Vile vile wawe na uwezo wa kuchukua hatua pale ambapo pana ulegevu. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa hatua nzuri waliyoianza sasa ya kutoa mafunzo kwa viongozi wa ngazi za Kata na ngazi za Vijiji. Hilo ndilo jawabu, bila kuwa na Utawala Bora katika ngazi hizo hatuwezi tukainua kiwango cha mafanikio tuliyofikia hivi sasa tukayapeleka katika hatua ya juu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie suala la elimu, labda nijihusishe zaidi katika elimu ya juu. Katika ukurasa wa 38 Mheshimiwa Rais amesema: "Uwezeshaji kwa njia ya elimu ni sehemu muhimu ya mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na utandawazi". Anasema: "Lengo la Serikali ifikapo mwaka 2008 ni kuwa na wanafunzi 55,000 katika Vyuo vya Elimu ya Juu."

Mheshimiwa Naibu Spika, naona hii ni changamoto kubwa sana kwanza kufikia hatua hiyo, najua tunaweza kabisa na kama tunataka kufanya hivyo ni lazima tuhakikishe kwamba, elimu ya sekondari inayotolewa iwe bora, tujenge mazingira mazuri ya shule zetu ili taaluma inayotolewa iweze kuwa bora. Hivyo basi, tuweze kupata vijana wanaoingia katika vyuo vyetu wakiwa bora na matunda ya wahitimu basi yawe bora. Hivi sasa naambiwa kwamba, pamoja na uwekezaji mbalimbali ambao tumeufanya, tumebinafsisha makampuni mengi, tuna makampuni ya kigeni yapo hapa ndani, baadhi ya hao wenye makampuni wanathubutu kusema kwamba vijana wetu hawajafikia kiwango kizuri cha elimu ya juu na hivyo kuleta vijana kutoka nje. Mimi nafikiri hayo ni matusi.

Naamini si kweli kwamba, vijana wetu hawajaelimika kiasi hicho. Sasa kama tunataka kupigana na wenzetu katika dunia basi tujielekeze katika kuboresha vizuri sana elimu ya watoto wetu iwe ya hali ya juu. Lakini pia naona ni changamoto kwetu, pia kwa kuweka mipango mizuri ya kuongeza idadi ya Vyuo Vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais amesema tunaweka malengo ifikapo mwaka 2008 tutakuwa na wanafunzi 55,000 katika vyuo vyetu; maana yake nini? Maana yake vile vile ni kupanua wigo wa vyuo vyetu. Mimi nakumbuka miaka ya 1984/85 Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, labda atanisahihisha, lakini nakumbuka Mheshimiwa Rais, Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, alisema pale Mbeya kwamba, Chuo cha Ufundi cha Mbeya kibadilishwe katika miaka 10 ijayo kiwe Chuo Kikuu cha Ufundi, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Ninayakumbuka sana maneno yale na yalitupa matumaini makubwa sana na niliamini kabisa kwamba, tangu wakati huo wenzetu waliosomea mipango au waliopewa dhamana ya mipango, basi wangeanza kuliweka hilo katika mipango. Hivi sasa ninavyozungumza, naamini kabisa baada ya miaka zaidi ya 15 hicho chuo kingekuwa kimeshaanza. Kuna tatizo gani? Tunaomba tupate maelezo. *(Makofi)*

Kama Mheshimiwa Rais anasema kwamba, hivi sasa tuna idadi ya wasichana katika vyuo vyetu kwa asilimia 33.1. Je, kama tungeweza kuongeza Chuo Kikuu cha Mbeya cha Sayansi na Teknolojia na vingine tusingeweza kufika hata asilimia 50 ya wasichana walioko katika Vyuo Vikuu hivi sasa. *(Makofi)*

Naomba sana, tena naomba sana, nitoe hii changamoto na Mheshimiwa Rais ametupa changamoto, anatuachia kazi sisi tunaomsaidia, sisi tunaomsaidia tumshirikishe katika mawazo haya mazuri kwamba kama tukiweza hapa Tanzania tukafanikiwa kuwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, ni rekodi ya Afrika, ni rekodi kabisa. Tutaweza kupiga hatua kubwa sana katika maendeleo yote ya kisayansi na kiteknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie kwa kifupi juu ya uwekezaji katika sekta ya mawasiliano. Nafurahi kwamba, Serikali ina mpango wa kukodisha huduma za reli. Nasema huduma za reli ni huduma muhimu sana katika nchi yetu na katika kukuza uchumi wetu. Ni kweli kabisa tumeelekeza

nguvu zetu katika kuboresha barabara zetu. Hatua nzuri kabisa na ninaipongeza hatua hiyo lakini iende sambamba na kuboresha huduma za reli. *(Makofi)*

Kama ilivyozungumziwa katika hotuba tuliyokuwa tunazungumzia hapa jana kwamba, hivi sasa tunahitaji usafirishaji wa reli ili kusafirisha chakula chetu kutoka kona nyingine kwenda kona nyingine, kama wangetumia magari, hatuwezi. Lakini vile vile magari mazito yanapokuwa barabarani yanaharibu barabara zetu, bora tupeleke mizigo kwenye reli halafu tuache na sisi tunufaike na barabara, si ndiyo hiyo. Si ingekuwa safi hiyo? *(Makofi)*

Mizigo mizito isafirishwe kwenye reli halafu sisi tufaidi barabara ili zidumu kwa muda mrefu, ndiyo tutaimarisha uchumi. Kwa hiyo, nafikiri hatua tuliyoanza jana ya kutoa ziada ya fedha shilingi bilioni 2 kama sikosei, kwa ajili ya kuimarisha huduma za reli ni pongezi kubwa na ni hatua nzuri tuliyoanza nayo. Lakini vile vile katika mipango yetu ya baadaye ya kiuchumi tuelekeze nguvu zetu kuboresha huduma za reli ziwe nzuri lakini na wale wanaopenda kusafiri kwa reli nao watafaidika sana na ninaamini hata hapa ndani wapo wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri wakati umefika wa kubadilisha mtazamo wetu wa kuelekeza nguvu zetu za kiuchumi kwa kuboresha miundombinu ya reli. Mwisho katika sekta hiyo, narudia kuyapongeza makampuni yanayofanya kazi ya kuweka mitandao ya simu kila mahali. Naamini siku moja simu zitafika mpaka Ludewa, mpaka kule Ziwa Nyasa, ili tuweze kuwasiliana vizuri na sehemu nyingine za dunia. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Mheshimiwa Rais. Ukweli bila kuficha, tumefurahishwa sana na kitendo hicho cha Rais na tunamshukuru sana. Napenda kuwapongeza Wabunge wenzetu ambao wamechaguliwa kuingia katika Bunge la Afrika. Vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kwenda kutuwakilisha katika *SADC.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza nasema kwamba, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais mia kwa mia. Napenda sana kumpongeza kwa hotuba yake nzuri, ambayo kwa kweli ametukumbusha tulichofanya huko nyuma na tunakokwenda katika kipindi cha miezi 20 na hata baada ya hapo tena ametuambia kwamba, Mungu akipenda, atatuachia uchumi unaofaa. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Awamu ya Tatu, mambo makubwa mengi yamefanyika. Kwanza la muhimu zaidi ni uchumi. Uchumi wetu kwa sasa unakua kwa asilimia 6.3. *Inflation* ipo kwa asilimia 4. Siyo nchi nyingi ambazo zimeweza kukuza uchumi wake kwa kiasi hicho na *inflation* kuwa chini. Kwa hiyo, napenda sana kumpongeza Rais ni kwa sababu ya uongozi mzuri tumefikia hapo. *(Makofi)*

Watoto wetu wote wa miaka saba sasa wanaenda shuleni. Awe maskini awe tajiri, sasa hivi watoto wetu wanaenda shule. Hicho ni kitu kikubwa mno na siyo nchi nyingi ambazo zimeacha ku-*achieve* hicho kitu na huo ni uongozi mzuri wa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Utawala Bora, kwa kweli Tanzania tunaishi kwa amani. Hata ukiwa na nani, unajua kabisa kwamba, ukifanya kosa utachukuliwa hatua. Kwa hiyo, napenda sana kumshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa hilo. *(Makofi)*

Imezungumzwa kuhusu rushwa, jamani mnajua kuna wakati ilikuwa ukifika mahali huwezi kupewa faili bila kutoa chochote. Lakini nimeanza, maofisa hawajui kwamba ni Mbunge, nimetuma watu maofisini, kwa kweli sasa hivi mafaili siku hizi yanatoka bila tatizo. *(Makofi)*

Nimetuma watu pale Ardhi kwa Mheshimiwa Cheyo, nimekwenda kila siku natuma vijana wanaenda wanafanya mambo wanarudi. Nimeenda *Airport* mambo yangu yanakwenda vizuri. Yaani kwa kweli jamani wanaosema kwamba kuna rushwa, ndiyo ipo, hatuwezi kukataa, lakini hakuna mtu asiyejua kwamba, Mheshimiwa Rais ameipiga vita rushwa. *(Makofi)*

Ninapongeza jamani, tumetoka mbali na Mheshimiwa Cheyo, nikupongeze sana pale Ardhi mambo yako ni mazuri na Naibu wako na wafanyakazi wote nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwamba, kila tarehe 30 ama 31 Mheshimiwa Rais hulihutubia Taifa na kuna kitu kimoja alipokuwa akisema mara ya kwanza niliona aah! Akapita tena mara ya pili, mara ya tatu likaniingia nacho ni utandawazi na soko huria. Mheshimiwa Rais haachi kulizungumzia hilo. Lakini ukweli jamani tukumbuke kwamba, Karne ya 21 Taifa hili lisipoingia kwenye utandawazi na soko huria tutaachwa nyuma. Namsihi sana Mheshimiwa Rais asichoke. Yeye aendelee kutuhamasisha kwamba, Watanzania jamani tujiunge kwenye utandawazi na soko huria tusiachwe nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake hiyo nzuri na mambo mengi yaliyofanyika, kuna machache ambayo nafikiri yanatakiwa kufanyiwa kazi ili tuwe na uchumi endelevu.

Moja ni *budget deficit.* Sisi tunapokuja hapa kwenye bajeti yetu 40%, mwaka huu tuna 42% *budget deficit.* Nimeingia hapa nasikia *40% to 50% budget deficit* huwezi kusema una uchumi uliokomaa kama una *budget deficit* ya 40%, haiwezekani. Tunaomba Serikali kwa makusudi kabisa itenge kipindi *may be* miaka kumi kila mwaka tupunguze *budget deficit by 5%* ama sivyo siku *donor* atakapokuja kutuambia mambo ambayo si ya maslahi ya Taifa tukakataa, watajenga hoja kina *Uncle Sam* watasema sasa usiipatie Tanzania hela hii 40% utaitoa wapi? Kwa hiyo, naomba sana hii *budget deficit* iangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni deni la nje bado ni kubwa pamoja na kwamba tumesamehewa lipo, naomba tukazane. Uchumi wetu unavyozidi kukua tuendelee kulilipa kwa kasi na tusikope hela ovyo ovyo bila sababu za kutosha. Nchi kama Morocco wanajaribu ku-*eliminate* deni lao la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *interest rates*. Siku hizi nchi zote ulimwenguni huwezi kujenga nyumba bila kukopa, huwezi kununua gari bila kukopa, huwezi kununua nguo bila kukopa sasa *interest rates* zetu bado ni kubwa na ili uchumi wetu utengemae, tunaomba tuziangalie hizi Benki kwa nini wana *interest* kubwa ukienda kukopa unalipa 24%, wewe ukiweka hela unalipwa 1%. Mimi nilishangaa sana tena anakulipa mwisho wa mwaka eti uweze kufuatilia kama amekulipa *interest* ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Kodi ya *VAT* ni kubwa mno. Nenda hapo *South Africa VAT is just 14%*, ukienda Uingereza haifiki 20%, sasa sisi hii *VAT* unakwenda kununua gari ukija kupigwa *VAT* gari ambayo unaileta ni kubwa mno. Sasa *VAT* inaweza kutudanganya kwamba tunapata hela nyingi lakini ni hela ambazo zinatokana na kodi ambazo ni za ajabu. Nashauri ingekuwa kati ya 13% - 15% ili tu-*stimulate* uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ukitembelea viwanda, tumetembelea viwanda vingi sana mfano *textiles,* ukimwuliza wewe una *export* vitu vyako? Anasema hakuna. Sababu kubwa ni bei ya umeme iko juu. Sasa sisi tunatengeneza vitu kwa ajili yetu wenyewe kununua humu ndani lazima tu-*export.* Hii bei ya umeme kwa nini iko juu sana. Kenya wanaleta vitu vyao hapa, tunaagiza *South Africa* bei ya umeme ni *cheap.* Huu umeme utatudumaza, lazima vitu vyetu viuzwe nje kwa nini sisi hatuuzi vitu nje tuagize tu? Jana nilisoma wanasema tunachoweza kuuza ni korosho tu na nini na ukiuliza watu wanasema eeh korosho na vinyago ndugu yangu huwezi kutegemea kuuza vinyago twende kwenye *textiles* utengeneze vitu kama nguo nzuri tukauze huko na kufanya hivyo lazima uwe na bei ambayo ina-*compete* kule *AGOA.* *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya *diesel* ukienda nchi nyingine tunanunua mafuta huko huko Mashariki ya Kati tunaleta hapa, ukienda hapo Rwanda mafuta yanapita yanakwenda kule bei rahisi sisi

tumeweka kodi pale pale. Ukisema kwamba utoe gari Musoma ulipeleke Bukoba kwa Mheshimiwa Masilingi, uwapelekee sijui bhangi ama ndizi, huwezi kulipeleka lile gari pale utakaporudi yaani ile bei tu ya kuzisafirisha hizo ndizi hazitanunulika. Tunaomba muangalie suala hili, kodi zimezidi sana *almost 50%* ni kodi. Sasa kwa nini tunakaba uchumi wetu kwenye uti wa mgongo ukimkaba mtu uti wa mgongo hawezi kusogea. Kodi hizi zinatuumiza, tuwe *productivity* iki-*stimulate transport* yako ikiwa rahisi ni kwamba unaweza kwenda Mbeya kule ukanunua vitu ukaleta Dar es Salaam kwa hiyo, unakuza uchumi wa kule, unaweza kwenda kule Musoma ukanunua kitu ukaleta, lakini nimejaribu niingie kwenye *transport business* nikapiga mahesabu nikataka kununua lori na mimi niingie kwenye soko huria lakini nikapiga mahesabu haraka haraka nikakuta hamna kitu hapo, nikaacha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote iliyo na madini ni nchi tajiri, ingia Botswana ni matajiri wa kutupwa, ingia *South Africa* ni matajiri, sisi tuna madini lakini ni maskini. Nimeenda Geita watu wa nje wanakuja kuchukua madini halafu wanaanzisha wanapewa *Agro-forest Project,* bustani hata juzi nilisoma, nenda kawaangalie wale watu waliopewa bustani wana maisha ya kusikitisha, nilienda Geita pale. Juzi nilienda Nyamongo kwetu huku yaani watu ni maskini. Tuna madini mengi kwa nini sisi tunaendelea kuwa maskini na ile sio *renewable resource,* ukienda ile miradi wanakuambia *ten years* sasa *ten years* mradi mbona umefika na watu hapa ni maskini? Tuangalie Sera yetu ya Madini kwa nini *South Africa* ni tajiri, Botswana ni matajiri kwa ajili ya madini na sisi sio matajiri wakati tuna dhahabu, sisi ni watu wa tatu katika ulimwengu kuwa na dhahabu nyingi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais alipotembelea Serengeti tarehe 4 Oktoba, 2000, alituahidi vitu viwili kwamba, tutapata umeme na maji. Napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa ahadi alizotoa na mwelekeo ni kwamba, ahadi zake hizi zitatimia, mwelekeo ni mzuri, mambo yameanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mambo ya maji, Mheshimiwa Lowassa, ambaye ni rafiki yangu wa karibu alikuja mwenyewe mpaka Serengeti tukamwitia mkutano akasema jamani mtapata maji. Mheshimiwa Lowassa mambo yameanza nakushukuru sana wewe, Naibu wako na wafanyakazi wote. Yale maji tunayahitaji na naamini kwa uongozi wako Mheshimiwa Lowassa tutayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme siachi kwenda kumwona Mheshimiwa Dr. Msabaha na Mheshimiwa Yona, nafikiri tenda zimefunguliwa au karibu watafungua kwa hiyo naona hiyo ahadi nayo itatimia. Kwa hiyo, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Daniel Yona, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kufuatilia ahadi za Mheshimiwa Rais. Tunaomba mtusaidie tupate vitu hivi kwa sababu ni muhimu sana ama sivyo hicho ndicho kitakuwa kigezo cha Wapinzani kusema tuliahidiwa na Mheshimiwa Rais na hakuna kitu lakini nashukuru sana kwamba mambo yanaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, naomba nimwombe Mwenyezi Mungu amsaidie Mheshimiwa Rais apone upesi, ampe hekima na afya njema aliendeleze Taifa hili kipindi kilichobaki na hata kipindi kikiisha bado aendelee kumpa afya njema na hekima, awe mshauri wetu kama Baba wa Taifa alivyofanya na Mzee Ruksa anavyofanya ni mtu ambaye tunamtegemea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sina mengi zaidi napenda kushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, *Asalaam alaykum!*

**WABUNGE FULANI:** *Waalaykum salaam!*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kushukuru sana kwa kupata nafasi hii niweze kusema machache katika hotuba ya maelekezo aliyotoa Rais mpendwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Mara nyingi tunamsikia Rais wetu katika hotuba zake anazotoa kila mwezi lakini hotuba aliyoitoa hapa Bungeni ni kubwa kuliko. Kwa hiyo, napenda kumshukuru na kumpongeza Rais kwa jinsi ambavyo alikuwa amejiandaa kuliambia Taifa mambo ambayo Taifa hili limefanyiwa kwa kipindi cha miaka nane ya utawala wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao wameingia Bungeni sasa hivi wanaweza kuwa labda wamesahau, lakini mimi nathibitisha kwa sababu nimekuwepo toka mwaka 1995, hali kwa kweli ni nzuri, yenye matumaini mazuri na hata ile ahadi aliyoisema Mheshimiwa Rais kwamba ataondoka ndege inapaa, naamini itakuwa mawinguni kabisa kwa jinsi kazi inavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maeneo machache sana ya kuongezea katika kuboresha Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Naamini sote tunakubaliana kwamba, Watanzania zaidi ya asilimia 80 ni wakulima, wafugaji na wavuvi. Wavuvi ni wachache sana na mimi kwangu kule sijui sana mambo ya wavuvi, sitaki kusema juu ya hilo, lakini nitazungumzia juu ya kilimo. Kilimo na ufugaji kwenye maeneo yetu vinaenda pamoja, sasa naanza na kilimo. Kilimo kinachukua zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania na tumesoma katika Hotuba ya Rais kwamba, kilimo kilikua kwa 3.1% kwa mwaka na mwaka 2002 kilikua kwa 5%, mwaka huu ilitegemewa kikue kwa 6%. Kwa hiyo, utaona jinsi kinavyokua kinakwenda polepole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia sababu kubwa za kilimo chetu kukua taratibu na kudhani kuwa pengine bado hatujatilia mkazo sana suala la kilimo. Tunayo Wizara ya Kilimo na Chakula lakini nadhani bado hatujatilia mkazo suala la kilimo. Sababu nyingine nadhani hata katika ile *vision* ya kufukuza umaskini ya 2025 haisemi sana ni namna gani tunawaondoa wakulima wetu katika kutumia jembe la mkono. *(Makofi)*

Mimi nadhani tukiwaondosha kwenye kutumia jembe la mkono tukawaingiza katika kutumia matrekta madogo madogo, tukawapeleka katika kutumia wanyama kazi na vitu vya namna hiyo, inawezekana kusaidia katika kufukuza umaskini lakini vile vile inawezekana kusaidia kukuza mashamba yao na kipato chao. Kwa hiyo, ni changamoto kubwa sana katika Wizara hii ya Kilimo kuangalia hili na kubuni namna ya kuwaondosha wakulima wetu katika kutumia jembe la mkono na pengine ndio sababu ya kuwa na balaa la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule kwetu kwa kweli tumejaliwa vitu vingi lakini kikubwa ambacho Mungu ametujalia ni nguvu, tuna nguvu, Wasukuma, Wanyamwezi wana nguvu, huo ndio ukweli wenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo makabila mengine hapa siku zote mimi huwa nasema, wanashindwa hata kuokota korosho mpaka wasimamiwe na Katibu Tarafa, kuokota korosho, lakini sisi tumejaliwa nguvu tunaweza. Yapo makabila mengine hata kupalilia shamba mpaka asimamiwe na Mtendaji wa Kijiji au Kata na wengine wana barabara nzuri tu kama Wazaramo wanatengenezewa barabara nzuri, za nini hizo? Sisi kule tumejaliwa nguvu. Kwa kweli kama maeneo yetu hayo tungewezeshwa, nawahakikishia Watanzania tungeweza kuilisha nchi hii bila matatizo kwa sababu tuna nguvu, uwezo na tuna akili na tuko wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu kuna msemo unasema: *"Wangebolya wangebokonalamiso"*. Maana yake ni kwamba, kwa njaa ya mwaka huu hata sisi wenye nguvu tumepata njaa. Hii ni changamoto kwa Serikali, Serikali iangalie sana maeneo ambayo wanaweza kutumia nguvu kazi, raslimali ya nguvu ambayo ipo kuepukana na njaa ambayo inasababishwa na watu wengine ambao wana maeneo mazuri, mvua nzuri, hawawezi kufanya kazi. Siku moja nilikwenda Lindi nilitamani ule Mkoa ungehamia kwetu kwa sababu tungefanya *wonders,* kweli kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ile ya hotuba nilisema tunaiambia Serikali mwaka huu tuna njaa na bado nasisitiza kwa Hotuba hii ya Rais pamoja na pesa ambazo tumezitoa kwenye ongezeko la bajeti yetu lakini bado nasema mwaka huu eneo la Kanda ya Ziwa, Magharibi, kuna njaa na ni njaa kweli kweli. Bahati nzuri sisi kule hatujazoea kuombaomba, yapo makabila mengine yana itikadi ya kuomba kama Wagogo. Ukipanda treni ukifika tu mahali unaambiwa "Saidia baba" wala usiulize Dodoma ni wapi ujue umeshafika Dodoma, wao tabia hiyo wamezaliwa nayo lakini sisi kwetu kule hatuna tabia ya kuombaomba. Sisi tunachotaka tunataka chakula cha kununua kwa bei rahisi hatutaki chakula cha msaada, tunataka chakula cha kununua kwa bei rahisi, hiki chakula cha ombaomba pelekeni Dodoma tuleteeni chakula cha kununua cha bei rahisi. Nilitaka niliseme hili ili tuweze kuelewana vizuri. Naomba Serikali izingatiwe, wakulima wa kanda hiyo wana njaa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Watanzania wengine ni wafugaji na eneo letu ni la wafugaji vile vile. Tanzania ni ya tatu katika Afrika kwa mifugo sijui kama takwimu zangu ni sahihi na inawezekana, Tanzania ina ng'ombe milioni 18 au zaidi, sisi tuko milioni 35 kwa hiyo kila watu wawili wana ng'ombe mmoja, ukisema mifugo maana yake ni ng'ombe na Tanzania ni nchi ya mwisho kwa kusafirisha nyama. Hii ni changamoto kwa Waziri wa Maji na Mifugo, rafiki yangu Mmasai. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara yake amefanya mambo mengi sana mazuri hasa kwa upande wa maji, lazima tumpongeze mazuri makubwa tu tangu nchi hii imepata uhuru hatujawahi kuchimba malambo katika msimu huu tumechimba malambo hata kule kwangu tumechimba malambo, kwa hiyo nampongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa mifugo bado hatuna kiwanda cha mifugo na bahati nzuri ni mtoto wa mfugaji ni wenzetu hawa wafugaji wenzetu, tujenge kiwanda cha mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, atetee wafugaji kwa nini tunaweza kutoa ruzuku kwa wakulima wa kilimo cha mahindi, tunashindwa kutoa ruzuku kwa mifugo hasa ng'ombe hasa katika eneo la madawa. Nao wanayo haki, kama tunayo haki kutoa ruzuku kwa mahindi basi tunayo haki ya kutoa ruzuku ya dawa ya majosho ili ng'ombe wetu waogeshwe, ng'ombe wetu wachanjwe, ng'ombe wetu wachomwe sindano ya kuzuia magonjwa na ndio watakuwa na soko kwenye masoko ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani pamoja na juhudi ambazo Serikali inafanya, bado kwenye mifugo hatujawekeza na mimi nasema kama tukiwekeza kwenye mifugo soko lipo. Tumezungukwa na nchi hizi zinazopigana kila siku za Rwanda, Burundi, *DRC,* sina hakika ya takwimu za Rwanda na Burundi lakini najua *DRC* wanakula nyani badala ya kula nyani tungewapelekea nyama ya ng'ombe, ilikuwa soko zuri sana kama tungekuwa wajanja kusimamia soko hilo la *DRC* tukapeleka ng'ombe wakaondokana na kula nyani watu wa *DRC*. Natoa changamoto Serikali iweze kufanya cha maana katika soko hili la mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilikuwa nataka kuzungumzia ni upande wa maji. Mheshimiwa Waziri wa Maji tunakupongeza lakini wakati wa bajeti yako ulituahidi kwamba, Benki ya Dunia imeahidi kuziingiza Wilaya 30 katika kusaidia ukarabati na upatikanaji wa maji. Wananchi wako tayari umeona mfano katika MMEM sasa tuambie ni lini watakuja kusaidiana na sisi kuondoa matatizo ya maji hasa katika maeneo kame.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii vile vile kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji katika suala la kutumia maji ya Ziwa Victoria. Kwa kweli hiyo ni kazi nzuri na tulikuwa tunasubiri kwa muda mrefu na tunasubiri utekelezaji wake kwa hamu sana. Tunaomba Serikali sasa baada ya kuanza kutumia maji hayo ya kunywa, hatua ya pili naomba tutumie hata kwa umwagiliaji. Pamoja na mikataba iliyopo ya kidunia iliyofanywa zamani hebu tuharakishe tutumie kwa umwagiliaji. Kuna Bonde la Mto Manonga pale linachukua Mkoa wa Shinyanga, Tabora, mpaka Singida ukiwezesha maji ya Ziwa Victoria yakateremka pale chini hatutakuwa na njaa, maji yale hayawezi kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kusema ni juu ya uchumi wa Kijiografia. Katika Hotuba ya Rais tumeambiwa kwamba, uchumi unakua kwa 5.6% lakini nadhani maeneo mengine ambayo bado hatujayaibua kwa mfano Kanda ya Magharibi, Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Sumbawanga na Kagera, maeneo haya tukiyaibua kwa uchumi yatasaidia sana kuibua uchumi wetu vile vile kwa sababu yana raslimali nyingi sana. Juzi nimesikia Kagera wanaweza kufanya hata utalii lakini hatujaibua uchumi wa kufanya utalii kwa Kagera, hebu tuchangamkie na uchumi wa maeneo mengine ambayo tunaweza kuyaibua. Kuna maeneo mengine hatujayaibua kabisa kwa utalii kama Mtwara, Mafia, nadhani ipo haja ya kuanza kufikiria upya maeneo mapya tusing'ang'anie maeneo yale yale ya Kijiografia ya tangu zamani, yako maeneo mengi mapya ambayo tunaweza kufanya mambo mazuri katika suala hili la kuinua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo inajenga barabara mbalimbali kuelekea Magharibi, Kusini na kadhalika lakini vile vile tunaomba ijenge ya kwenda Kigoma na Mbeya kutokea Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tutumie nafasi hii kufanya *Mwanza Airport* uwe ni Uwanja wa Kimataifa. Hakuna dhambi kuwa na viwanja vya Kimataifa vingi, tuwe na Uwanja wa Kimataifa kwa ajili ya kuchukua Rwanda, Burundi, Uganda, pamoja na Kenya na pale pana samaki wengi tu ambao wanaweza kuvuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nisingeweza kukaa kimya, mimi ni mwanamichezo. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais, bahati mbaya sana kwa sababu ilikuwa na mambo mengi ambayo yamefanyika, hakuzungumzia juu ya Uwanja wa Taifa. Sasa Serikali ipo na ahadi ya Rais ilisema kwamba, kabla hajaondoka madarakani atakuwa amejenga Uwanja wa Taifa Dar es Salaam. Sasa kwa niaba ya wanamichezo wenzangu, napenda kujua hatma ya Uwanja wa Taifa imefikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nichukue nafasi hii kuitahadharisha *FAT* na yenyewe ibadilike. Inawezekana mambo mengine tunaweza kusababisha sisi wenyewe *FAT* na vyombo vingine vinavyoendesha michezo vinafanya hata mambo mengine kuwa ya wasiwasi kuyashabikia. Kila siku sisi Watanzania tumekuwa ndio wasindikizwaji wa kufungwa magoli mengi sana lakini tungeweza kuwa ni moja ya vitu vizuri vya kujivunia hata kwenye mpira wa miguu. Sasa hivi kuna vuguvugu la kufanya sijui mikutano, sitaki kusema sana juu ya hilo lakini hata kama aingie nani, awepo nani *FAT* ibadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa dhati kabisa, kwa kunipa nafasi ya kufunga pazia kwenye majadiliano yetu jioni ya leo. Awali ya yote, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza sana Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais aweze kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hakika Mheshimiwa Rais, ametekeleza na kukamilisha kazi yake kama alivyopewa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Lakini pia napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamechaguliwa na Bunge hili kwenda kutuwakilisha katika Bunge la Afrika, nawapongeza sana. Nisiwe mnyimi pia naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuweza kutuwakilisha kwenye Bunge letu la *SADC. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme naunga mkono Hotuba ya Rais kwa asilimia mia moja. Hotuba ya Rais ilikuwa nzito sana na mimi nasema ilikuwa ni hotuba shirikishi kwa sababu alituweka mle katika hotuba yake na akatufanya ni sehemu ya utekelezaji wa shughuli zake katika kutekeleza kazi zake za maendeleo ya nchi hii kwa kipindi ambacho kimesalia. Kwa hiyo, nampongeza sana na ni wajibu wetu kama Wabunge kweli tumsaidie aweze kumaliza kipindi chake na kukamilisha yale ambayo amekusudia kwa kipindi hicho. Kazi alizokwishafanya Mheshimiwa Rais pamoja na timu yake ya Mawaziri kwa kipindi chote ambacho amekuwepo madarakani cha miaka minane kwa kweli sio haba labda mtu aliyekipofu na asiyesikia ndiye anaweza kuhoji kazi ambayo imekwishafanyika mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri pamoja na Watendaji wa Serikali, ambao wamekuwa ni sehemu ya utekelezaji wa kazi hizo wakimsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia machache, namshukuru sana Mheshimiwa kaka yangu Kagonji amezungumzia hoja ambayo mimi nakusudia kuizungumza tena nayo ni hoja ya rushwa. Pamoja na mafanikio yote ambayo Serikali yetu ya Awamu ya Tatu imepata lakini lazima tukubali kwamba, rushwa bado ni tatizo kubwa ambalo linatuzungukia.

Hatuwezi kukwepa hilo kwa sababu viongozi ndani ya Makanisa wanasema, viongozi ndani ya Misikiti wanasema, wananchi wanasema na baadhi ya viongozi wa Serikali wanasema. Sasa najiuliza ni nani wa kumtupia mzigo wa kupambana na rushwa kwenye nchi yetu? Tumwachie Mheshimiwa Rais hii

kazi ya kupambana na rushwa peke yake, tuwaachie Mawaziri, Wabunge au tuwaachie *PCB* maana *PCB* wamefika mahali wanakubali kazi ya kupambana na rushwa sio kazi lele mama na wao sasa wanasema kwamba, sehemu kubwa ya chimbuko la rushwa ni rushwa ya kisiasa ambayo hawataki kuizungumza vizuri ni rushwa ipi hii ya kisiasa. Lakini nashukuru kwamba, Mheshimiwa Kagonji ameeleza suala la rushwa tusipoli-*address* kwa kiasi cha kutosha litavunja nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, CCM kama Chama Tawala, ndani ya Katiba yetu tunasema rushwa ni adui wa haki, Katiba ya nchi inapinga rushwa lakini bado ni tatizo ambalo sasa kila mtu anakuwa mkimya kulijadili. Tofauti ya mapato inazidi kuwa kubwa kati ya maskini na wachache walionazo sasa hivi tofauti na miaka ile ya 1960 sisi tulivyokuwa vijana wadogo wakati huo wazee wetu, kaka zetu, walikuwa kweli wamedhamiria kufanya kazi ya nchi, maslahi ya nchi yalikuwa mbele na maslahi binafsi ilikuwa ni kitu cha baadaye sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika kipindi hiki tulichonacho, watu wanashindana kuhodhi mali aidha zimepatikana kihalali au kiharamu. Fedha haramu ambayo inatokana na wafanyabiashara wachache wanaokwepa kulipa kodi ya Serikali wamekuwa na fedha ambazo sasa wanatengeneza na viongozi. Sasa hao viongozi ambao watatokana na hao *kingmakers* hivi tutaifikisha nchi wapi? Kwa hiyo, sasa tunashindana kutafuta fedha na mali haramu ili baadaye tuingie kwenye siasa, tukishaingia kwenye siasa tutengeneze viongozi kwa hiyo tunatengenezewa Madiwani, Wabunge na hatimaye tutatengenezewa Marais na watu wa namna hii. Naomba niwapongeze sana watu wa habari wamekuwa wakizungumza kwa kina kabisa kuhusu tatizo la rushwa, haliwafurahishi watu wengi lakini ndio ukweli. Hivi kwa nini unyooshewe vidole mara tatu, mara nne, wewe mtu mmoja tu?

Kwa hiyo, nasema suala la rushwa ni lazima litafutiwe utaratibu mpya wa kulishughulikia. Nimekuwa nikihudhuria semina na warsha nyingi sana zinazoendeshwa na Taasisi yetu ya Kuzuia Rushwa. Hii taasisi inapewa bajeti ya kutosha, taasisi inawezeshwa na Serikali kwa maana ya bajeti na vifaa vya kisasa ili iweze kupambana na rushwa lakini taasisi hii inabadilika kuwa taasisi ya kufanya utafiti wa rushwa na si kupambana na rushwa. *(Kicheko/Makofi)*

Hatuwezi kusema sisi ni kisiwa kama nchi. Leo wenzetu wa Kenya, Serikali iliyoko madarakani nadhani mmesikia kwenye vyombo vya habari, Majaji zaidi ya 40 wapo nje pale ambapo si kitu cha kawaida na hasa ukichukulia kwamba watu wale ni mhimili wa tatu wa utawala wa nchi lakini leo unasikia pale na wengine wameamua kuacha kazi zao kwa sababu wanajua yatawakumba yale. Sasa *PCB* inatuambia nini kuhusu hili? Sasa hata viongozi wengine wanazungumza wanasema rushwa zetu tunazopokea ni ndogo ndogo, rushwa kubwa zipo kwenye mikataba, Viongozi wa Serikali!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namshauri Mheshimiwa Rais kwamba, umefika wakati Kitengo hiki cha *PCB* kiondolewe chini ya Ofisi yake. Kwa sababu kitendo cha *PCB* kuendelea kuwa chini ya Ofisi ya Rais, kinawanyima haki ya kufanya kazi kwa uhuru zaidi maana baadhi ya watuhumiwa ni watu ambao ni wateuliwa na Rais. Kwa hiyo, hawawezi kwenda kuwashughulikia watu hao kwa sababu ni lazima wapate kibali cha Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema pamoja na mafanikio yote ambayo tumekwishayapata tatizo la rushwa hata kwenye vitabu vya dini wanasema hiyo ni dhambi. Kwa hiyo, lazima suala la rushwa lipewe msisitizo na msimamo mpya. Kwa hiyo, nilikuwa namshauri na namwomba Mheshimiwa Rais kwamba, amefanya kazi kubwa sana lakini kazi hii inaweza kutiwa dosari na vitendo vya rushwa ambavyo wananchi wanaviona. Sifanyi biashara leo hii nikawa nahodhi mali ambayo hailingani na hizi posho na mishahara ya Bunge, hizo pesa nyingine natoa wapi? Maana tunachosema si mtu kuwa na mali tunachosema hii mali inapatikana kihalali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunachosema, mimi nikisimama hapa kama Mbunge, nataka nijitazame mwenyewe, mimi kama Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Jimbo la Musoma, napokea rushwa na kutoa rushwa kiasi gani kabla sijasema? Maana hata wakati mmoja Serikali iliamua kufanya utaratibu wa kupiga kura za kuwatambua majambazi na wala rushwa na mtindo huo ulisaidia kwa sababu tuliweza kujua majambazi ni watu gani na wala rushwa ni watu gani na hatukusubiri mpaka upatikane ushahidi, ndiyo utaratibu wa kuendesha mambo. Tunazungumzia umoja wa nchi, hatuwezi kujenga nchi hii kwa watu

wengine kuwa na mapato ambayo kabisa kabisa tunajua hayakutokani na vipato halali. Kama mtu anafanya biashara zake anapata uwezesho wa kumwezesha kuwa na mali, nani anamkatalia? Lakini kwa nini tusifike mahali ambapo kwa kweli tukaona hili ni tatizo ambalo linaweza kuipeleka nchi hii mahali pabaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu kitu kimoja. Siku hizi tumekuwa waoga sana kuzungumzia mambo ya nchi maana tukisema tunaambiwa kwamba aah, wewe mtu wa kizamani, mtu wa Azimio la Arusha, lakini maadili yaliyokuwepo ndani ya Azimio la Arusha ndiyo maadili ambayo yalifanya nchi hii ikawa salama. Kwamba watu wafike mahali ambapo watakuwa na imani na sisi tunaowawakilisha hapa na ukisimama mtu asi-*question* ile *integrity* yako, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilidhani nizungumzie kuhusu hili tatizo la rushwa ambalo nadhani ndiyo tatizo kubwa ninaloliona kwamba pamoja na mafanikio mengi ambayo tumeyapata lakini ni lazima sasa tujue huu ndiyo uozo utakaosababisha nchi yetu ishindwe kwenda. Kuna mikataba mingi humu ukitaka kuifuatilia wakati mwingine ukijaribu kuzungumza wanasema kwa bahati mbaya, hakuna bahati mbaya katika kutekeleza kazi ya nchi hii. Kama mtu anafanya bahati mbaya akae pembeni asiye na bahati mbaya afanye kazi hiyo. Nataka niseme kwa dhati kwamba, Mheshimiwa Rais ana msimamo wa dhati, si mpenda madaraka wala utajiri na hilo wote tunalikubali ila tunasema na sisi tujitazame tunamsaidia Rais kweli kupambana na rushwa au tunataka hii kazi aifanye peke yake? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, huyo ni mchangiaji wetu wa mwisho. Wiki iliyopita Mheshimiwa Spika, aliwataja wenzetu wawili Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro na Mheshimiwa Tatu Ntimizi kwamba, walikuwa wamerejea kutoka kuhiji. Sasa naona leo nimtaje mwingine Mheshimiwa Hashim Saggaf,ambaye pia na yeye amerejea kutoka huko. Basi naomba wote niwakaribishe tena hapa nyumbani mwendelee tuwe pamoja katika shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.35 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 18 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*